
SportPesa
JACKPOT BABA LAO!
TZS. 233,880,320
CHEZA SASA KWA 1000/= TU!
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



UKURASA 3

**MABAKI** ya Panya Magawa kuhifadhiwa Makumbusho Taifa


HOTUBA Jumanne Mei 31, 2022 Nipashe 11

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM

BAJETI YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM KWA MWAKA 2022/2023

Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima (Mb)

Mhe. Mwanaidi Ali Khamis (Mb)

Dkt. Zainab Chaula

Amon Mpanju

UKURASA 11

Jumanne Mei 31, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580962
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



UKURASA 2, 11, 12, 13, 14, 15 & 16

# Mabilioni yatengwa Vita dhidi ya ukatili

- 01 Wanawake kuwezeshwa kiuchumi na kiuongozi
- 02 Utoaji huduma za msingi wenye mahitaji maalum
- 03 Kodi zinazokwamisha ukuaji biashara kufutwa
- 04 Usuluhishi migogoro ya ndoa na kisaikolojia
- 05 Huduma za wazee na ujenzi wa masoko mikoani
- 06 Huduma watoto wanaoishi mazingira hatarishi
- 07 Ajira kwa maofisa ustawi wa jamii zinakuja

# Kikokotoo bado mjadala

UKURASA 2



# Aliyeua mke naye akutwa kajiua kwa risasi

UKURASA 3

**MICHEZO** MO ANGURUMA TENA SIMBA UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na baadhi ya wabunge, kutoka kushoto ni Mbunge wa Morogoro Kusini, Hamisi Shaban Taletale na Mbunge wa Viti Maalumu, Khadija Shaaban Taya, bungeni jijini Dodoma. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

# Mabilioni yatengwa vita dhidi ya ukatili

**Na Romana Mallya,** DODOMA

WIZARA ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum imeliomba Bunge kuidhinishia Sh. bilioni 43.4 ili kutekeleza vipaumbele vinane kwa mwaka wa fedha 2022/23 ikiwamo kukabiliana na ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto, upungufu wa maofisa jamii na kujenga masoko ya machinga nchini.

Waziri wake, Dk. Dorothy Gwajima, aliwasilisha hoja hiyo bungeni jijini hapo jana alipowasilisha makadirio ya mapato na matumizi ya wizara hiyo kwa mwaka ujao wa fedha, akisisitiza umuhimu wake katika kutekeleza vipaumbele hivyo ili kuboresha utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii.

**USAWA KIJINSIA**

Alisema wizara inakwenda kuratibu afua za kukuza usawa wa kijinsia, uwezeshaji wanawake kiuchumi na kiongozi na kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake, watoto na wazee.

"Pili; wizara inakwenda kukuza ari ya jamii kushiriki katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo iliyoibuliwa ngazi ya jamii. Tatu; kutambua na kuratibu makundi maalum wakiwamo wafanyabiashara ndogo (machinga) ili kuboresha mazingira ya biashara zao," alisema.

Dk. Dorothy alisema wizara kwa kushirikiana na wizara zingine inakwenda kuratibu mchakato wa utambuzi wa machinga kwa kuwapa vitambulisho, kuondoa kodi zilizokuwa zinakwamisha ukuaji wa biashara zao, kutenga na kujenga miundombinu ya masoko mikoa mbalimbali.

"Nne, kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ambapo kwa mwaka 2022/23 vyuo vinatarajia kupeleka wanafunzi 931 kujifunza mafunzo mbalimbali kwenye kampuni, mashirika na taasisi 334.

**WENYE MAHITAJI MAALUM**

"Kipaumbele cha tano ni kuratibu utoaji wa huduma za msingi kwa watu wenye mahitaji maalum, huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa na familia na huduma ya msaada wa kisaikolojia kwa manusura wa majanga mbalimbali na makundi mengine yenye uhitaji katika jamii.

"Sita; kuratibu na kuwezesha upatikanaji wa huduma za ustawi wa jamii kwa wazee.

"Kipaumbele cha saba ni kuratibu na kusimamia afua za upatikanaji wa haki za mtoto, ulinzi na malezi chanya ya watoto na cha nane ni kuimarisha ushiriki na mchango wa mashirika yasiyo ya kiserikali katika maendeleo ya Taifa," Dk. Dorothy alisema.

Waziri huyo alisema ili kutekeleza vipaumbele hivyo, wizara kwa mwaka 2022/23 imekadiria kutumia Sh. bilioni 43.4 zitakazotumika kutekeleza majukumu ya wizara ikiwa ni pamoja na kuwezesha uendeshaji wa ofisi na utekelezaji wa miradi wa maendeleo.

"Baadhi ya maeneo yaliyotengewa fedha kwa mwaka 2022/23 ni pamoja na eneo la ukatili na masuala ya usawa wa kijinsia, Sh. bilioni 2.65 zimetengwa kwa ajili ya kuratibu utekelezaji wa afua za kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto ikiwamo kampeni ya 'Twende Pamoja, Ukatili Tanzania Sasa Basi', " alisema.

Pia alisema fedha hizo zitatumika kwa ajili ya kusambaza Mwongozo wa Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi, kuwezesha utekelezaji wa ahadi za nchi kuhusu Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa na kuwezesha ushiriki wa wanawake katika maonyesho ya kitaifa na kimataifa.

**BAJETI WATOTO**

Waziri Dorothy alisema eneo la watoto limetengewa Sh. bilioni 2.36 kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa huduma kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na marekebisho ya tabia kwa watoto waliokinzana na sheria, kukarabati mahabusu za watoto katika mikoa ya Mbeya na Arusha, kujenga mahabusu ya watoto mpya katika Mkoa wa Mwanza.

"Kuratibu utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Mtoto (2021/22 - 2025/26) na kuanzisha vituo vya kijamii vya malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto," alisema.

**WAZEE**

Waziri huyo alisema eneo la wazee limetengewa Sh. bilioni 1.45 kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa huduma za ustawi kwa wazee wasiojiweza katika makazi ya wazee 14 na ukarabati wa majengo na miundombinu katika makazi ya wazee ya Ipuli na Njoro.

Alisema eneo la taasisi na vyuo limetengewa Sh. bilioni 5.6 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo na miundombinu katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Taasisi ya Ustawi wa Jamii (Kampasi ya Kisangara) na vyuo vinane vya Maendeleo ya Jamii.

Pia alisema eneo la uratibu wa mashirika yasiyo ya kiserikali limetengewa Sh. milioni 642.3 kwa ajili ya ufuatiliaji wa mashirika 1,000 katika kanda tano, kuendesha mfumo wa kielektroniki wa usajili wa mashirika, kuwezesha vikao vya bodi ya uratibu wa mashirika hayo, kuyasajili na kuratibu Jukwaa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

"Eneo la maendeleo ya jamii limetengewa Sh. milioni 160.2 kwa ajili ya kutekeleza kampeni ya kitaifa ya kuamsha ari ya jamii kuhusu ujenzi wa nyumba bora za gharama nafuu kwa kutumia teknolojia rahisi katika mikoa 26 ya Tanzania Bara.

"Eneo la ufuatiliaji na tathmini, fedha zilizotengwa ni Sh. milioni 200 kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa mipango, programu na miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika taasisi, vyuo na vituo vya ustawi vilivyo chini ya wizara," alisema.

Wizara hiyo mpya imeanzishwa na Rais Samia Suluhu Hassan, akiigawa kutengeneza wizara mbili, liyokuwa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

# Kikokotoo bado chaleta mjadala

**Na Jenifer Gilla**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimesema licha ya kikokotoo kipya cha mafao kufanyiwa maboresho, lakini maboresho hayo hayatawasaidia wastaafu badala yake wataendelea kuumia.

Chama hicho katika taarifa iliyotolewa jana na Msemaji wa Sekta ya Uwekezaji, Mashirika ya Umma na Hifadhi ya Jamii wa ACT-Wazalendo, Mwanaisha Mndeme, kilieleza kuwa kikokotoo hicho kinaporomosha mafao kwa kuwa kinatumia kanuni za mwaka 2018 za 1/580 badala ya za sasa za 1540.

Alisema kanuni za zamani ilikuwa ni miaka 15.5 na malipo ya mkupuo asilimia 50, pensheni ya mwaka ikiwa Sh. milioni 9.6 na malipo ya mkupuo/kiinua mgongo Sh. milioni 74.4 na pensheni ya mwezi (posho) ilikuwa Sh. 400,000.

Mndeme alisema kanuni mpya ambayo ni ya mwaka 2018 (na marekebisho ya 2022), kikokotoo cha 1/580, miaka 12.5, malipo ya mkupuo ni asilimia 33, pensheni ya mwaka itakuwa Sh. milioni 8.937, malipo ya mkupuo/kiinua mgongo itakuwa Sh. milioni 36.8 huku pensheni ya kila mwezi (posho) itakuwa Sh. 499,034.

Alisema kwa muktadha huo kikokotoo kipya kinapunguza mafao ya mtumishi aliyestaafu ya mwaka kwa asilimia 6.9, malipo ya mkupuo ya kiinua mgongo kwa asilimia 50.5, ikilinganishwa na kanuni za awali.

Alisema pia kinafupisha umri wa kuhudumiwa mstaafu kwa takribani miaka mitatu kutoka miaka 15.5 ya awali hadi 12.5.

Alitahadharisha kuwa kutakuwa na ongezeko kwenye posho ya kiinua mgongo cha kila mwezi kwa asilimia 24.7, lakini kwa kukokotolewa jumla ya mafao atakayepokea kwa miaka 12.5 yanaongezeka kwa asilimia 0.6 pekee kutokana na kufupishwa kwa miaka mitatu tofauti na awali.

"Hatupaswi kuwaadhibu wazee wetu kwa kukubali kanuni hizi kandamizi zinazoenda kuwapunja mafao yao na kufupisha muda wa kuwahudumia kwa kuwakadiria kifo mapema zaidi," alisisitiza Mndeme.

Kutokana na hali hiyo, aliitaka serikali kuhakikisha wafanyakazi wastaafu wanufaika na michago yao kwa kulipa madeni yote inayodaiwa na mifuko ya hifadhi ya jamii kwa mkupuo mmoja ili kuiwezesha mifuko kujiendesha na kuhudumia wateja wake kwa wakati.

Pia, aliitaka serikali kurejesha kanuni za zamani za mwaka 2017, menejimenti za mifuko ya hifadhi ya jamii kufanya uwekezaji wa miradi itakayoleta faida kuendana na mahitaji ya wanachama.

Alivitaka vyama vya wafanyakazi nchini vishikamane kama ilivyofanya miaka mitatu nyuma kupinga udhalimu huo.

Hivi karibuni baada ya Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye ulemavu), Profesa Jamal Katundu, kutangaza kanuni mpya za kikokotoo hicho, Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wafanyakazi (TUCTA), Tumaini Nyamkokya, alisema upangaji wa kanuni hizo umekuwa shirikishi na umeridhiwa na wadau, hakuna eneo lililofichwa.

Hatua hiyo pia ilipongezwa na wadau mbalimbali kwa kusema serikali imesikia malalamiko yao na kuyafanyia kazi.

# Mabaki ya panya Magawa kuhifadhiwa Makumbusho

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

SERIKALI kupitia Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), inakusudia kurudisha mabaki ya panya Magawa nchini Tanzania kwa ajili ya kuhifadhiwa katika Makumbusho ya Taifa ili kutambua mchango wake kutokana na panya huyo kuliletea taifa heshima pamoja na sifa nje ya nchi.

Magawa ambaye alikuwa panya buku mkubwa kutoka Tanzania alikufa na kuzikwa nchini Cambodia, Januari mwaka huu baada ya kujitolea kuokoa maisha ya watu kupitia kazi yake ya kutambua mabomu hatari yaliyokuwa yametegwa ardhini nchini humo na kujizolea sifa kubwa.

Panya Magawa amekuwa wa kwanza kupewa nishani ya dhahabu, kutokana na uwezo wake kubaini mabomu yaliyotegwa ardhini pamoja na silaha nyingine 28 ambazo hazijalipuliwa nchini Cambodia.

Akizungumza katika mahafali ya 39 ya kati kati ya mwaka wa msomo wa 2021/2022 iliyofanyika Kampasi ya Mazimbu, Makamu Mkuu wa SUA, Profesa Raphael Chibunda, alisema tayari wameshaanza mazungumzo na serikali ya nchi hiyo ambayo Panya Magawa alikufa na kuzikwa kwa ajili ya kurudisha nchini mabaki yake.

"Mazungumzo mpaka sasa yanakwenda vizuri," alisema Profesa Chibunda kwenye mahafali hayo.

Alisema lengo la kurudisha mabaki ya panya Magawa ni kumpa heshima yake kwa ajili ya kazi kubwa aliyofanya kwa manufaa ya taifa pamoja na kutunza historia yake katika makumbusho ya taifa.

Kwa mujibu wa Kituo cha Utafiti cha Mradi wa Panya Buku cha Apopo, kilichoko Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Magawa kutokana na ushujaa wake, Septemba 2020, alikabidhiwa rasmi Medali ya Dhahabu iliyotolewa na Shirika la Hisani ya Wanyama la Uingereza (PDSA) - tuzo ya juu zaidi ya ushujaa ambayo mnyama anaweza kupokea.

Pia aliwezesha kugunduliwa kwa zaidi ya mabomu 100 ya kutegwa ardhini nchini Cambodia na vilipuzi vingine na alisherehekea siku yake ya kuzaliwa Novemba 2021 kwa kutumiza umri wa miaka nane.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kituo hicho, Magawa alistaafu akiwa nchini Cambodia kutokana kupungua kwa uwezo wake wa kunusa na kubaini mabomu yaliyotegwa ardhini.

Hata hivyo, Januari 11, 2022, kituo hicho kiliitaja habari ya kusikitisha kwamba 'Hero RAT' Magawa aliaga dunia kwa amani wiki moja kabla ya siku hiyo na kuzikwa nchini humo.

Kwenye mahafali hayo jumla ya wahitimu 209 kati yao wanawake 62 walitunukiwa vyeti na Mkuu wa Chuo Kikuu hicho, Jaji mstaafu Joseph Warioba.



Meneja wa karakana ya Taasisi ya Uhandisi na Usanifu Mitambo Tanzania (TEMDO), Nicas Bernard (watatu kulia), akimwonyesha Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji, Dk. Ashatu Kijaji pamoja ujumbe wake moja ya kifaa cha mashine ya kuchakata miwa kinachotengenezwa na taasisi hiyo juzi, alipotembelea kiwanda hicho kuona namna wanavyofanya kazi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Mume aliyeua mke akutwa kajiua

## ●Simulizi ya tukio zima yasimuliwa na familia

**Na Richard Makore,**
MWANZA

SIKU mbili baada ya mauaji ya Swalha Salmu (26), kutokea jijini Mwanza, wadogo zake wamesimulia mkasa mzima ulivyokuwa kabla ya kifo chake Jumamosi iliyopita usiku nyumbani kwake eneo la Buswelu, wilayani Ilemela.

Mdogo wake wa watu marehemu, Suleira Salmu, amesimulia mkasa mzima na namna alivyoshuhudia dada yake akimiminiwa risasi saba.

Akizungumza jana nyumbani kwao eneo la Kirumba, Suleira alisema siku hiyo, shemeji yake ambaye alikuwa mume wa dada yake alitoka kwenye biashara zake wilayani Ukerewe na kufika kwake saa 1.45 usiku.

Hata hivyo, hakumkuta mkewe nyumbani, lakini muda mfupi naye alifika akitokea nyumbani kwao Kirumba.

Alipoingia chumbani, alisikia wakigombana na mume wake na muda mfupi, mdogo wake akiwa jikoni na mfanyakazi wa ndani walisikia milio ya risasi.

Milio hiyo ilimshtua na kukimbilia ndani, lakini alikuta mlango wa chumbani umefungwa na baadaye akaendelea kusikia risasi zikiendelea kupigwa mfululizo.

Alisema baada ya muda mfupi shemeji yake alifungua mlango na kutoka nje na yeye alipoingia ndani alimkuta dada yake amelala kitandani huku akiwa anatokwa damu nyingi.

Ilimbidi akimbie kuita majirani ili kumsaidia dada yake, lakini walikataa kwa kuwa siku za nyuma shemeji yake aliwakataza kufika kwake kwa madai wao walikuwa wakichangia ndoa yake kuwa na migogoro.

Baada ya kukosa msaada, alikimbia kwa madereva wa bodaboda na kufanikiwa kuwapata wawili, lakini hata hivyo walipofika nyumbani walikataa kumshika marehemu dada yake na kusimama mbali.

Kutokana na kukosa msaada, alisema ilibidi amuombe mama mmoja jirani yake amsaidie na wakaweza kumbeba hadi sebuleni kabla ya kupiga simu kwa baba yake ili aje kuwasaidia.

Baba yake alipofika na watu wengine, walibeba mwili wa marehemu hadi Kituo cha Polisi cha Kirumba kwa ajili ya kuandika maelezo.

Kwa upande wake, mdogo wake wa pili marehemu, Arafa Salmu, alisema dada yake na mume wake walikuwa na ugomvi wa kwa zaidi ya wiki moja na nusu.

Alisema chanzo kikubwa cha ugomvi wao ilikuwa shemeji yake kumwonea wivu wa kupitiliza na kwamba baadhi ya majirani waliwahi kumpigia simu na kumwambia wamemwona mke wake akiwa katika hoteli moja ya jijini Mwanza.

Alisema ugomvi huo ulimalizika na mume aliaga na kurudi katika biashara zake Ukerewe, kabla ya kurudi tena siku ya Jumamosi usiku na kufanya mauaji hayo.

Arafa anasema mara kadhaa dada yake alikuwa akilalamika kwamba mume wake alikuwa akimpigia simu na kumtukana na alikuwa amechoka na matusi hayo.

Mdogo wake huyo anasema wiki moja iliyopita dada yake alipata kazi ya kwenda kupamba maharusi mkoani Shinyanga na kumuaga mume wake.

Hata hivyo, licha ya kumuaga mume wake ambaye alikuwa Ukerewe kwa njia ya simu na dada yake kwenda Shinyanga kwenye kazi hiyo, aliendelea kumpigia simu na kumtukana.

Alisema hali hiyo ya kutukanwa ilimkasirisha dada yake na kuamua kutopokea simu za mume wake na siku ya Jumamosi mume huyo alirudi Mwanza akitokea Ukerewe na dada yake alikataa kwenda kumpokea na gari lake.

Alisema mara kadhaa alikuwa akishuhudia wakipigana nyumbani kwao kwa kuwa alikuwa akiishi nao.

Mama mzazi wa marehemu, Tiba Mohamed, alikiri mtoto wake kuwahi kumsimulia kuhusu ugomvi wa mara kwa mara na mume wake.

Alisema siku ya tukio mtoto wake alienda kumsalimia nyumbani kwao eneo la Kirumba na wakati akiwa huko, alipigiwa simu na mume wake akimuomba awahi kurudi nyumbani ili akampikie chakula cha jioni kwa kuwa alikuwa hakula kitu tangu asubuhi.

Baadhi ya marafiki zake walisema Swalha aliwahi kuolewa na kuachika mara tatu ingawa hawakusema chanzo cha kuachika kilikuwa ni nini.

"Mimi namfahamu marehemu alikuwa rafiki yangu sana amewahi kuolewa mara tatu na kuachika, lakini hakuwahi kuniambia sababu ya kuolewa mara kwa mara na kuachika," alisema rafiki yake ambaye aliomba jina lake lisiandikwe.

Swalha alipigwa risasi na mume wake na kufariki dunia usiku wa Jumamosi iliyopita baada ya kutokea ugomvi wa mara kwa mara.

Rafiki yake huyo alisema kabla ya mwanamume huyo kufanya mauaji hayo alituma ujumbe mfupi wa simu kwa marafiki zake kwamba alikuwa amepanga kumuua mke wake.

Mwanamke huyo alipigwa risasi saa 2:00 usiku Jumamosi nyumbani kwao eneo la Buswelu ikiwa ni miezi mitano tangu wawili hao kufunga ndoa.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, Ramdhan Ng'anzi, tukio hilo lilitokea nyumbani kwao baada ya kuwapo na mgogoro wa muda mrefu tangu wafunge ndoa yao.

Akizungumza na Nipashe jana Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Mwanza, Mairi Makori, alisema mwanaume aliyefanya mauaji hayo aliyejulikana kwa jina moja la Said mwili wake umeokotwa kando ya Ziwa Victoria ukiwa na majeraha ya risasi.

"Ni kweli mwili wa mtu anayedaiwa kufanya mauaji hayo umeokotwa na kutokana na picha tulizonazo atakuwa ni yeye," alisema.

Alisema wanasubiri ndugu zake ili waende kutambua mwili huo.

Mwili wa marehemu Swalha ulizikwa jana jijini Mwanza.

# Mahakama yapokea kielelezo meno 660 ya tembo

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imepokea vipande 660 vya meno ya tembo kama kielelezo cha upande wa Jamhuri katika kesi ya uhujumu uchumi inayomkabili mfanyabiashara, Ally Anguzuu raia wa Guinea na wenzake 10.

Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rhoda Ngimilanga wa Mahakama hiyo, alifikia uamuzi huo wa kupokea kielelezo hicho baada ya kupitia hoja za pande zote mbili kutokana na upande wa utetezi kupinga kupokelewa kwa meno hayo.

Pingamizi hilo linatokana na madai kwamba sheria haikufuatwa wakati wa uwasilishwaji wa kielelezo hicho na hakimu katika uamuzi wake alitupilia mbali hoja hiyo.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Juni 2, 2022, shahidi wa kwanza wa upande wa mashtaka Wilfred Ollomy ambaye ni mtunza vielelezo kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii anatarajiwa kuendelea kutoa ushahidi wake.

Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni mfanyabiashara Victor Mawala, Haruni Abdallah, Abbas Hassan, Solomoni Mtenya, Khalfani Kahengele, Ismail Kassa, Juma Buguma, Kassim Saidi, Peter Nyachiwa, John Buhanza na Mussa Abdallah, wote wakazi wa Dar es Salaam.

Katika kesi hiyo, washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka ya kujihusisha na nyara za serikali bila kuwa na kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Wanyamapori, ambazo ni meno hayo yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 4.6.

Washtakiwa hao wanadaiwa kuwa na mtandao mkubwa wa uhalifu wa ujangili ambao unajihusisha kuuza na kununua, kupokea na kuhamisha, kusafirisha nyara za serikali ambazo ni meno ya tembo.

# Serikali yashauriwa kuweka mwongozo madini kimkakati

**Na Salome Kitomari**

SERIKALI imeshauriwa kuwa na mwongozo mmoja utakaoelekeza nini kifanyike katika kipindi dunia inabadilika kutoka matumizi ya nishati ya mafuta, gesi na makaa ya mawe kwenda nishati jadidifu (renewable energy) ambayo ni rafiki kwa mazingira.

Aidha, imeshauriwa kuwa na msimamo kuangalia njia ya kupita kwenda kwenye mabadiliko ya nishati, kwa kuwa nchi zilizoendelea zilizoanza mabadiliko hayo zilichafua mazingira na zilishanufaika na mafuta, gesi na makaa ya mawe na sasa inazitaka nchi zinazoendelea kuacha kutumia.

Kwa mujibu wa mpango wa taifa ujulikanao kama National Determined Contribution (NDC) wa Julai 2021, Tanzania itapunguza hewa ukaa kwa asilimia 30 hadi 35 ifikapo 2030, Afrika inachangia asilimia nne ya hewa ukaa duniani huku wachangiaji wakubwa wakiwa ni Marekani na China.

Ushauri huo ulitolewa hivi karibuni na mjiolojia, Bosco Tindyebwa, wakati akizungumza na gazeti hili kuhusu madini ya kimkakati na namna nchi inaweza kupita salama kipindi cha mpito kuelekea kuingia kwenye nishati jadidifu.

Alisema ni lazima kuangalia sera, kanuni na mipango iliyoko ili kuwa na kauli ya nchi namna ambavyo itaenda kwa kipindi ambacho dunia inajiondoa kwenye matumizi ya nishati hizo, kwa kuwa inagusa usalama wa nchi, sekta za nishati na madini.

Tindyebwa ambaye ni mshauri wa madini, alisema kwa muda nchi imekuwa tegemezi kwenye vyanzo vya nishati visivyo vyake kama mafuta na kwamba ndiyo maana jambo lolote likitokea la upatikanaji wa bidhaa nchi inayumba.

"Kwa bahati nzuri tunapohama kutoka kwenye vyanzo hivi na kwenda kwenye utegemezi zaidi wa nishati jadidifu, nchi imejaliwa rasilimali za kutosha kama madini ya kila aina ikiwamo madini ya kimkakati, jua, upepo, mawimbi na upepo wa bahari na kinyesi cha wanyama," alisema.

Alitaja mikoa yenye viwango vya juu vya jua, joto ardhi na upepo ni Kilimanjaro, Njombe, Simiyu, Manyara, Singida, Dodoma, Songwe, na kwamba kila kilomita ya mraba ya ardhi inaweza kuzalisha kiwango cha juu cha nishati kwa upepo na jua.

"Tanzania ina uwezo wa kuingia kwenye mabadiliko ya nishati kama wazalishaji kuliko wategemezi kama ilivyokuwa kwenye mafuta, ni muhimu watunga sera wakaelewa na kuangalia namna ya kutumia, siyo kwa matumizi yetu pekee bali kibiashara zaidi," alisema Tindyebwa.

Mtaalamu huyo alisema ni lazima nchi kuangalia uhusiano mabadiliko yaliyoko na madini ya kimkakati (critical minerals) ambayo yanatumika kuzalisha nishati jadidifu, mathalani matumizi ya magari ya umeme yanahitaji madini mengi yanayopatikana nchini.

"Pale ambako nchi nyingine zimeshaanza kutengeneza mahitaji ya madini haya lazima kujiandaa, tuna madini ya nickel Kabanda na cobalt, kuna miradi mingi inayoendelea ambayo tuna uwezekano mkubwa wa kupata madini kama haya kwenye maeneo mengi nchini kama graphite (kinywe) ambayo yapo kwa wingi Mahenge (Morogoro) na Lindi," alisema.

"Nchi tuna haya madini ambayo yameshagunduliwa na yataendelea kugunduliwa, tunapaswa kujiandaa na kujipanga ili tuwe wazalishaji wazuri ambao tutanufaika kwa kuwa yanahitajika sana duniani. Mahitaji ya madini ya kimkakati ni makubwa sana duniani kwetu bado hatujayaelewa ila wenzetu wameshayaona na wanayakimbilia kwa kuwa yanahitajika sana," alisema.

Katika mkutano wa COP26 nchi za Afrika ziliomba muda zaidi kwenye kukabili mabadiliko ya tabia nchi, na katika mkutano wa COP27 utakaofanyika nchini Misri zitatakiwa kueleza hatua iliyofikiwa.



Gari la Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Nchini (TANROADS), Mhandisi Rogatus Mativila yakipita juu ya daraja la Chang'ombe kuashiria kuanza kutumika kwa njia moja katika daraja hilo, jijini Dar es Salaam ili kupunguza msongamano wa magari Barabara ya Nyerere. **PICHA: SHUKURU SENKORO**

# Maimu kuanza kujitetea leo

**Na Grace Gurisha**

ALIYEKUWA Mkurugenzi wa Mamlaka ya Vitambulisho (NIDA), Dickson Maimu, anayetuhumiwa kwa kesi ya uhujumu uchumi pamoja na wenzake wanne, anatarajiwa kuanza kujitetea leo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, baada ya kesi hiyo kuahirishwa mara mbili.

Awali, Maimu alishindwa kuanza kujitetea mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Evodia Kyaruzi kwa sababu mawakili kutoka ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini wanayoendesha kesi hiyo kupewa kazi maalum na kushindwa kufika mahakamani.

Hayo yalielezwa na Wakili wa Serikali kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Nickson Shayo na Wakili wa Maimu, Wabeha Kung'e.

Shayo alidai kuwa, kesi ililetwa kwa ajili ya kuendelea kusikilizwa kwa upande wa utetezi, lakini mawakili kutoka ofisi ya DPP ambao wanashirikiana nao katika kesi hiyo wamepata dharura kufika mahakamani na kuomba ahirisho.

Kung'e alibariki ahirisho hilo kwa kudai kuwa alipigiwa simu na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ladslaus Komanya na kumweleza kwamba walitaka kuja kuendelea, lakini wamepewa kazi maalum.

"Kwa mazingira haya hatuna pingamizi kwa ombi la upande wa mashtaka la kutaka kesi iahirishwe," alidai Kung'e.

Awali, Maimu aliieleza mahakama hiyo kuwa atakuwa na mashahidi sio chini ya 20 na vielelezo 10, baada ya upande wa mashtaka kuleta mashahidi 26 na vielelezo 45 na hakimu kujiridhisha kuwa washtakiwa wana kesi ya kujibu.

Mbali na Maimu washtakiwa wengine ni aliyekuwa Mkurugenzi wa Sheria wa mamlaka hiyo, Sabina Raymond, Meneja wa Biashara, Xavery Kayombo, Aveln Momburi na George Ntalima.

Shahidi wa mwisho katika kesi hiyo, Ofisa wa TAKUKURU, Emmanuel Koroso, alidai kuwa Mkurugenzi wa Sheria wa Mamlaka hiyo, Sabina Raymond alishuhudia utiaji saini mkataba ulioingizia serikali hasara ya Dola za Marekani 551,500.

Akiongozwa na Wakili Komanya, Koroso alidai wakati akifanya mahojiano na Sabina alimweleza kuwa yeye ndiye alikuwa msimamizi wa masuala yote yanayohusu sheria NIDA ikiwamo kusimamia na kushuhudia utiaji saini wa mikataba mbalimbali.

Washtakiwa hao wanakabiliwa na mashtaka mbalimbali ikiwamo kuisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni 1.175.

Mwisho

# Chongolo asisitiza usimamizi miradi yenye tija

**Na Maulid Mmbaga**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amewataka viongozi na wasimamizi wa miradi ya maendeleo kutumia vizuri fedha zinazotolewa kutekeleza miradi ya kipaumbele inayowagusa wananchi kwa ukaribu na inayokamilika kwa asilimia 100.

Alitoa wito huo jana wilayani Kishapu mkoani Shinyanga alipokuwa akikagua ujenzi wa daraja linalounganisha kata ya Ipeja na Itilima, mkoani humo.

Alisema miundombinu ikijengwa nyakati za mvua ikinyesha inasaidia kuwa na ubora unaoendana na mazingira, huku akipongeza Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) kwa kusimamia na kukamilisha ujenzi wa daraja hilo kwa wakati.

"Miezi mitano changamoto imeisha wananchi wanaanza kulitumia maisha yanawanyookea, hii ndiyo miradi tunayoitaka sio mradi unakuja mnapewa Shilingi bilioni moja, mnapeleka kwenye miradi 40 halafu mnapeleka Sh. milioni 20 hiyo zama imepita, tunataka pesa zielekezwe kwenye mradi unaokwenda kukamilika kwa asilimia 100," alisema Chongolo.

Aliongeza kuwa fedha zinazotolewa na kwenda kufanya vitu vidogo tija yake haionekani, alisisitiza idara na viongozi mbalimbali nchini kuelekeza nguvu kubwa katika utekelezaji wa miradi yenye ulazima kwa wananchi kwa wakati uliopo na ambayo utekelezaji wake utafikia asilimia 100.

Kwa upande wake Meneja wa TARURA Wilaya ya Kishapu, Wilson Gutta, alisema daraja hilo lenye urefu wa mita 32.2 na upana wa mita 7.1 liligharimu zaidi ya Sh. milioni 486 kati ya milioni 500 zilizokisiwa kutumika katika utekelezaji wa mradi huo.

"Kukamilika kwa mradi huu utakuwa na manufaa makubwa hasa kwa wakulima wa mpunga ambao wanahitaji kusafirisha mazao yao ili kufikia masoko makubwa yaliyoko katika Manispaa ya Shinyanga," alisema Gutta.

# Vituo 8 kujaza gesi za magari kujengwa

**Na Salome Kitomari**

SERIKALI imesema inajipanga kujenga vituo vikubwa vinane wa kuuza gesi kwenye malori jijini Dar es Salaam, huku ikisambazwa kupitia mikoa mingine hadi Uganda ili kukuza uchumi.

Hayo yalisemwa juzi na Katibu Mkuu Wizara ya Nishati, Felchesmi Mramba, wakati akihojiwa na ITV kwenye kipindi maalum kuhusu mafanikio katika sekta ya nishati.

Alisema vituo vikubwa vitajengwa maeneo ya hosteli za Magufuli za Chuo Kikuu cha Dar Es Salaam (UDSM), Mlalakuna na Ubungo Maziwa na Msasani Beach.

Pia vitajengwa vituo vidogo eneo la Feri kwa ajili ya magari ya ukanda huo, Muhimbili, Kibaha, Ubungo karibu na kituo cha mwendokasi kwa kuwa wamekubaliana na TAMISEMI kuwa awamu ya pili na tatu yatakayoletwa yawe ya mfumo wa gesi.

Vile vile, alisema kampuni 18 zimeonyesha nia ya kujenga vituo vya kuuza gesi ya magari, huku wengine ni wenye vituo ambao wanataka kuweka huduma hiyo ili kuwa na wengi wanaouza nishati hiyo.

"Nishati ya gesi haiwezi kuwa kwa Dar es Salaam pekee bali tunatarajia kuisafirisha kupitia magari yenye mitungi na kujazwa kwenye vituo, ili wananchi waweze kutumia. Tunafanya haya kwa haraka sana kuhakikisha huduma hii inasambaa," alisema.

"Wakati haya yanaendelea taratibu za kisera zinaendelea, wakati Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imeanza kutengeneza bei elekezi za gesi ili kuweka usawa, huku tukifuatilia wanaotengeneza magari wanafuata viwango, kusiwe na upungufu wa kiusalama, tunaamini magari mengi yatabadilishwa," alisema.

"Tukipeleka gesi tutapata mapato pia nchini, gesi itafungua fursa nyingi za uchumi. Mathalani magari ya Dangote yote yamebadilishwa yanatumia mfumo wa gesi ambao ni rahisi," alisema.

Katibu Mkuu huyo alisema gesi ina mfumo wa usalama kwa kuwa mtungi wake unawekwa kwenye buti na linapotokea tatizo kuna kifaa kinafunga, huku akieleza hatua zote za usalama zimezingatiwa.

Kuhusu faida za gesi alisema ni bei rahisi na kwa waliofunga wanasema matumizi ni asilimia 40, nishati inayopatikana nchini kirahisi na kwasababu ni raslimali ya nchi ni muhimu kuitumia.

**KUPELEKWA UGANDA**

Kwa mujibu wa Mramba, kwa sasa wako kwenye mazungumzo na Uganda, ili kusafirisha gesi kwenda nchini humo, lakini ipite kwenye miji ya Tanzania ili wananchi waweze kutumia.

"Rais ametoa maelekezo mahususi katika ujenzi wa bomba kwenda Uganda lisipite kwenye mkuza wa bomba la mafuta, bali lipite kwenye miji kama Kibaha, Morogoro, Dodoma, Singida, Nzega hadi Mwanza, Tunaamini litafungua fursa nyingi za kiuchumi," alisema.

Aidha, alisema kwa sasa mkazo unawekwa kwenye matumizi ya gesi nyumbani, itafungua fursa nyingi za kiuchumi na kwamba kwa sasa msisitizo mkubwa matumizi ya gesi nyumbani na kwenye magari.

VITUO VYA GESI

Alisema hadi sasa kuna vituo vichache vya kuuza gesi na kwamba kutokana na bei ya mafuta kupanda mwamko wa watu kuelekea kwenye gesi ni mkubwa, hali inayoashiria wengi wamebadilisha mfumo wa magari. "Hadi sasa kituo cha kubadilisha magari kiko Ubungo, lakini tunajenga vituo vikubwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Malalakua,"

**GRIDI YA TAIFA**

Alisema mafanikio yaliyopo gridi ya taifa inaunganishwa na Zambia, Kenya, Burundi na Rwanda na kwamba wako kwenye mazungumzo na Uganda kwenye mradi wa Mwanza-Masaka ili kuondoa nchi kuwa kisiwa cha nishati.

Alisema Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), limekamilisha ukarabati wa miundombinu na lengo ni wananchi kupata huduma hiyo kwa ukamilifu bila usumbufu.




Baadhi ya mawaziri wa serikali ya Zanzibar wakifuatilia kikao cha Baraza la Wawakilishi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# NEMC yaonya kelele nyumba za ibada

**Na Joseph Mwendapole**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limezionya nyumba za ibada na sehemu za burudani zinazotoa kelele nyingi kuacha kufanya hivyo kwenye makazi ya watu.

NEMC imesema hivi karibuni itaendesha operesheni ya kuwabaini na ikiwezekana kuchukua vifaa vyote vinavyotumika kutoa sauti kwenye maeneo hayo kukomesha hali hiyo.

Onyo hilo lilitolewa jana jijini Dar es Salaam na Mkurugenzi wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu malalamiko ya wananchi kuhusu kelele.

Dk. Gwamaka alisema hivi karibuni baraza limepokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi kuhusu kelele kutoka kwenye nyumba za ibada na maeneo ya burudani.

"Ongezeko la malalamiko kuhusu kelele limekuwa kubwa sana na inashangaza kwani tumefanya semina nyingi sana kwa viongozi wa dini kwa watendaji kata na mitaa na hata kwa wamiliki wa nyumba za starehe kama baa na kumbi za sherehe, lakini bado hali imezidi kuwa mbaya sana," alisema.

Alisema NEMC imefanya jitihada mbalimbali kuhakikisha hali hiyo inakoma ikiwamo kuwanyang'anya vifaa vya muziki vinavyopiga kelele kwenye baadhi ya baa na nyumba za burudani na kuwapiga faini, lakini bado.

Alisema siku za hivi karibuni kumetokea mlipuko mkubwa wa ujenzi wa nyumba za ibada na burudani jirani na makazi ya watu na wanapotumia vifaa vyao vya muziki husababisha kero kwa wananchi wa maeneo hayo.

"Kuna wananchi wanasema wamejengewa nyumba za ibada kwenye madirisha yao kabisa na wengine wamejenga jirani kabisa na shule. Tunajua viongozi wa dini ni wadau muhimu katika kudumisha amani kwenye jamii, lakini lazima wazingatie sheria na taratibu za nchi," alisema.

Alisema viongozi wa dini wanapaswa kuwa wa kwanza kutii sheria kwa kuhakikisha wanaweka viwango vya kelele vya chini ambavyo havisababishi kero kwa wananchi wa jirani.

"Inashangaza sana wakati mwingine mtu anaweka spika hadi nje ya kanisa, waumini unaowahubiria wako ndani sasa spika unaiweka nje ya kazi gani. Kila mtu ana uhuru wa kuabudu, lakini kuabudu kwako kusiathiri maisha ya mtu mwingine," alisema Dk. Gwamaka.

"Haitapendeza ifike wakati sisi NEMC twende kuwaadhibu viongozi wa dini kwasababu ya kelele ni vizuri sote tuzingatie sheria tusifike wakati tukawa kama nchi jirani walioweka masharti ya elimu kwa viongozi wa dini na wanafunga kabisa makanisa, tusifike huko," alisema.


Aliwataka wamiliki wa nyumba za starehe na zile za ibada kuweka mazingira ambayo sauti zitakuwa hazitoki nje ya majengo yao ili waweze kufanya ibada au starehe zao kwa muda wowote wanaotaka hata kama ni saa 24.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ukatili wa kijinsia tatizo kubwa

**JUZI** wabunge walipaza sauti kuhusu kukithiri vitendo vya ukatili nchini, vinavyogharimu maisha ya wengi huku wakiachwa na mateso kisaikolojia.
Wawakilishi wa wananchi hao walikuwa kwenye semina ya wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, wakitaka serikali na jamii kuja na njia za kukomesha ukatili huo kwa lengo la kuwa na kizazi chenye ustawi na kusichokuwa na maumivu kutokana na ukatili.
Katika semina hiyo iliyoandaliwa na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, aliwaeleza wabunge walivyopokea ujumbe kutoka kwenye mkoa fulani ukieleza jinsi babu alivyokuwa akimbaka mjukuu wake kwa mwaka mmoja.
Wabunge walisema kuna ukatili mwingi unaendelea kwenye jamii na sio kila mtu anaweza kwenda kuripoti, huku wakisema idadi ya madawati yaliyoko ni ndogo ikilinganishwa na kesi.
Wapendekeza lazima kuwe na msaada wa kisaikolojia kwasababu mtoto anapofanyiwa ukatili, kuna uwezekano wa kulipiza kwa wengine baadaye.
Kila siku kuna wastani wa matukio zaidi ya mawili yakitokea mikoa tofauti, ambayo yanahusu mtoto kubakwa na mtu wa karibu au wa mbali, wakati mwingine hadi mzazi.
Tukio la juzi ni la kijana kumuua mkewe mwenye umri wa miaka 26 waliodumu kwenye ndoa kwa miezi mitano, huku Arusha kuna mtu ameuawa na wananchi wenye hasira kali kwa madai ya kubaka wanawake kwa muda mrefu, kisha kujipaka mafuta ili watu watakapojaribu kumkamata wasiweze kutokana na mwili kuteleza.
Zipo jitihada nyingi zimefanywa na serikali ikiwamo kuunda kamati mbalimbali, pia kuanzisha dawati la jinsia kwenye vituo vya polisi, ili iwe rahisi mtu kuripoti anapofanyiwa ukatili.
Ni lazima kufanya tathmini ya hatua zilizochukuliwa kama zimeleta matokeo sahihi au zinasaidia kwa kuwa licha ya kuwapo bado matukio yameendelea kuwapo kwa wingi na kuumiza wengi.
Kama ambavyo wabunge wameona hata watu wengine kwenye jamii wanaona na kufikiria nini kifanyike, mathalani wanasaikolojia wanaeleza sababu za watu kufikia kufanya ukatili, huku wengine wakichukua hatua ya kujiua au kuua wengine.
Watoto wanabakwa na kulawitiwa, kwenye shule za msingi na sekondari matukio hayo yanaripotiwa kwamba wanafunzi kwa wanafunzi wanafanyiana matukio hayo au kufanyiwa na walimu au wazazi wao.
Ni lazima jamii itafakari na kuchukua hatua, jambo hili sio la serikali pekee na waliotendewa ukatili huo peke yake, bali kila mwanajamii kwa kuwa kuna uwezekano wa wengi kuendelea kuumia kama hakutakuwa na hatua sahihi.
Ni muhimu vyombo vya habari vikasaidia kutoa elimu, kualika wataalamu wa saikolojia kuzungumza kwanini mtu anafikia kufanya ukatili, kuwatambua wenye matatizo ya akili na serikali kuboresha hali ya maisha ya wananchi wake kwa kufungua fursa zaidi za ajira ili kupunguza makali ya maisha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Wananchi ni zamu yenu kuenzi tuzo ya AU

Na Gaudensia Mngumi

**HONGERA** Rais Samia Suluhu Hassan na pongezi kwa Tanzania kwa kuongeza mtangamano wa Afrika kupitia kujenga miundombinu ya barabara na juhudi hizo kutambuliwa na Umoja wa Afrika (AU).
AU imekunwa na kazi ya ujenzi wa barabara hizo unaofanywa na serikali na kwa niaba ya Watanzania, Rais Samia akapokea Tuzo ya Babacar Ndiaye 2022 kuenzi mafanikio ya ujenzi huo.
Babacar Ndiaye, alikuwa Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (the African Development Bank Group) tangu 1985 hadi 1995 na tuzo yake hutolewa kuenzi mafanikio katika ujenzi wa miundombinu miongoni mwa mataifa wanachama wa AU.
Tanzania inastahili tuzo hiyo kwa mafanikio mengi, kwanza kazi ya kujenga miundombinu ya usafirishaji inayofanyika, imekuwa sehemu ya kutekeleza mtangamano wa Afrika, ikifanikisha usafirishaji wa shehena na watu kutoka mataifa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) pamoja na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC).
Bila shaka AU, imeliona hilo ndiyo maana Tanzania inastahili pongezi na kutambuliwa kutokana na juhudi kubwa za kuunganisha watu wa mataifa mbalimbali ambao ndiyo mwelekeo wa kuwa na Afrika moja ifikapo 2063 chini ya ajenda ya The Africa We Want.
Afrika moja yenye shirikisho la kisiasa, raia wake wanaotumia pasi na visa moja ya kusafiria, inayomiliki sarafu moja na kubwa zaidi bara lisilo na mipaka linalounganishwa na usafiri usiojali mipaka ya barabara, reli, anga na bahari ndilo linalotazamiwa.
Tanzania imeanza kufanikisha maono hayo kwa kuwa barabara inazojenga ambazo zimeziunganisha nchi nyingi za Afrika Kusini wanachama wa SADC, kuanzia Msumbiji inayojivunia kuwapo daraja la Mtamba Swala mkoani Ruvuma.
Lakini, si hivyo, Malawi na Tanzania zimeunganishwa na mtandao wa barabara madhubuti zinazoanzia kwenye mpaka wa Kasumulu na ule wa Tunduma ukiingia Zambia.
Kadhalika barabara hiyo ndiyo inayotumiwa kufika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, ikisafirisha shehena kuanzia mafuta hadi mavazi kutoka Bandari ya Dar es Salaam hadi Kinshasa.
Barabara hiyo ni utimilifu wa Barabara Kuu ya The Great North Road au the Cairo-Cape Town Highway, inayoanzia Cape Town Afrika Kusini hadi Cairo Misri.
Juhudi hizo zinakwenda pamoja na ujenzi wa barabara za Dar es Salaam hadi Bujumbura, Kigali, Kampala, Mombasa na Nairobi zote hizo zikiendeleza juhudi za ushirikiano, mtangamano na mshikamano.
Ni wazi kuwa mikoa yote 31 ya Tanzania Bara na Zanzibar imeunganishwa na mtandao wa barabara za lami kadhalika na wilaya karibu zote zimeunganishwa na mtandao huo wa wenye lami. Ni juhudi kubwa ambazo hata AU imeziona.
Sasa ni zamu ya Watanzania kuionyesha AU kuwa imepokea tuzo ya Babacar na wako pamoja na serikali yao kutunza na kulinda barabara hizo kwa ajili ya maendeleo yao.
Wananchi watambue kuwa kuchimba mchanga chini ya madaraja, kulima bustani pembezoni ya barabara na kuchimba madimbwi ili kuzimwagilia, kulisha mifugo barabarani pamoja na kuinywesha maji chini ya madaraja ni dharau na chukizo kwa serikali yao inayotumia mabilioni kujenga miundombinu.
Ni vyema wazitumie kwa maendeleo yao ikiwa ni pamoja na kuanzisha miradi ya uzalishaji na biashara mbalimbali ambayo soko lake ni wasafiri wanaozitumia.
Kadhalika halmashauri zingie ubia na wawekezaji mbalimbali kujenga miradi ya kiuchumi pembeni ya barabara hizo hasa viwanda, kusindika mazao, kilimo na uongezaji wa thamani.
Kazi hizo zitaongeza kipato, ajira kwa vijana na kufungua maeneo mapya kiuwekezaji ambayo hayatumiki kwa maendeleo ya taifa.

## Viongozi wa dini wampongeza Rais Samia

**Na Vitus Audax,** MWANZA

VIONGOZI wa dini mkoani Mwanza wamempongeza Rais Samia Suluhu Hassan, kutokana na shughuli mbalimbali anazofanya za kuwaletea wananchi maendeleo.

Walitoa pongezi hizo jana jijini hapo wakati wa kikao cha kujadili shughuli zilizotekelezwa na Rais Samia katika kipindi cha muda mfupi wa uongozi wake.

Akizungumza na waandishi wa habari kwa niaba ya Kamati ya Amani ya Viongozi wa Dini mkoani humo, Shekhe Huseni Kabeke, alisema katika kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wa Rais Samia, kiongozi huyo amekuwa tumaini la Watanzania wote.

Pamoja na mambo mengine, viongozi hao walimpongeza Rais Samia kwa kupewa tuzo ya mjenzi bora Afrika.

"Mama Samia kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama ndani ya mwaka mmoja amesimamia amani na usalama mpaka sasa hakuna vurugu wala misuguano yoyote, vilevile ametoa Sh. bilioni 339.6 kwa ajili ya miradi ya kimkakati katika Mkoa wa Mwanza," alisema Shekhe Kabeke.

Alisema fedha hizo zimetumika katika ujenzi wa Stendi ya Mabasi ya Nyamongolo ambao umefikia asilimia 100, ujenzi wa stendi ya Nyegezi, asilimia 77, ujenzi wa Soko la Mwanza Mjini, asilimia 66.

Alitaja miradi mingine kuwa ni ujenzi wa jengo la abiria katika Uwanja wa Ndege ambao pia umefikia asilimia 88, ujenzi wa meli ya MV Mwanza asilimia 59 na ujenzi wa Daraja la Kigongo-Busisi asilimia 42.

Askofu Charles Sekelwa wa Kanisa la Charismatic Epscopac (CECL) aliwaomba waumini wa madhehebu mbalimbali kumuunga mkono Rais Samia katika mipango yote ya ujenzi wa taifa.

Kwa upande wake, Mchungaji Jacob Mutashi wa EAGT aliomba serikali kutoa elimu kuhusu sensa ya watu na makazi kwa viongozi dini ili iweze kufika kwa urahisi katika jamii.

"Hili suala linatakiwa kuifikia jamii mapema na haraka, hivyo niombe serikali itoe elimu kwa viongozi na watumishi wa dini ambao nyuma yao wanao waamini wengi ambao wanawasikiliza na kuwafuata."

# Shaka: Wananchi muungane kupiga vita vitendo udhalilishaji

**Na Beatrice Shayo**

KATIBU wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Shaka Hamdu Shaka, amewataka wananchi kuungana kupiga vita mambo yote yanayodhalilisha na kukatisha ndoto za mtoto wa kike kupata elimu.

Akizungumza baada ya kutembelea na kushiriki ujenzi wa shule maalumu ya wasichana ya Mkoa wa Lindi inayojengwa Kilangala B, Shaka alisema ipo haja ya kumuunga mkono kwa vitendo Rais Samia Suluhu Hassan, ambaye amejipambanua kuleta usawa wa kijinsia kuanzia ngazi ya chini na kupiga vita udhalilishaji.

"Nichukue fursa hii kumpongeza Rais Samia kwanza kwa namna ambavyo amekuwa kinara wa usawa wa kijinsia nchini. Tangu ameingia madarakani moja ya jambo ambalo amejipambanua nalo na lazima tukiri hatukuwa vizuri katika kusimamia suala la usawa wa kijinsia, lakini ametoa kipaumbele kwenye jambo hili," alisema Shaka.

"Rais amekuwa na msisitizo sana kuwasaidia watoto wa kike sio kwamba anabagua hapana, amekuwa na msukumo kwa sababu huko tulikotoka hali haikuwa nzuri katika mtazamo wa kumtunza na kumlinda mtoto wa kike," alisema.

Shaka alisema kimepatikana kioo ambacho ni Rais Samia ambaye ameonyesha utayari wake katika kumkomboa mtoto wa kike, kusimamia na kuhakikisha usawa wa kijinsia.

"Walio wengi wanaweza kutafsiri usawa huu wa kijinsia unaishia kwenye kuteuana tu, hapana, hatugusi kwenye kuteuana tu. Kwenye kuteuana tunateuana, lakini lazima tuunge nguvu za pamoja wazazi, walezi kinababa na kinamama. Tunapiga vita mambo yote yanayomdhalilisha mtoto wa kike, lakini mambo yote yanayowadhalilisha watoto wetu," alisema.

Aidha, Shaka alisema Mkoa wa Lindi umekuwa na mfumo dume kwa muda mrefu ambao hausaidii kwenye kusukuma na kuharakisha maendeleo ya taifa.

"Kwa hiyo Mkuu wa Mkoa, Chama na wananchi wote tuna kazi ya kufanya kumuunga mkono Rais Samia kufanya mabadiliko kwenye mkoa huu ili wote tuimbe ama wote tuende na kauli moja ya kumsaidia ama kumkomboa mtoto wa kike katika Mkoa wa Lindi.

"Ukienda kwenye kumbukumbu mkoa huu ni miongoni mwa mikoa inayoongoza kwa mimba za utotoni, tujiulize shida ni nini. Ni mkoa ambao wasichana wengi wamekatishwa masomo yao, wamekosa fursa muhimu, ni mkoa ambao wasichana wameathirika kisaikolojia kutokana na vitendo viovu na mambo kadhaa ambayo wanafanyiwa kinyume na ubinadamu," alisema.

Wananchi mkoani Lindi, wamemshukuru Rais Samia na serikali ya awamu ya sita jinsi anavyoonyesha kwa vitendo kuzikomboa kaya maskini. Wakizungumza wakati wa ziara ya Katibu Shaka wananchi hao walioko katika Kijiji cha Kilangala, wanaonufaika na fedha za kusaidia kaya maskini zinazosimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), walisema kupitia fedha hizo wamejiinua kiuchumi kwa kubuni miradi mbalimbali.

Akizungumza kwa niaba ya wanufaika wenzake wa kijiji hicho, ambao wanajihusisha na mradi wa kilimo cha mazao mbalimbali ya biashara ikiwamo minazi, Dalini Makwaya, alisema wanatoa shukrani kwa Rais Samia kwa uamuzi wake wa kutoa fedha hizo na kuwafikia moja kwa moja wahusika.




Wananchi wa Jiji la Tanga wakipanga foleni kwa ajili ya kupata huduma za Kitambulisho cha Taifa kwenye banda la NIDA katika maonyesho ya 9 ya biashara yanayoendelea jijini humo jana. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

## Ahukumiwa kunyongwa hadi kufa kwa kumuua mama mzazi

**Na Samson Chacha,** TARIME

MKAZI wa Kijiji cha Komarera wilayani Tarime mkoani Mara, Mwinga Kerambo, amehukumiwa kunyongwa hadi kufa baada ya kupatikana na hatia ya kumuua kwa kukusudia mama yake mzazi, Bhoke Mohere kwa kumniga shingo na kumnyonga hadi kufa.

Imedaiwa kuwa mama huyo aligoma kumpa kipande cha ardhi ya shamba, alichokuwa akitaka mtoto wake.

Akisomewa hukumu hiyo Mei 25, katika Mahakama Kuu Kanda ya Musoma, Mahakama ya Wilaya Tarime chini ya Msajili wa Mahakama Kuu Kanda ya Musoma, Frank Moshi, Mwanasheria wa Serikali, Yese Temba, alidai mahakamani kuwa mshtakiwa Kerambo, Oktoba 19, 2019 akiwa nyumbani na mama yake alimlazimisha kumpa eneo la ardhi ya shamba na mama huyo aligoma kumpa.

Mwanasheria Temba alidai mshtakiwa Mwinga alichukua uamuzi wa kumshambulia mama yake kwa kumniga shingo na kumnyonga hadi kufa.

Mshtakiwa huyo alikana shtaka hilo na upande wa mashtaka ulikuwa na mashahidi sita vikiwamo vielelezo vya PF 3 na mganga aliyefanya uchunguzi wa mwili wa marehemu.

Mshtakiwa katika kesi hiyo alijitetea mwenyewe bila ya ushahidi mwingine wa kumuunga mkono. Msajili wa Mhakama Kuu Moshi alisema kulingana na ushahidi uliotolewa na upande wa mashtaka, mahakama haina pingamizi na shaka yoyote katika ushahidi huo.

"Mshtakiwa alimuua mama yake kwa makusudi, mahakama hii inakuhukumu kunyongwa hadi kufa ili iwe fundisho kwa watu wengine kama hao ambao hawana maadili mema hata kwa wazazi wao," alisema Moshi.

# WMA yaonya matumizi mizani isiyohakikiwa

**Na Said Hamdani,** LINDI

WAFANYABIASHARA, taasisi za umma na binafsi mkoani Lindi, zimeonywa kutumia mizani bila kufanyiwa uhakiki na Wakala wa Vipimo (WMA) ili kuondoa malalamiko kutoka kwa wananchi wanaowahudumia.

Onyo hilo lilitolewa na Meneja wa Vipimo mkoani humo, Andrew Mbwambo, alipokuwa anazungumza na mwandishi wa habari hizi ofisini kwake.

Mwandishi alitaka kufahamu kama uhakiki wa mizani kwa vyama vya msingi na ushirika vinavyohusika na ununuzi mazao unafanyika kuelekea maandalizi ya mauzo ya zao la ufuta mwaka huu.

Mbwambo alisema uhakiki wa mizani kwa vyama vya msingi na ushirika (Amco's) umefanywa kwa halmashauri nne kati ya sita mkoani humo na kuzitaja kuwa ni Nachingwea, Mtama, Ruangwa na Kilwa, ikiwa ni maandalizi ya ununuzi wa ufuta uliotarajia kuanza rasmi Mei 28, mwaka huu.

Alitaja mizani zingine zilizo hakikiwa kipindi hiki kuwa ni pamoja na kupima magari makubwa yanayobeba madini aina ya mchanga, kokoto, mawe katika kijiji cha Kiranjeranje, Wilaya ya Kilwa.

Hata hivyo, hakutaja idadi ya mizani zilizohakikiwa kwa upande wa vyama vya msingi na ushirika.

Meneja huyo ametaja uhakiki mwingine uliofanyika ni pamoja na mizani 13 zinazotumika kupima uzito wa watu wakubwa na watoto wachanga katika Hospitali ya Kinyonga iliyoko mji mkongwe wa Kivinje, Wilaya ya Kilwa.

Mbwambo alisema mizani walizozihakiki na zilizobainika kuwa na kasoro wamezifanyia marekebisho ni za wodi za watoto wakiwamo wachanga, maabara, kifua kikuu (TB), CTC na zinazotumika kupima watu wakubwa.

Alitoa wito kwa kuwasisitiza wananchi kutokubali kuuza mazao yao kwa mizani ambazo hazijahakikiwa na Wakala wa Vipimo (WMA) ili kuepuka kudhulumiwa.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, akizungumza na wabunge katika semina iliyoandaliwa kwa ajili ya maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wanawake Iringa wampa kongole Rais Samia

**Na Francis Godwin,** IRINGA

WANAWAKE wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa wa Iringa, wamempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa jinsi anavyokitendea haki kiti hicho na kuahidi kumchukulia fomu ya kuwania nafasi hiyo mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa 2025 utakapokaribia.

"Hii ni ahadi yetu kwake katika kuenzi kazi kubwa anayoifanya, tutagharamia fomu yake ya kuwania kiti hicho mwaka 2025," alisema Katibu wa CCM Mkoa wa Iringa, Rukia Mkindu.

Aliyasema hayo juzi kwenye kongamano la Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) wa chama hicho mkoa wa Iringa lililolenga kumpongeza Rais na serikali yake kwa kazi kubwa aliyoifanya kwa kipindi kifupi tangu akalie kiti hicho. Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Iringa, Nikilina Lulandala, aliuzungumzia mkopo wa masharti nafuu wa Sh. trilioni 1.2 uliotolewa na Benki ya Dunia hivi karibuni na jinsi utakavyofungua milango ya kuboresha usalama, ustahimilivu wa tabianchi, uwezo wa barabara za ndani na viwanja vya ndege vya mikoa.

"Kwa kupitia mkopo huo, mkoa wetu unatarajia kunufaika kwa kujenga barabara ya Iringa hadi Hifadhi ya Taifa ya Ruaha-Msembe yenye urefu wa kilometa 104. Mpango huu umekuja wakati muafaka sana kwani dunia inajua jinsi Rais anavyoshiriki yeye mwenyewe kutangaza vivutio vya utalii wa Tanzania," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Queen Sendiga, alizungumzia Sh. bilioni 14.3 zilizotolewa na Rais Samia kwa ajili ya kuboresha sekta ya afya mkoani humo, Sh. bilioni 5.1 (Maji), Sh. bilioni 4.6 (Elimu), Sh. bilioni 11.5 (TARURA) na Sh. bilioni 19.2 TANROADS.

Sendiga pia alizizungumzia kazi zilizofanywa katika sekta nyingine ikiwamo ya kilimo na zaidi ya Sh. milioni 911 zilizotolewa na serikali kwa ajili ya kutoa ruzuku kwa kaya maskini na Sh. bilioni 1.16 kwa ajili ya kuviwezesha vikundi vya wanawake, vijana na wenye ulemavu katika halmashauri za mkoa huo.

"Tunampongeza Rais kwa kuwajali watumishi wa umma na kuwapa nyongeza ya mishahara kwa asilimia 23.3, na kuwaongozea posho za kujikimu. Pamoja na kuongeza posho hizo haina maana kutakuwa na safari holela, tutadhibiti safari ili kupunguza mzigo kwa serikali," alisema.

## 'Wenye ulemavu jishughulisheni acheni kuombaomba'

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WATU wenye ulemavu wametakiwa kujenga tabia ya kujishughulisha kuondokana na hali ya kuwa ombaomba.

Akizungumza na Nipashe nyumbani kwake, Happiness Matagi, mwenye ulemavu wa kuona alisema kukosa shughuli ya kufanya kumekuwa kukiwasababishia watu wenye ulemavu kuishi maisha duni.

Aliwataka kujiunga na vikundi kubuni shughuli za ujasiriamali za kufanya zenye kuwaingizia kipato ambazo zitawakwamua kwenye utegemezi.

"Niliwahi kufungua duka baada ya kuchukua mkopo kutoka halmashauri, lakini lilikufa, wenzangu wengi wenye ulemavu walikuwa wananitembelea na kueleza vikwazo vyao inanibidi nitoe fedha kuwasaidia mwisho duka lilikufa," alisema.

Happiness ambaye ni Katibu wa Shirikisho la Watu wenye Ulemavu (SHIVYAWATA), Wilaya ya Kibaha, alisema kwa sasa anajishughulisha na ufugaji wa ng'ombe na kupitia ufugaji huo anapata maziwa ambayo anauza kila siku na kupata kipato.

Kwa mujibu wa kiongozi huyo, mipango yake ni kupata shamba na kuanza shughuli za kilimo kutokana na vikwazo anavyokumbana navyo kwa sasa kwenye ufugaji wa ng'ombe.

Alisema kutokana na ulemavu wake wa kuona anashindwa kujua kama banda lake la kufugia linafanyiwa usafi unaostahili, kwa kuwa hivi karibuni alikumbana na adha ya ng'ombe kufa.

Aidha, alisema kwa kuwa alisomea masuala ya kilimo na ufugaji atabadilisha shughuli ili kuendelea kupambana kiuchumi.

**Aliwataka kujiunga na vikundi kubuni shughuli za ujasiriamali za kufanya zenye kuwaingizia kipato ambazo zitawakwamua kwenye utegemezi.**

# KOICA yawakumbuka wanafunzi mazingira magumu

**Na Yasmine Protace,** KISARAWE

SERIKALI ya Korea Kusini kwa kushirikiana na Shirika la KOICA nchini, wamekabidhi vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni 50 katika Shule ya Sekondari ya Sister of Marry ambayo inatoa elimu bure kwa wanafunzi wanaotoka katika mazingira magumu.

Vifaa vilivyotolewa ni taulo ngumu paketi 2,100, cherehani 20, kifaa cha maji ambacho husaidia yasiwe na chumvi pamoja na mashine ya kuchunguza meno yenye matatizo.

Shule hiyo ni ya wanafunzi wasichana wanaotoka katika mazingira magumu.

Kyucheol Eo, kiongozi mkuu kutoka KOICA nchini Tanzania, alisema wameamua kutoa msaada katika shule hiyo, ili wasichana waweze kusoma kama wanafunzi wengine na kufikia ndoto zao.

"Hii shule ina watoto wa kike pekee, wanaotoka katika mazingira magumu, tumeona ni vyema kuwasaidia ili nao waweze kufikia malengo yao.

Alisema katika shule hiyo, changamoto ni maji kuwa na chumvi nyingi, kifaa walichotoa kitawasaidia kupata maji mazuri yasiyo na chumvi.

Kadhalika, alisema shule hiyo inatoa pia elimu ya ufundi wa cherehani na kuwawezesha kuendelea na elimu hiyo, ambayo kwao itakuwa mkombozi.

Alisema kutokana na kuwapo kwa malalamiko ya watoto kuumwa meno na kulazimika kuwapeleka nje ya shule kupata huduma hiyo, sasa wameona ni vyema kuwapatia msaada wa kifaa hicho kwa ajili ya uchunguzi wa meno.

"Tumewapatia shule kifaa kwa ajili ya uchunguzi wa meno, pamoja na kutoa kifaa hicho tunafanya utaratibu wa kuongea na Wizara ya Afya ili kifaa hicho kiweze kutumiwa na shule kuwasaidia wanafunzi kutotoka nje kwenda kufuata huduma ya meno," alisema.

Alisema mwezi Septemba mwaka huu, baadhi ya walimu kutoka nchini kwao watakuja Tanzania na Zanzibar kwa ajili ya kuja kujitolea kufundisha masomo mbalimbali katika shule za sekondari.

Olva John, mwanafunzi kutoka shule hiyo, aliishukuru KOICA kwa kuwapatia misaada hiyo.

# CBE sasa kuanzisha mitaala ya kuwezesha wanafunzi kujiajiri

**Na Joseph Mwendapole**

CHUO cha Elimu ya Biashara (CBE), kimepanga kutatua changamoto ya ajira kwa vijana na uhaba wa vipimo vya kidigitali nchini kwa kuanzisha mitaala itakayowawezesha wanafunzi kuanzisha kampuni za kutengeneza vipimo hivyo.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Mkuu wa chuo hicho, Profesa Emmanuel Mjema, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Vipimo Duniani yaliyofanyika chuoni hapo na kaulimbiu ya mwaka huu ni 'Vipimo katika ulimwengu wa kidigitali'.

Profesa Mjema alisema elimu ya juu inapaswa kutatua changamoto za nchi badala ya wahitimu wake wengi kutegemea kuajiriwa na kwamba wanafunzi lazima waandaliwe kutengeneza fursa za ajira kwa wenzao.

Profesa Mjema alisema kwa nchi zote za Afrika Mashariki, Tanzania ni pekee inayofundisha kozi ya vipimo na mizani kupitia Chuo cha CBE lengo ikiwa ni kutatua uhaba wa wataalamu wa fani hiyo kwenda ukanda huo.

"Kaulimbiu ya mwaka huu imechaguliwa kwasababu teknolojia hii ya kidijitali inatumika maeneo mengi duniani kwa mfano matumizi ya akili bandia 'artificial intelligence', inatumika sana kwenye masuala ya vipimo duniani," alisema Profesa Mjema.

Alisema hata Tanzania vipimo vingi vinavyotumika kwa sasa ni vya kidijitali akitoa mfano wa mizani inayotumika kwenye maduka mengi ya kuuzia nyama na vipimo vya kupima joto la mwili wa binadamu kwenye hospitali mbalimbali.

"Wengi mtakumbuka zamani kupimwa joto unawekewa kile kipimajoto mdomoni sasa kwa mazingira ya sasa magonjwa yalivyo mengi hebu fikiria kama bado tungekuwa tunatumia kipimo hicho nani angekubali kuwekewa lile lidude mdomoni mwake likiwa limetoka kwenye mdomo mwingine," alihoji.

Alisema hata vipimo vya ujazo wa mafuta kwenye matangi umebadilika, badala ya utaratibu wa zamani wa kupanda juu ya gari na kuingiza fimbo ndani ya tangi la mafuta sasa mtu anaweza kujua ujazo wa mafuta akiwa nje.

"Ulimwengu wa kidijitali umeleta mapinduzi makubwa sana naamini hata Chuo cha Elimu ya Biashara kwa kuwa ndicho kinaongoza kwenye kozi hii ya vipimo lazima twende kidijitali isiwe ulimwengu unaenda kule sisi tunabaki kizamani," alisema.

Alisema elimu ya kidijitali itakuwa na msaada mkubwa kwa jamii ikiwamo kuhakikisha wananchi wanapata vipimo sahihi wanapokwenda kununua bidhaa mbalimbali.

"Vipimo vya kizamani wananchi waliibiwa sana, yale mawe yalikuwa yanakwanguliwa mpaka yanapoteza uzito fulani. Muuzaji anakuwa na mawe feki na halisi akija mtu anayeonekana kwamba hajui mambo anabambikiwa jiwe feki, lakini akija anayeonekana mjanja mjanja anawekewa jiwe sahihi, lakini kwa dijitali haya yote hayapo tena," alisema.




Mkuu wa Kitengo cha Miamala wa Benki ya NMB, Linda Teggisa, akizungumza katika hafla fupi iliyokutanisha wadau wa mafuta na gesi na kufanya majadiliano, iliyofanyika hoteli ya Serena jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ushauri kwa wajawazito wenye VVU

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

KINAMAMA wanaoishi na Virusi vya Ukimwi wametakiwa kupata mapumziko baada ya kujifungua ili wapate kuimarika kiafya pamoja na mtoto kwa kufuata maelekezo ya daktari wakati mwingine anaotakiwa kubeba mimba.

Akizungumza na mwandishi wa habari hizi, Msimamizi wa vituo vya kutoa huduma kwa watu wenye VVU, Dk. Rahila Salim Omar, alisema, mwili unapotoa kiumbe unahitaji kujirejesha katika hali ya kawaida na kubeba mimba nyingine.

Alisema, wakati wa ujauzito kinga ya mwili inashuka na uwezekano wa kupata maambukizi mengine unakuwa mkubwa na kumhatarisha mtoto kupata VVU.

"Hata kama mama mwenye VVU tumempima jana, basi akija leo ikiwa tumemgundua na ujauzito, tunampima tena wingi wa virusi, kama idadi imeongezeka," alisema.

Dk. Rahila, alisema kama virusi vimeongezeka, wanampa huduma ya ziada kumkinga mtoto na maambukizi hayo na kumpima kila baada ya miezi mitatu.

Kwa upande wake Dk. Khamis Hamad, Msaidizi Meneja Kitengo Shirikishi cha Ukimwi, Kifua Kikuu, homa ya ini na ukoma, alisema mjamzito anayeishi na VVU anahitaji zaidi kuzaa kwa mpangilio kutokana na kinga yake kupungua.

"Ingawa wajawazito wote kinga yao hupungua, lakini hawa wanaoishi na VVU inapungua zaidi, hivyo anatakiwa apangiwe muda wa kuzaa kulingana na idadi ya virusi alivyonavyo," alisema.

Alifafanua kuwa, mimba za papo kwa papo, zinasababisha mwili kutokujirudi na kuwa dhaifu na mama atakuwa hana muda wa kumshughulikia mtoto wake kwa malezi na hata katika mfumo wa kula.

"Mtoto anatakiwa anyonye maziwa ya mama kwa miezi sita bila kumchanganyia chochote, lakini ikiwa mama atabeba mimba nyingine kabla ya wakati unaotakiwa, atamkosesha mwanawe haki zinazostahiki," alieleza daktari huyo.

Maryam Salum ni mama anayeishi na VVU, mkaazi wa Mabaoni Chakechake alisema, alipata elimu kupitia madaktari na aliambiwa kwamba anapotaka kubeba mimba afike kliniki kupewa ushauri.

"Najitahidi kufuata ushauri wa daktari ili kumkinga mtoto wangu dhidi ya maambukizi, kwa sababu unapotaka kubeba mimba unapewa maelekezo na ni vizuri uyafuate," alisema.

Pia, baada ya kubeba mimba anatakiwa kutumia dawa vizuri na chakula kizuri kwa lengo la kujenga afya yake na mtoto, ili kumkinga mtoto asipate maambukizi.

Kwa upande wake Maryam Said Abdalla, mkaazi wa Chakechake, alieleza umuhimu mkubwa kwa mama mwenye VVU kutumia uzazi wa mpango kwa kuwa kinga zao ni tofauti na wasio na virusi.

Mratibu wa Tume ya Ukimwi Pemba, Ali Mbarouk Omar, aliwataka kinamama hao kutumia njia za uzazi wa mpango kuhakikisha wanapata muda wa kupumzika ili mwili ujirudi katika hali nzuri.

Alisema kuwa, ipo haja ya kufuata ushauri wa daktari mara kwa mara, jambo hilo litasaidia kumkinga mtoto na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi.

# Wabunge wahoji tatizo la hati chafu kujirudia

WABUNGE wametaka serikali kuimarisha utoaji mafunzo ya uandaaji wa taarifa za fedha za mwisho kwenye halmashauri ili kuondokana na tatizo la hati chafu linalojirudia kwenye baadhi ya maeneo.

Akiuliza swali bungeni jana, Mbunge wa Viti Maalum, Grace Tendega, alihoji serikali ina mpango gani wa kuhakikisha maofisa masuuli na wahasibu katika halmashauri wanapata mafunzo juu ya uandaaji wa taarifa hizo.

"Serikali haioni umuhimu wa kupeleka fedha za mafunzo, ili kuwa na uwiano sawia? Kumekuwa na mfululizo wa hati chafu ambazo ni zaidi ya miaka 10 mfululizo, je, serikali haioni inaendelea kupoteza fedha za wananchi kwa kutokuwa na watu wenye weledi?" alihoji.

Naye Mbunge wa Vwawa (CCM), Japhet Hasunga, alisema serikali imetoa mafunzo kwa maofisa 210 ambao ni wachache ikilinganishwa na halmashauri zilizoko nchini na mikoa iliyopo. "Je, serikali ina mpango gani wahasibu na wakaguzi wa ndani wanapatiwa mafunzo stahili katika uandaaji wa hesabu?" alihoji.

Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, alisema katika mwaka wa fedha 2021/22 serikali imetoa mafunzo kwa watumishi 210 ya uandaaji wa taarifa za fedha za mwaka unaoishia Juni 30, mwaka 2022. Alisema mafunzo hayo yametolewa kwa watumishi waliopo ngazi ya mikoa na halmashauri zote nchini.

"Serikali imeendelea kuboresha mwongozo wa uhasibu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa wa mwaka 2020 na waraka wa ufungaji hesabu kila mwaka," alisema.

Alibainisha kuwa maboresho hayo yanakusudia kuzikumbusha taasisi za umma mambo ya msingi ya kuzingatia na kuwaongoza maofisa masuhuli na wahasibu kutekeleza majukumu yao ikiwa ni pamoja na uandaaji wa hesabu za mwisho.

Kadhalika, alisema lengo la serikali ni kuongeza fursa za mafunzo na kuzigawa kulingana na uwiano wa halmashauri moja na nyingine na kuzuia wizi wa fedha za umma kwenye halmashauri.

"Moja ya kazi kubwa ambayo tumeifanya sasa hivi ya kuzuia hati chafu ni kuwaondoa watu wanaosimamia fedha kwenye maeneo hayo wakiwamo wahasibu, waweka hazina na wakurugenzi na hatutakuwa tunahamisha kama awali," alisema.

Alisema kwa sasa wameongeza fedha kutoa mafunzo hayo ili kufanya kazi inayokusudiwa.



Mbunge wa Jimbo la Vunjo, Dk. Charles Kimei, akiuliza swali la nyongeza jana, bungeni ambapo aliomba serikali kuwasaidia kinamama kujengewa vibanda kwa ajili ya shughuli zao. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Mwongozo kutolewa wawekezaji biashara hewa ukaa

KUTOKANA na ongezeko kubwa la wadau wanaotaka kufanya biashara ya hewa ukaa, Ofisi ya Makamu wa Rais inaandaa mwongozo wa kitaifa utakaotumiwa na wawekezaji, taasisi, watu binafsi wenye nia kufanya biashara hiyo nchini.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo, aliyasema hayo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kilolo (CCM), Justine Nyamoga.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kuomba fedha katika mifuko ya kupunguza hewa ukaa duniani na kuwalipa wananchi wanaopanda na kutunza misitu kwenye Wilaya ya Kilolo.

Akijibu swali hilo, Waziri Jafo, alisema hewa ukaa ni moja ya gesijoto ambazo mrundikano wake angani husababisha mabadiliko ya tabianchi.

"Moja ya njia zinazotumika kupunguza hewa ukaa chini ya mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Mabadiliko ya Tabianchi ni misitu ambayo hunyonya hewa ukaa wakati mimea inapotengeneza chakula," alisema.

Aidha, alisema mkataba huo hauna mfuko mahsusi wa kulipa miradi ya hifadhi ya misitu inayotekelezwa katika nchi wanachama zinazoendelea kwa ajili ya kupunguza hewa ukaa.

"Badala yake, mkataba huo umeweka utaratibu wa kibiashara ambapo kampuni kutoka nchi zilizoendelea ambazo zinawajibika chini ya mkataba huo kupunguza gesijoto hulipa miradi ya kupunguza hewa ukaa kupitia hifadhi ya misitu katika nchi zinazoendelea," alisema.

Alitoa mfano wa kampuni kutoka nchi zilizoendelea ni Carbon Tanzania kutoka Uingereza ambayo hugharamia miradi ya Mkuhumi katika mikoa ya Manyara na Katavi.

"Kutokana na ongezeko kubwa la wadau wanaotaka kufanya biashara hii, Ofisi ya Makamu wa Rais inaandaa mwongozo wa Kitaifa wa Biashara ya Hewa Ukaa utakaotumiwa na wawekezaji, taasisi, watu binafsi wenye nia kufanya biashara hii hapa nchini," alisema.

## TARURA kuja na fomula ugawaji rasilimali fedha

BUNGE limeelezwa kuwa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) inaandaa fomula ya ugawaji wa rasilimali fedha zinazohitajika kwenye ujenzi na matengenezo ya miundombinu ya barabara kulingana na mahitaji ya eneo husika.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), David Silinde, aliliambia Bunge jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Same Magharibi (CCM), Dk. David Mathayo.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji kwanini serikali haitengi fedha za TARURA kwa kuzingatia jiografia, ukubwa wa eneo na mazingira ya wilaya au jimbo.

Akijibu swali hilo, Silinde alisema fomula hiyo itazingatia ukubwa wa mtandao wa barabara, thamani ya miundombinu ya barabara iliyopo, hali ya barabara, wingi wa magari, idadi ya wakazi, mazingira, kiwango cha mvua na kilimo.

Katika swali lake la nyongeza, Mbunge wa Mbozi (CCM), George Mwenisongole, alisema Jimbo la Tunduma linaingia mara sita kwa Mbozi lakini wanapata fedha sawa za mgao wa barabara.

"Sasa haoni (Naibu Waziri Silinde) sio sawa?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Silinde alikiri kuwa Jimbo la Mbozi ni kubwa kuliko la Tunduma na kwamba utaratibu uliotumika mwaka uliopita walikubaliana wabunge wote.

Hata hivyo, alisema kwasasa wanabadili fomula ili kulinganisha ukubwa wa maeneo na mahitaji ya eneo husika.

Katika swali jingine la nyongeza, Mbunge wa Ukerewe (CCM), Joseph Mkundi, alisema pamoja na serikali kutoa fedha nyingi kwenye miradi inayotekelezwa na wakala huo, lakini bado imesimama au kusuasua ikiwamo Jimbo la Ukerewe kutokana na makandarasi kutokuwa na uwezo au kuwa na mrundikano wa kazi na kuhoji kauli ya serikali kwenye suala hilo.

Akijibu swali hilo, aliwataka makandarasi kuhakikisha wanakamilisha kazi hiyo kwa muda uliopangwa na kutoa wito kuwasilisha taarifa za maeneo ambayo makandarasi hawafanyi kazi ili kuchukua hatua ikiwamo kuvunja mikataba ya kazi hizo.




Habari zote na Augusta Njoji

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM

### BAJETI YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM KWA MWAKA 2022/2023



**Mhe. Dkt. Dorothy Gwajima (Mb)**
Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake Makundi Maalum



**Mhe. Mwanaidi Ali Khamis (Mb)**
Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum



**Dkt. Zainab Chaula**
Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum



**Amon Mpanju**
Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum

# HOTUBA YA WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WANAWAKE NA MAKUNDI MAALUM, MHE. DKT. DOROTHY GWAJIMA (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2022/23

## A. UTANGULIZI

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii ndani ya Bunge lako Tukufu, ambayo imechambua Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, ninaomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (Fungu 53) kwa mwaka 2021/22 na Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2022/23. Aidha, ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida pamoja na Miradi ya Maendeleo ya Wizara kwa mwaka 2022/23.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili kuwasilisha hotuba yangu siku ya leo. Pia, nitumie fursa hii kumshukuru sana **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri katika kuimarisha utoaji wa huduma za ustawi na maendeleo ya jamii kwa Watanzania. Kipekee ninamshukuru kwa kuunda Wizara mpya ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum na kuniteua kuiongoza Wizara hii. Natambua kuwa matarajio ya Mheshimiwa Rais ni kuona hali ya usawa wa kijinsia hapa nchini inaimarika na utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii unafanyika kwa kasi kubwa na ufanisi. Ninamuahidi kwamba nitaendelea kutimiza majukumu yangu kwa weledi mkubwa ili kuhakikisha kwamba matarajio yake yanafikiwa kikamilifu. Aidha, nampongeza kwa kuendelea kuongoza nchi yetu kwa mafanikio makubwa tangu aingie madarakani akiwa ni Rais wa Awamu ya Sita wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sote tumeshuhudia mafanikio makubwa yaliyopatikana katika nyanja mbalimbali chini ya uongozi wake.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, napenda kumshukuru **Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango,** Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye amekuwa mstari wa mbele katika jitihada za kuboresha huduma za maendeleo na ustawi wa jamii, kuhimiza usawa wa jinsia, uwezeshaji wa wanawake kiuchumi na kuzingatia haki za mtoto katika jamii. Wizara yangu itaendelea kutekeleza kikamilifu maelekezo na mikakati inayotolewa na Ofisi yake.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kumshukuru **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb)**, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri uliowezesha kuleta tija na ufanisi katika utendaji na kuimarisha huduma zinazotolewa katika Sekta ya Maendeleo na Ustawi ya Jamii. Aidha, ninampongeza kwa hotuba yake aliyoiwasilisha kwenye Bunge lako Tukufu tarehe 6 Aprili, 2022 ambayo imetoa mwelekeo wa majukumu yatakayotekelezwa na Serikali katika mwaka 2022/23.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kukupongeza wewe binafsi kwa kuaminiwa na Waheshimiwa Wabunge na kuweza kuchaguliwa kwa kishindo kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, ninampongeza **Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu (Mb)** kwa kuchaguliwa kuwa Naibu Spika. Ni imani yangu kuwa mtatekeleza majukumu yenu kwa weledi na ufanisi mkubwa katika kuliongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, nawapongeza sana Wenyeviti wa Bunge kwa kuendelea kusimamia vyema mijadala mbalimbali ndani ya Bunge hili Tukufu.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, nitumie fursa hii kuwapongeza **Mheshimiwa Emmanuel Lekishon Shangai** kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro na **Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha** kwa kuteuliwa kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naamini kuwa Bunge lako Tukufu litaendelea kushirikiana nao ili waweze kutekeleza majukumu yao kikamilifu.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kuwashukuru Mawaziri wenzangu kwa ushirikiano wanaonipatia ambao unaiwezesha Wizara yangu kuendelea kuimarisha na kuboresha utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Wizara itaendelea kushirikiana nao na kuhakikisha tunatimiza dhamira ya **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kuhakikisha kuwa Sekta ya Maendeleo na Ustawi wa Jamii inaratibiwa vyema kwa matokeo chanya.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee ninapenda kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, chini ya Mwenyekiti **Mheshimiwa Stanslaus Haroon Nyongo (Mb)** na Makamu wake, **Mheshimiwa Aloyce John Kamamba (Mb)** kwa ushauri na maelekezo waliyoyatoa wakati wa maandalizi ya Bajeti hii. Aidha, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano mzuri wanaotupatia ikiwemo kutoa ushauri na maoni mbalimbali yenye lengo la kuboresha huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Ninawaahidi kwamba, Wizara ninayoiongoza itazingatia ushauri wao na kuendelea kuwapa ushirikiano katika kutekeleza majukumu ya kuwatumikia wananchi kwa moyo wote ndani na nje ya Bunge.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa pole kwako, Bunge lako Tukufu na wananchi wote kwa vifo vya wapendwa wetu **Mheshimiwa Elias John Kwandikwa**, aliyekuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa na Mbunge wa Jimbo la Ushetu; **Mheshimiwa William Tate Olenasha,** aliyekuwa Naibu Waziri wa Uwekezaji (Ofisi ya Waziri Mkuu) na Mbunge wa Jimbo la Ngorongoro; **Mheshimiwa Khatibu Said Haji**, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Konde Zanzibar); na **Mheshimiwa Irene Alex Ndyamkama**, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Rukwa (CCM). Aidha, nawapa pole Watanzania wenzetu waliopoteza maisha kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo ukatili. Mwenyezi Mungu azilaze roho za marehemu wote mahala pema peponi. Amen.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kutoa maelezo ya awali, ninapenda sasa kutoa maelezo kuhusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2021/22, Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi pamoja na Maombi ya Fedha kwa ajili ya kutekeleza Vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2022/23.

## B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2021/22

11. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sera, Mpango Mkakati pamoja na Makubaliano ya Kitaifa na Kimataifa yenye lengo la kuimarisha utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii nchini. Sera hizo ni pamoja na Sera ya Maendeleo ya Jamii (1996); Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia (2000); Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2001); Sera ya Taifa ya Wazee (2003); na Sera ya Maendeleo ya Mtoto (2008). Vilevile, katika kuandaa mpango na bajeti, Wizara imezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo (2025), Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26), Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020, Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (2017/18 – 2021/22), Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs 2030) na Agenda ya Afrika Tuitakayo (2063). Aidha, Wizara inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Ahadi za Nchi katika Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa (*Generation Equality Forum* – GEF, 2021 – 2026).

***12. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara ilipanga kutekeleza afua mbalimbali zenye lengo la kuboresha utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii katika maeneo yafuatayo: -

(i) Kukuza ari ya jamii, uzalendo na kujenga moyo wa kujitolea katika kujiletea maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa kutumia nguvukazi na rasilimali zinazowazunguka;
(ii) Kutekeleza dhana ya uanagenzi, ubunifu na ushirikishwaji jamii kwenye Taasisi na Vyuo ili kuzalisha wanafunzi wanaoajirika na kujiajiri na kuwa chachu ya maendeleo; (iii) Kuratibu uwezeshaji wa wanawake kiuchumi na uingizaji wa masuala ya jinsia katika Sheria, Sera, Mipango, Mikakati, Programu na Bajeti;
(iv) Kuendelea kuimarisha huduma za ustawi wa jamii na haki kwa familia na watoto ikiwemo malezi ya kambo na kuasili, watu/walezi wa kuaminika, malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya watoto, ulinzi na usalama kwa watoto dhidi ya vitendo vya ukatili pamoja na huduma za utengemao katika familia kwa watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani;
(v) Kuimarisha huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa na familia, Msaada wa Kisaikolojia na Kijamii kwa familia, jamii na makundi mbalimbali wakiwemo wazee, watoto walio katika mazingira hatarishi pamoja na manusura wa ukatili na majanga mbalimbali;
(vi) Kuimarisha ufuatiliaji na uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili yaweze kutoa mchango chanya katika ujenzi wa Taifa;
(vii) Kuendelea kuratibu kampeni mbalimbali za kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto; (viii) Kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ili kutoa mafunzo yanayokidhi mahitaji ya soko;
(ix) Kusimamia, kufuatilia na kuimarisha uanzishaji na uendelezaji wa Vituo vya Kulelea Watoto Wadogo na Vituo vya Kijamii vya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto katika ngazi ya jamii ili kuboresha malezi na makuzi ya kila mtoto;
(x) Kuendelea kuimarisha utoaji wa huduma za msingi katika Vituo vya Ustawi wa Jamii ikiwemo Makazi ya Wazee na Watu wenye Ulemavu, Mahabusu za Watoto, Makao ya Watoto na Shule ya Maadilisho;
(xi) Kuimarisha mifumo ya kusimamia, kufuatilia na kutathmini viwango vya huduma za ustawi wa jamii zinazotolewa nchini;
(xii) Kuanzisha na kuimarisha utendaji wa Mabaraza ya Watoto na Dawati la Ulinzi la Watoto Shuleni;
(xiii) Kuendelea kuratibu uundwaji wa Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto pamoja na kuzijengea uwezo; (xiv) Kuratibu uanzishwaji wa vikundi vya malezi katika ngazi ya jamii; na
(xv) Kuhamasisha ushiriki wa wanawake katika ngazi za uongozi na nafasi mbalimbali za maamuzi.

### MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA (FUNGU 53)

13. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara ilipanga kukusanya kiasi cha **Shilingi 6,000,000,000** kutokana na ada za wanafunzi katika Vyuo nane (8) vya Maendeleo ya Jamii, uuzaji wa Mitaala ya Vyuo vya Maendeleo ya Jamii, usajili na ada za mwaka za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (NGOs), uuzaji wa Mitaala ya Vyuo vya Ustawi wa Jamii, ada za mwaka, uuzaji wa Mitaala ya Vituo vya kulelea Watoto Wadogo Mchana na vyanzo vingine vya mapato. Hadi kufikia mwezi Aprili 2022, Wizara imefanikiwa kukusanya kiasi cha **Shilingi 3,566,324,302** sawa na asilimia 59 ya makadirio ya mapato. Ni matarajio yangu kuwa hadi kufikia mwezi Juni 2022, Wizara itafikia lengo la asilimia 100 ya makusanyo kama ilivyopangwa.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, Wizara iliidhinishiwa na Bunge lako tukufu jumla ya matumizi ya **Shilingi 45,966,248,430.83.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 31,066,248,430.83** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 18,080,576,430.83** ni fedha za Matumizi Mengineyo (OC) na **Shilingi 12,985,672,000** ni kwa ajili ya Mishahara. Aidha, kiasi cha **Shilingi 14,900,000,000** kilikuwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambapo **Shilingi 4,900,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 10,000,000,000** ni fedha za nje.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia mwezi Aprili 2022, Wizara imepokea jumla ya **Shilingi 31,315,282,868.47** sawa na asilimia 68 ya bajeti kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha zilizopokelewa, Matumizi ya Kawaida ni **Shilingi 25,143,892,668.47** sawa na asilimia 81 ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 14,294,778,313.27** ni Matumizi Mengineyo na **Shilingi 10,849,114,355.20** ni kwa ajili ya Mishahara. Aidha, **Shilingi 6,171,390,200** ni Fedha za Maendeleo ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 4,900,000,000** ni fedha za ndani na **Shilingi 1,271,390,200** ni fedha za nje. ***Naipongeza sana Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuipatia Wizara kiasi hicho cha fedha kwa mtiririko mzuri unaowezesha utekelezaji wa majukumu.***

## C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA (FUNGU 53)

16. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2021/22, utekelezaji wa majukumu ya Wizara ulilenga kuimarisha ushiriki wa jamii katika shughuli za maendeleo, kuimarisha upatikanaji wa haki na maendeleo ya mtoto, kuboresha huduma za ustawi wa jamii, kuchochea maendeleo ya jinsia na uwezeshaji wa wanawake, kuratibu utekelezaji wenye ufanisi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA). Uratibu wa utekelezaji wa majukumu haya ulifanywa na Wizara kwa kushirikiana na Taasisi zake pamoja na wadau mbalimbali.

### ENEO LA 1: MAENDELEO YA JAMII

17. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Jamii ya Mwaka 1996, ambayo inasisitiza dhana ya ushiriki wa jamii katika kujiletea maendeleo kwa kutumia rasilimali zilizopo katika maeneo yao. Aidha, inasisitiza kuendeleza na kukidhi mahitaji ya makundi maalum wakiwemo wafanyabiashara ndogondogo (Machinga) ambao wengi wao ni vijana. Katika utekelezaji wa jukumu hilo, yafuatayo yamefanyika: -

18. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi mwezi Aprili 2022, Wizara imeimarisha uratibu na usimamizi wa shughuli za wafanyabiashara ndogondogo wajulikanao kama Machinga, kufuatia maelekezo ya **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan,** Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyotoa tarehe 25 Januari 2022 kwamba Serikali anayoiongoza inawatambua Machinga wote nchini kama kundi maalum ambalo litakuwa chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Hivyo, uongozi wa Wizara uliwapokea rasmi na kukutana na viongozi wa Shirikisho la Umoja wa Machinga Tanzania (SHIUMA) ngazi ya Taifa. Aidha, katika vipindi tofauti kuanzia mwezi Februari hadi Aprili 2022, Wizara imejadiliana nao na kubaini kuwa Shirikisho hilo lilikuwa linakabiliwa na changamoto za kiuongozi na kiusimamizi, kiuchumi, kimfumo (TEHAMA), kutokuwa na usajili, kutokuwa na mahali pa uhakika pa kufanyia kazi na kutokuwa na anwani.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutatua changamoto hizo, Wizara imewezesha usajili wa SHIUMA kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na kupatiwa cheti chenye usajili **Namba 21825**. Pia, imewajengea uwezo viongozi 10 wa SHIUMA ngazi ya Taifa pamoja na washiriki 198 kutoka Mikoa 26 ya Tanzania Bara. Lengo la mafunzo hayo lilikuwa ni kuwajengea uwezo kuhusu uongozi bora, fursa za kifedha, ujasiriamali na utii wa sheria bila shuruti. Aidha, imewapatia sehemu ya kufanyia kazi ndani ya jengo lake. Vilevile, inaendelea kuimarisha mahusiano ya kiutendaji baina ya viongozi na wanachama wa shirikisho kuanzia ngazi ya Taifa hadi kwenye masoko. Wizara kupitia Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) imeanza kutengeneza Mfumo wa Kieletroniki wa utambuzi wa wafanyabiashara ndogondogo (Machinga) ujulikanao kama "*Wajasiriamali Connect*". Mfumo huo utawawezesha wafanyabiashara hao kupata fursa mbalimbali ikiwemo upatikanaji wa mikopo nafuu kutoka katika taasisi za fedha.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeratibu mafunzo kwa viongozi 803 wa SHIUMA kuanzia tarehe 16 – 19 Mei, 2022 Jijini Dodoma. Kaulimbiu ilikuwa "Machinga ni Fursa Sahihi ya Kukuza Uchumi wa Nchi Yetu". Katika mafunzo hayo, **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alishiriki kwa njia ya simu ambapo aliweza kuahidi kutoa **Shilingi Milioni 10** kwa kila Mkoa kuanzia mwaka 2022/23 ili kukabiliana na changamoto wanazopata Machinga katika uendeshaji wa shughuli zao. Mwelekeo zaidi kuhusu Machinga ni kuandaa Sheria moja ya Machinga pamoja na Mkakati wa Maendeleo ya Machinga hatua ambazo zimeanza kuchukuliwa.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inapenda kutambua mchango wa Wadau mbalimbali, Taasisi na Wizara za Kisekta ikiwemo: Ofisi ya Makamu wa Rais; Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu; Ofisi ya Rais – TAMISEMI; Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Wizara ya Fedha na Mipango; Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara; Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; na Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari. Wizara hizi kwa pamoja zimeweza kutekeleza majukumu yake katika kutatua changamoto za Machinga kama ifuatavyo: kuratibu zoezi la utambuzi wa Machinga kwa kuwapa vitambulisho na kuondoa kodi zilizokuwa zinakwamisha ukuaji wa biashara za Machinga; kutenga na kujenga miundombinu ya masoko katika Mikoa mbalimbali ili kurahisisha utendaji wa shughuli za Machinga; kuwapa elimu juu ya utambuzi wa bidhaa bandia; athari zinazotokana na bidhaa bandia kwa Machinga na katika uchumi wa nchi; na kuwapa elimu juu ya kuheshimu sheria za Nchi wakati wa utekelezaji wa majukumu yao.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** *napenda kutoa shukrani za dhati kwa Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri nchini na Wadau wengine kwa namna wanavyoshughulikia suala la ujenzi wa miundombinu na upangaji wa wafanyabiashara ndogondogo nchini. Aidha, shukrani zangu za dhati ziwafikie viongozi wa SHIUMA ngazi ya Taifa kwa kuendelea kushirikiana na Wizara yangu katika kuhakikisha kuwa changamoto za Machinga Nchini zinapatiwa ufumbuzi.*

23. ***Mheshimiwa Spika,*** Wataalam wa Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na viongozi ngazi mbalimbali wamekuwa chachu ya kutekeleza kampeni mbalimbali za Kitaifa na wanaendelea kuamsha ari ya jamii kuboresha makazi yao. Kampeni hii inatumia mfumo wa asili wa kusaidiana katika maeneo yenye makazi duni ikiwemo Mikoa ya Lindi, Kagera, Tanga, Tabora, Pwani, Arusha, Kigoma, Singida, Mtwara na Katavi. Ujenzi wa nyumba hizo unatumia gharama nafuu kati ya **Shilingi 7,000,000** hadi **Shilingi 10,000,000** ambapo jamii au kikundi humsaidia mmoja wao anayejenga nyumba kufyatua tofali za kuchoma, kukusanya mawe, mchanga na kuchota maji ya kujengea ili kupunguza gharama za ujenzi. Fedha taslimu hutumika kununua vifaa vya dukani kama bati na saruji. Aidha, jamii hutumia vikundi vya kuweka na kukopa (VICOBA) au mtindo wa kupeana fedha kwa ajili ya kununua vifaa vya dukani.

Vilevile, ili kurahisisha ujenzi wa nyumba bora, Vyuo vya Maendeleo ya Jamii Ufundi vya Mabughai na Misungwi vimekuwa na utaratibu wa kuandaa ramani za makazi na kuzitoa kwa gharama nafuu. Katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi mwezi Aprili 2022, kampeni ya makazi bora imetekelezwa katika Mikoa 10. Nyumba zilizojengwa zimeongezeka kutoka nyumba 751 mwaka 2020/21 hadi nyumba 5,002 kufikia mwezi Aprili, 2022. Nyumba hizo zimejengwa katika Mikoa ya Arusha (683), Morogoro (2,397), Songwe (225), Shinyanga (698), Rukwa (22), Mwanza (273), Tanga (350), Ruvuma (2), Pwani (186) na Geita (166). Kampeni inalenga kufikia Mikoa 26 ifikapo mwaka 2025. **Nitumie fursa hii kuishukuru Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa miongozo ya Kisera, OR-TAMISEMI kwa kusimamia utekelezaji wa kampeni na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali hususan Shirika la Kivulini kwa kushiriki kuhamasisha jamii kuboresha makazi yao.**

24. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuamsha ari ya jamii kushiriki kikamilifu kwenye miradi ya kijamii kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi mwezi Aprili 2022, Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na viongozi ngazi mbalimbali kuanzia Taifa, Mkoa, Halmashauri hadi Kata wameendelea kuhamasisha jamii kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye Mikoa 26 ya Tanzania Bara, ambapo jamii imeshiriki kikamilifu kwenye miradi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 963 katika Mikoa ya Singida, Morogoro, Arusha, Kilimanjaro, Rukwa, Katavi, Dodoma, Dar es Salaam, Geita, Kagera, Kigoma, Lindi, Mara, Mbeya, Mtwara, Pwani, Njombe, Ruvuma, Shinyanga, Simiyu, Tabora, Tanga, Iringa na Lindi. Aidha, jamii imeshiriki katika ujenzi wa vituo 294 vya kutolea huduma za afya katika Mikoa ya Iringa, Singida, Morogoro, Arusha, Katavi, Dar es Salaam, Geita, Kagera, Kigoma, Lindi, Mara, Mbeya, Mtwara, Njombe, Pwani, Ruvuma, Rukwa, Tanga, Tabora, Simiyu na Kilimanjaro. Juhudi za ujenzi wa madarasa hayo kupitia utaratibu huu zinachangia hesabu ya madarasa kama ilivyowasilishwa na Waziri wa Nchi, OR-TAMISEMI, **Mhe. Innocent Lugha Bashungwa** wakati akiwasilisha Bungeni Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2022/23 hivyo kuleta msukumo wa maendeleo ya jamii kwenye Sekta ya Elimu.

25. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuboresha utoaji wa mafunzo ya Taaluma ya Maendeleo ya Jamii katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vya Buhare, Mlale, Misungwi, Rungemba, Mabughai, Ruaha, Uyole na Monduli kwa kusimamia ubora wa mafunzo na kuboresha miundombinu. Udahili wa wanafunzi umeongezeka kutoka wanafunzi 4,753 (Me 1,871 na Ke 2,882) mwaka 2020/21 hadi wanafunzi 5,135 (Me 2,112 na Ke 3,023) kufikia mwaka 2021/22 ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 382 sawa na asilimia 8. Aidha, mwaka 2020/21, wanafunzi 2,759 walihitimu katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ikilinganishwa na wanafunzi 3,953 waliohitimu mwaka 2019/20 sawa na upungufu wa asilimia 30 ya wahitimu. Hii ni kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo kuahirisha masomo na kushindwa kulipa ada.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutatua changamoto hizo, Wizara imefanya jitihada mbalimbali ikiwemo kuwaunganisha wanafunzi na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanayosaidia wanafunzi wanaoishi katika mazingira magumu yakiwemo; *Compassion*, CAMFED, Tumaini Fund, *Black School Learning*, SEMA Singida, *King Lion* na Ngorongoro *Community-Based Organization*. Aidha, wanafunzi wengine wamekuwa wakiunganishwa na Mikoa na Halmashauri ili kuwawezesha kuendelea na masomo kupitia mafungu ya kuwasaidia wanafunzi wasio na uwezo. Hadi Aprili 2022, jumla ya wanafunzi 29 wasio na uwezo wa kulipa ada wameunganishwa na Mashirika mbalimbali ambapo wamewezeshwa kuendelea na masomo yao.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuboresha utoaji wa mafunzo ya Taaluma ya Maendeleo ya Jamii katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru (TICD) na Vyuo nane (8) vya Maendeleo ya Jamii (CDTIs) kwa kutekeleza dhana ya Uanagenzi ili kuzalisha wahitimu wenye weledi na umahiri unaoendana na soko la ajira. Uanagenzi (*apprenticeship*) ni programu ya kukuza ujuzi ambapo vyuo huwaunganisha wanafunzi/wahitimu wake na Kampuni, Mashirika na Taasisi mbalimbali ili waweze kupata ujuzi/kujengewa uwezo katika eneo fulani kulingana na mahitaji yao. Programu hii ilianzishwa rasmi mwaka 2019/20. Aidha, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi Ibara ya 22 (a) ukurasa wa 22 imehimiza kuongeza ujuzi wa mafunzo kwa vitendo kwa vijana ili kuwasaidia





vijana kujiajiri, kuajiriwa na kuajiri wengine.

28. ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya wanafunzi na wahitimu wa Vyuo 721 walijiunga na programu ya uanagenzi mwaka 2021/22 ambapo kati ya hao, vijana 114 sawa na asilimia 16 wamehitimu programu ya uanagenzi katika mwaka huu wa fedha na kupata ujuzi katika maeneo ya ujasiriamali, ujenzi wa barabara, usimamizi wa miradi, uandishi wa maandiko ya miradi, uelimishaji rika na ujenzi wa majengo. Aidha, kati ya hao, vijana 40 wamepata ajira (27 wamejiajiri na 13 wameajiriwa katika Kampuni na Mashirika mbalimbali) na wengine 607 bado wanaendelea na programu ya uanagenzi. Katika mwaka 2022/23, vyuo vinatarajia kupeleka wanafunzi 931 kujifunza mafunzo mbalimbali kwenye Kampuni, Mashirika na Taasisi 334. Kwa maelezo hayo, ni dhahiri kuwa Wizara imejielekeza kwenye mapinduzi ya mafunzo ili wahitimu waweze kujiajiri na kuajiri.

29. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inatekeleza programu ya ushirikishaji jamii zinazozunguka Taasisi na Vyuo nane vya Maendeleo ya Jamii kutatua changamoto zinazowakabili kwa kutumia rasilimali zinazowazunguka kama ifuatavyo: elimu ya lishe imetolewa kwa wananchi 825 wanaozunguka Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vya Rungemba na Ruaha; na hamasa ya kilimo cha parachichi imetolewa na Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba katika Vijiji vya Kitelewasi, Itimbo na Rungemba ambapo jumla ya miche 6,120 imepandwa katika Vijiji hivyo. Pia, elimu ya ujasiriamali imetolewa kwa wananchi 376 wanaozunguka Vyuo vya Maendeleo ya Jamii vya Mlale na Monduli. Aidha, mafunzo ya ufundi ujenzi yametolewa na Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ufundi Misungwi kwa mafundi 40.

***Napenda kutoa wito kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii waliopo katika ngazi ya Mkoa, Halmashauri na Kata kushirikiana na wadau wengine wote na kuendelea kwa kasi zaidi kuelimisha na kushirikisha jamii kuimarika katika dhana nzima ya utekelezaji wa shughuli za maendeleo.***

30. ***Mheshimiwa Spika,*** *napenda kutoa shukrani za dhati kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kwa kuipatia Wizara fedha za maendeleo kiasi cha* **Shilingi Bilioni 3.6** *kwa ajili ya ukarabati wa majengo na miundombinu katika Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Hatua hii itaboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Vyuo hivyo.*

31. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na juhudi zote za ushirikishaji jamii zinazofanywa na Maafisa Maendeleo ya Jamii nchini, bado tunakabiliana na changamoto ya uhaba wa Maafisa hao. Jumla ya Maafisa Maendeleo ya Jamii 5,296 wanahitajika nchini. Hadi mwezi Aprili 2022, Maafisa waliopo katika ngazi ya Mkoa, Halmashauri na Kata ni 3,014 ambapo upungufu ni Maafisa 2,282 sawa na asilimia 43 kama inavyoonesha katika **Jedwali Na. 1**. Mahitaji makubwa zaidi ya wataalam hawa yapo ngazi ya Kata ambapo kuna changamoto nyingi za jamii zinazopaswa kushughulikiwa.

**Jedwali Na. 1:** Idadi ya Maafisa Maendeleo ya Jamii katika Ngazi Mbalimbali

| NA. | NGAZI | MAAFISA WANAOHITAJIKA | MAAFISA WALIOPO | | UPUNGUFU / ZIADA | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | IDADI | % | IDADI | % |
| 1. | Mkoa | 52 | 51 | 98 | -1 | -2 |
| 2. | Halmashauri | 1,288 | 1,329 | 103 | 41 | 3 |
| 3. | Kata | 3,956 | 1,634 | 41 | -2,322 | -59 |
| | **JUMLA** | **5,296** | **3,014** | **57** | **-2,282** | **-43** |

**Chanzo:** *OR-TAMISEMI*

32. ***Mheshimiwa Spika***, ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa Maafisa Maendeleo ya Jamii, Wizara itaendelea kuwasiliana na OR-TAMISEMI pamoja na OR-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kutatua changamoto ya upungufu wa Maafisa hao katika ngazi ya Kata kwa kuwaajiri kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kadiri bajeti ya Serikali itakavyoruhusu kila mwaka.

***Nitoe rai kwa Wadau wa Maendeleo yakiwemo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutoa ajira za muda kwa Maafisa Maendeleo ya Jamii hususan katika ngazi ya Kata ambapo kuna upungufu mkubwa ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa afua za kutatua changamoto zinazoikabili jamii yetu. Pia, Wizara inatoa wito kwa wote wenye taaluma ya maendeleo ya jamii ambao wapo katika jamii baada ya kustaafu wajitokeze ili kuendelea kutoa mchango wao kwenye jamii kama ambavyo taaluma zingine zimekuwa zikifanya. Lengo ni kila mzalendo mwenye nafasi na nia ya kuchangia maendeleo ya jamii apewe nafasi.***

33. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Vyuo nane vya Maendeleo ya Jamii vya Buhare, Monduli, Rungemba, Ruaha, Uyole, Mlale, Misungwi na Mabughai imeendelea kutekeleza programu mbalimbali zinazolenga kukuza ubunifu na maarifa. Ubunifu na Maarifa ni programu ambayo wanafunzi na jamii inayozunguka vyuo wanapewa fursa ya kutoa mawazo yao ya kibunifu ambayo yanalenga kutatua changamoto fulani katika jamii ambapo mawazo hayo hulelewa ili yafikie hatua ya kuwa huduma au bidhaa iliyokusudiwa. Programu zinazotekelezwa katika Taasisi na Vyuo hivyo ni pamoja na: kutoa uelewa kwa wananchi kuhusu uwepo wa nafasi za kupokea na kulea mawazo ya kibunifu kwenye vituo na umuhimu wa ubunifu katika kuongeza kipato chao; kuwajengea uwezo wanafunzi na wananchi katika eneo la ubunifu kwa kuwaunganisha na wabunifu wakubwa pamoja na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali; na kuwaunganisha wabunifu na masoko kwa ajili ya kutangaza na kuuza bidhaa/huduma zinazotokana na ubunifu wao.

34. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya mawazo ya kibunifu saba (7) yameibuliwa na hivyo kuwa na jumla ya mawazo ya kibunifu 61 tangu kuanzishwa kwa dhana ya ubunifu na maarifa mwaka 2019/20. Kati ya hayo, mawazo ya kibunifu 23 (sawa na asilimia 38) yamekamilika na yapo kwenye hatua za mwisho kuwa bidhaa au huduma. Huduma/bidhaa hizo ni pamoja na: kifaa cha kugundua madini ardhini katika Chuo cha Maendeleo Jamii Ufundi Misungwi ambapo mbunifu ametengeneza sampuli kifani na Chuo kimeshirikisha Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) ili kukamilisha wazo hilo kuwa bidhaa; mashine ya kuchakata viazi katika Chuo cha Maendeleo Jamii Ufundi Misungwi ambapo Chuo kimeshirikisha SIDO kukamilisha wazo hilo; na mashine ya kusukuma maji inayotumia nishati ya maji katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Mlale ambapo mbunifu huyo amefanikiwa kutengeneza mashine tatu na kuziuza kwa kiasi cha **Shilingi Milioni 2.2** kila moja. Aidha, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru imeanzisha huduma ya ***web application*** kwa ajili ya kusaidia uuzaji, utunzaji wa hesabu na kutangaza masoko ya bidhaa za wajasiriamali.

35. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa shukrani kwa COSTECH kwa kutoa mafunzo ya namna ya kuanzisha, kusimamia na kuviendesha vituo vya kidijitali vya ubunifu na maarifa katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Aidha, Wizara inaendelea kushirikiana na Maafisa Maendeleo ya Jamii kuhamasisha jamii kwenda kwenye vituo vya kidijitali vya ubunifu na maarifa kwa kuonesha vipaji vya kibunifu walivyonavyo na kufanya uhamasishaji kwa Taasisi za elimu ya juu, kati na Sekondari ili kuongeza mwitikio wa jamii kujiunga katika vituo hivyo. Wizara inaendelea kutafuta wadau kwa ajili ya kufadhili wabunifu kufikia malengo yao.

**ENEO LA 2: HAKI NA MAENDELEO YA MTOTO**

36. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha kwamba vitendo vya ukeketaji kwa watoto wa kike na wanawake vinatokomezwa, Wizara imeshirikiana na wadau kuandaa Mkakati wa Taifa wa Kutokomeza Ukeketaji utakaotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2020/21 – 2024/25. Mkakati unalenga kupunguza ukeketaji nchini kutoka asilimia 10 mwaka 2015/16 hadi asilimia 5 mwaka 2021/22 na hatimaye kutokomeza ukeketaji ifikapo mwaka 2024/25. Mkakati huo utafikia malengo yake iwapo: (i) Wasichana na wanawake watakataa vitendo vya ukeketaji; (ii) Msaada na huduma zitapatikana kwa waathirika wa ukeketaji kwa wakati; (iii) Familia zitakataa kuwatoa watoto wao wa kike kwa ajili ya kukeketwa; (iv) Jamii zitapinga na kukataa ukeketaji ikiwemo jamii ya wanaume wa rika zote; (v) Ngariba wengi watakataa na kuacha vitendo vya ukeketaji; na (vi) Uratibu wa wadau katika kushughulikia masuala ya ukeketaji utaimarishwa. Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Kutokomeza Ukeketaji utachangia katika utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008; Sera ya Maendeleo ya Wanawake na Jinsia ya mwaka 2000; Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 na Sheria mbalimbali zikiwemo Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 na marekebisho yake ya mwaka 2019; na Sheria ya Kanuni ya Adhabu, Sura ya 16 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2018.

37. ***Mheshimiwa Spika,*** ukeketaji una madhara makubwa katika maendeleo na ustawi wa jamii. Madhara hayo ni pamoja: maumivu makali kwa mtoto (ukatili wa kimwili); kutokwa damu nyingi kwa mtoto jambo linaloweza kusababisha kupoteza maisha; na kovu la kudumu linalosababisha maumivu wakati wa kujamiiana na hatimaye kupoteza hisia na kusababisha migogoro katika ndoa. Aidha, ukeketaji unaweza kusababisha kupata magonjwa kama Fistula (kutokwa na haja ndogo mara baada ya kujifungua) na maambukizi katika njia ya mkojo (UTI).

38. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau wa ukeketaji inaratibu utendaji wa Muungano (coalition) wa Taifa wa utekelezaji wa afua za Kutokomeza Ukeketaji Nchini. Muungano huo unajumuisha watendaji wa Wizara za Kisekta, Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na Wadau wengine wa masuala ya ukeketaji. Vilevile, Wizara inaratibu utekelezaji wa Maazimio na Mpango Kazi wa Kushughulikia Ukeketaji Mipakani mwa nchi za Afrika Mashariki. Mpango huo unalenga kuzuia vitendo vya ukeketaji wa kuvuka mipaka ambapo familia zinawavusha watoto kwenda nchi jirani kwa kuhofia vyombo vya dola kuwachukulia hatua. Hadi kufikia mwezi Aprili, 2022 jumla ya Kamati tano (5) za Ulinzi na Usalama katika Wilaya za Tarime (Sirari), Longido (Namanga), Mkinga (Hororo), Rombo (Holili) na Serengeti zimejengewa uwezo ili kukabiliana na vitendo vya ukeketaji wa kuvuka mipaka. Serikali kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutekeleza afua za kutokomeza ukeketaji katika mikoa yenye takwimu za juu ambayo ni Manyara kwa asilimia 58; Dodoma asilimia 47; Arusha asilimia 41; Mara asilimia 32; na Singida asilimia 31. Afua hizo zimewezesha takribani ngariba 1,800 katika mikoa hiyo kusalimisha zana za ukeketaji na kuachana na vitendo hivyo kwa kipindi cha mwaka 2015/16 hadi kufikia Aprili, 2022.

39. ***Mheshimiwa Spika***, katika kukabiliana na aina mpya ya Ukatili dhidi ya Watoto Mitandaoni unaosababishwa na kukua kwa maendeleo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), Serikali imeunda kikosi kazi cha Taifa cha Ulinzi na Usalama wa Mtoto mtandaoni chenye lengo la kuhakikisha kuwa watoto wanalindwa dhidi ya ukatili wa mtandaoni na kuwasaidia kutumia vifaa vya kieletroniki kwa usahihi na usalama. Pia, Kikosi Kazi kina jukumu la kuratibu wadau katika Serikali na Sekta Binafsi kuhuisha masuala ya ukatili dhidi ya watoto mtandaoni na utekelezaji wa Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015 na Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009. Aidha, Serikali imeandaa machapisho/majarida ya kufundishia watoto, wazazi na walimu kuhusu ukatili wa watoto mtandaoni.

40. ***Mheshimiwa Spika***, katika kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 na Kanuni zake, Wizara imebaini kuwa kuna uhitaji wa kuifanyia marekebisho Sheria hiyo ili iweze kuakisi mazingira ya sasa ikiwa ni pamoja na ukatili wa watoto mtandaoni (*online child abuse*). Ili kutekeleza hilo, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Mwandishi Mkuu wa Sheria) imeshaandaa mapendekezo ya marekebisho ya Sheria na kuyawasilisha kwa wadau ili kutoa maoni ambapo tayari Wizara imeanza kupokea maoni. Mchakato wa marekebisho ya Sheria hiyo unatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Desemba, 2022. Pia, Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari inayosimamia Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015 inafanya mapitio ya Sera ya hali ya usalama katika mitandao ili kubaini maeneo ya kuboresha. Aidha, ifikapo mwezi Oktoba, 2022 zoezi la tathmini litakuwa limekamilika na litatoa mwelekeo wa kuandaa Sera na Sheria mpya ya Makosa ya Mtandao.

41. ***Mheshimiwa Spika***, mwezi Machi 2022, Wizara ilizindua Taarifa ya Utafiti kuhusu Hali ya Ukatili wa Watoto Mtandaoni nchini (*Disrupting Harm Report in Tanzania*). Utafiti huo ulifanywa mwaka 2021 kwa ushirikiano wa Mashirika yafuatayo: Shirika la kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF – Tanzania), Shirika la ECPAT International na INTERPOL kwa uratibu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya usimamizi wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Aidha, nchi nyingine 12 za Afrika zilifanya utafiti kama huu kutoka Barani Afrika (Nchi 6 kutoka Mashariki na Kusini mwa Afrika na 6 Kusini Mashariki mwa Bara la Asia). Taarifa hiyo inaeleza tathmini ya kina ya hali ya ukatili nchini, athari za ukatili wa kingono, mitazamo ya watoto juu ya ukatili wa kingono mtandaoni na mwitikio wa kitaifa wa namna ya kupambana na aina hii ya ukatili. Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa: -

(i) Asilimia 4 ya watumiaji wa mtandao wenye umri wa miaka 12 – 17 nchini Tanzania ni manusura wa ukatili wa mtandaoni;
(ii) Watoto wengi hufanyiwa vitendo vya ukatili kupitia mitandao ya kijamii kama vile WhatsApp, Instagram, Facebook, Tik Tok;
(iii) Wanaofanya vitendo vya ukatili ni watu wanaofahamika na watoto wakiwemo ndugu wa karibu na marafiki; na
(iv) Watoto wanaofanyiwa ukatili hawajui namna na sehemu ya kutoa taarifa ili wapate msaada.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha Malezi na Makuzi Jumuishi ya Watoto wa umri wa miaka 0 - 8 ambao ndio umri muhimu sana katika ukuaji wa ubongo wa binadamu, Wizara imezindua Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT- MMMAM) itakayotekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2021/22 – 2025/26). Programu hii inalenga kutatua changamoto za ukuaji na maendeleo ya watoto wenye umri wa miaka 0-8 na kuhakikisha watoto wote Tanzania wapo kwenye mwelekeo sahihi wa kufikia ukuaji timilifu. Pia, Programu ya MMMAM inalenga kuharakisha upatikanaji wa matokeo chanya kwenye malezi na makuzi ya watoto kwa kuhimiza ushiriki wa Sekta mbalimbali katika kutoa huduma za malezi jumuishi kwa watoto kwenye maeneo makuu matano (5) ambayo ni: ***Afya bora kwa Mtoto na Mama/Mlezi; Lishe ya kutosha kuanzia Ujauzito; Malezi yenye Mwitikio; Fursa za Ujifunzaji wa Awali; na Ulinzi na Usalama.*** Aidha, ili kuhakikisha programu hiyo inaleta matokeo chanya kwa watoto wadogo, itatekeleza mambo makuu manne ambayo ni: kuboresha mazingira wezeshi ili kuwezesha uratibu wenye ufanisi na utoaji wa huduma za malezi jumuishi; kuimarisha mifumo ya utoaji wa huduma jumuishi za MMMAM na uthibiti ubora; kuongeza upatikanaji wa huduma bora na zilizoratibiwa za malezi jumuishi kwa watoto wenye umri wa miaka 0-8 na walezi wao; na kuwawezesha wazazi, walezi, familia na jamii kutoa huduma za malezi jumuishi.

43. ***Mheshimiwa Spika,*** katika hatua za awali za utekelezaji wa Programu ya MMMAM, mwezi Desemba 2021, mafunzo ya uelewa kuhusu Programu hiyo yalitolewa kwa Watendaji wa Sekretarieti za Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara ambapo kila Mkoa uliwakilishwa na watendaji watano (5) wakiwemo Maafisa Maendeleo ya Jamii, Maafisa Ustawi wa Jamii, Waganga Wakuu, Maafisa Elimu na Maafisa Lishe wa Mikoa. Pia, mafunzo hayo yalitolewa kwa wanahabari vinara wa Programu hiyo ili kuwajengea uwezo wa kutoa taarifa za utekelezaji wake. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilijenga hamasa kwa Waheshimiwa Wabunge ambao wameanzisha Kikundi cha Wabunge Vinara (*champions*) wapatao 30 kuwa Mabalozi katika kusukuma Ajenda ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto ndani na nje ya Bunge. Kikundi hicho kinaongozwa na **Mhe. Dkt. Pius Chaya** (Mwenyekiti), **Mhe. Esther Matiko** (Makamu Mwenyekiti) na **Mhe. Justine Nyamoga** (Katibu). Aidha, kikundi hicho kimeandaa Katiba na Mpango Mkakati wa Miaka Mitatu (3) utakaowaongoza katika kutekeleza majukumu yao. **Nitumie fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge hawa kwa kujitolea kusukuma Ajenda hii muhimu katika Nchi yetu inayolenga kuimarisha malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya Mtoto**.

44. ***Mheshimiwa Spika,*** ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la BRAC Maendeleo imeratibu ujenzi wa Vituo 30 vya mfano vya Kijamii vya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (*Community-Based Early Childhood Development Centers*) katika Mikoa ya Dar es Salaam (10) na Dodoma (20). Vituo hivyo vina lengo la kutoa huduma jumuishi za Malezi na Makuzi kwa Watoto walio na umri kuanzia miaka miwili (2) hadi chini ya miaka mitano (5) kwa kuwapatia huduma jumuishi za afya, lishe, ulinzi, ujifunzaji na uchangamshi wa awali kabla ya kujiunga na darasa la awali. Katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya Vituo vya mfano 15 kati ya 30 vimeanza kufanya kazi na jumla ya watoto 883 (Wavulana 426 na Wasichana 457) wamesajiliwa na kupatiwa huduma katika Vituo hivyo kama inavyoonesha katika **Kiambatisho Na. 1**. Aidha, vituo hivyo vitatumika kama mfano katika ujenzi wa vituo vingine vitakavyojengwa katika Vijiji/Mitaa yote ya Tanzania Bara.

45. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha Programu hii ina mfumo madhubuti wa kukusanya na kutunza taarifa za utekelezaji, Wizara kwa kushirikiana na UNICEF na Wataalam wa Mifumo kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam imetengeneza Dashbodi ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (*ECD Dashboard*) ambayo itawezesha ukusanyaji na utunzaji wa taarifa mbalimbali zinazohusu masuala ya Lishe, Afya, Fursa za Ujifunzaji wa Awali, Malezi yenye Mwitikio, Ulinzi na Usalama kwa Watoto wenye umri kati ya miaka 0-8. Aidha, Dashbodi hii imeunganishwa na mifumo mbalimbali inayotoa taarifa zinazohusu watoto wadogo.

46. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kushughulikia changamoto zinazowakabili vijana balehe wenye umri wa kati ya miaka 10 - 19, Wizara imeandaa na inatekeleza Ajenda ya Kitaifa ya Kuwekeza katika Afya na Maendeleo kwa Vijana Balehe nchini (2021/22-2024/25). Ajenda imeandaliwa kwa ajili ya kutatua changamoto za upatikanaji wa huduma rafiki za afya na kuondoa vikwazo vya maendeleo kwa vijana balehe nchini ambapo makadirio ya idadi ya vijana balehe kwa mwaka 2020 ni milioni 13 sawa na asilimia 23 ya watu wote nchini. Ajenda hii imejikita katika nguzo kuu sita (6) ambazo ni: Kuzuia Maambukizi ya Virusi Vya UKIMWI; Kutokomeza Mimba za Utotoni; Kuzuia Ukatili wa Kimwili, Kisaikolojia na Kingono; Kuboresha Lishe, Kuhakikisha Watoto wa Kike na Kiume Wanabaki Shule; na Kuwajengea Vijana Balehe Ujuzi na Uwezo wa Kufikia Fursa za Kiuchumi.

Ajenda imejikita katika kutekeleza afua za kipaumbele zitakazoleta matokeo makubwa katika kipindi cha muda mfupi na muda wa kati. Pia, afua saidizi na afua nyinginezo zitakazoibuka zitatekelezwa katika muda wa kati na muda mrefu. Afua zinazohitajika katika kuboresha afya na maendeleo ya vijana balehe zinagusa maeneo mahsusi ya **Mahitaji, Usambazaji na Mazingira Wezeshi**. Kwenye eneo la **Mahitaji,** afua zinalenga kuboresha elimu, kupunguza kiwango cha umaskini, kupunguza athari zitokanazo na mila na desturi zenye viashiria vya kibaguzi katika jamii. Kwa upande wa **Usambazaji,** afua zinalenga kuongeza wigo wa huduma bora na rafiki za afya kwa vijana balehe. Aidha, **Mazingira Wezeshi** yanalenga kutoa elimu na ujuzi kwa vijana ili kuondokana na vikwazo vinavyosababisha vijana balehe kushindwa kushiriki katika shughuli za kijamii, kiuchumi na kiutamaduni.

Katika kuratibu na kutekeleza Ajenda hii, Wizara kwa hisani ya Shirika la UNICEF imeajiri Mtaalam Mshauri (*Individual Consultant*) kwa kipindi cha mwaka mmoja (Mei, 2022 - Aprili, 2023) ili kwa kushirikiana na Wataalam wa Wizara kuratibu na kusimamia utekelezaji wa ajenda hiyo. Vilevile, Mtaalam huyo atawajengea uwezo wataalam wetu katika uratibu na utekelezaji wa Ajenda hii baada ya kumaliza muda wake.

Uratibu na utekelezaji wa Ajenda utakuwa jumuishi na **utahusisha wajumbe kutoka Wizara za Kiseka, Idara za Serikali, Vijana balehe na Sekta Binafsi** ikiongozwa na Wizara mtambuka na yenye dhamana ya watoto na vijana balehe Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum. Uratibu utakuwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu) kupitia kamati elekezi ya Taifa ambayo itawahusisha Makatibu Wakuu wa Taasisi za Serikali.

47. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha Elimu ya Malezi Chanya kwa Wazazi na Walezi, Wizara kupitia Kitini cha Elimu ya Malezi katika Familia imetoa elimu ya malezi chanya katika mikoa nane (8) ya Kigoma, Kilimanjaro, Songwe, Iringa, Mwanza, Tanga, Mtwara na Mbeya ambapo jumla ya wazazi/walezi 800,000 walifikiwa. Vilevile, Wizara imeandaa Ajenda ya Taifa ya Wajibu wa Wazazi na Walezi katika Matunzo ya Watoto na Familia. Kupitia Ajenda hiyo Wizara imeandaa jumbe mahsusi za kuelimisha wazazi wote wawili kushiriki kikamilifu katika malezi ya watoto. Ajenda imeandaliwa katika nguzo tatu ambazo ni: (i) Mjali Mtoto kwa kumpatia huduma zote za msingi; (ii) Mlinde Mtoto dhidi ya Ukatili; na (iii) Wasiliana na Mtoto mara kwa mara ili kuwa huru kueleza changamoto za makuzi yake na maendeleo kwa ujumla.

48. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha jumbe hizo zinafika kwa wazazi na walezi wengi na kwa ubora, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la PACT Tanzania na NIMR Mwanza imetambulisha na kufanya utafiti wa mbinu mpya ya utoaji elimu ya malezi kwa njia ya kidijitali kupitia simu zenye programu tumizi (***apps***) katika Mikoa ya majaribio ya Mwanza na Shinyanga. Programu tumizi itawezesha wazazi na walezi kupata ujuzi wa malezi bora na kubadilishana taarifa za malezi, makuzi na ulinzi wa watoto katika ngazi ya familia na jamii. Programu hiyo imezinduliwa mwezi Mei 2022 na itasambazwa katika mikoa yote nchini kuanzia mwezi Julai, 2022.

***49. Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha watoto wanapata haki ya kushiriki na kushirikishwa kwenye masuala yanayowahusu, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeanzisha Mabaraza ya Watoto kuanzia ngazi ya Mtaa/Kijiji, Mkoa na Taifa. Mabaraza ya Watoto ni jukwaa la watoto lililoanzishwa kwa lengo la kuwashirikisha watoto katika masuala yanayowahusu ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mikataba ya Kimataifa na Kikanda ambayo nchi yetu ilisaini na kuridhia. Aidha, ni utekelezaji wa Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 2008, inayobainisha Haki ya Kushiriki kuwa ni moja ya haki za msingi za Watoto.

50. ***Mheshimiwa Spika,*** Mabaraza ya Watoto ni jukwaa linalotumika katika kuwaelimisha watoto masuala mbalimbali yanayohusu maisha yao ya sasa na baadaye nje ya mfumo rasmi wa elimu, ikiwa ni pamoja na uongozi, uadilifu, uzalendo kwa Taifa lao na masuala mengine mtambuka ikiwa pamoja na VVU na UKIMWI, mazingira, stadi za kazi na usawa wa Kijinsia. Mabaraza ya Watoto yameimarisha uwezo wa watoto katika kujitambua, kujiamini, kujieleza na kujilinda dhidi ya ukatili wa aina mbalimbali. Wizara imeanzisha Mabaraza ya Watoto katika ngazi ya Mtaa/Kijiji, Mkoa na Taifa. Hadi Aprili 2022, jumla ya Mabaraza ya Watoto 2,669 yameanzishwa nchini ikiwa pamoja na Baraza la Watoto la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Baraza hilo linalojumuisha wajumbe wawili (2) kutoka katika kila mkoa kwenye Mikoa 26 ya Tanzania Bara na wajumbe 10 kutoka Tanzania Visiwani kwa kuzingatia uwiano wa jinsi zote.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na changamoto za uundaji wa Mabaraza ya Watoto, Serikali imefanya mapitio ya Mwongozo wa uundaji na uimarishaji wa Mabaraza ya Watoto wa mwaka 2010 ili kuboresha maeneo yaliyokuwa na changamoto. Moja ya eneo lililoboreshwa ni muundo wa mabaraza hayo kupelekwa katika ngazi za shule badala ya kuwa ni jukumu la Kijiji/Mtaa ambapo ufanisi wake umekuwa mdogo. Hivyo, Baraza la Watoto katika ngazi ya chini litakuwa katika shule za msingi na sekondari zilizopo katika Kijiji/Mtaa husika sambamba na uanzishwaji wa Klabu za Watoto shuleni. Uratibu na usimamizi wa Mabaraza ya Watoto utafanywa na Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na Afisa Elimu Wilaya na Kata kwa usaidizi wa Mkuu wa Shule au Mwalimu Mkuu. Kupitia Mabaraza hayo, watoto wamepata fursa ya kushiriki kwenye majukwaa mbalimbali ya

Kitaifa na Kimataifa na kutoa maoni kwenye nyaraka mbalimbali kama vile maandalizi ya Ajenda ya Wajibu wa Wazazi na Walezi katika Malezi Bora ya Familia na Watoto ya mwaka 2021. Aidha, mwezi Februari, 2022 wajumbe wa Baraza la Watoto la Taifa walipata fursa ya kipekee ya kushiriki katika kutoa maoni ya maboresho ya Mtaala wa Elimu kwa Shule za Msingi, Sekondari na Vyuo vya Ufundi Nchini unaoratibiwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Kisekta imedhamiria kuhakikisha watoto wa Taifa hili wanakuwa na ufahamu wa kutosha wa mambo yanayowahusu na hakuna anayekatisha ndoto zao kwa kutumia mwanya wa watoto kutofahamu haki zao.

52. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeratibu uandaaji wa Mwongozo wa Dawati la Ulinzi na Usalama wa Mtoto ndani na nje ya shule. Dawati hilo linaundwa na Watoto Vinara wanaochaguliwa na Watoto wenzao chini ya usimamizi wa Maafisa Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na Mkuu wa Shule kwa lengo la kuwezesha watoto kutoa huduma stahiki kwa wakati. Mwongozo huo umefanyiwa majaribio kwa kuanzisha Madawati 185 katika Halmashauri tatu (3) za Mkoa wa Rukwa (Nkasi, Sumbawanga na Mlele). Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI pamoja na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tumekubaliana kuendelea kuanzisha Madawati ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto kwenye Shule za Msingi na Sekondari nchini kuanzia mwezi Julai, 2022. Utekelezaji wa Mwongozo huu unaenda sambamba na Mwongozo wa Malezi, Unasihi na Ulinzi wa Mtoto Shuleni na kwenye Vyuo vya Ualimu ulioandaliwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na kuanza kutumika Mwaka 2020.

**ENEO LA 3: HUDUMA ZA USTAWI WA JAMII**

53. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha huduma za ustawi wa jamii kwa watoto, Wizara imeendelea kutoa huduma kwa watoto waliokinzana na sheria katika Halmashauri zote hapa nchini. Kwa kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya watoto 2,109 (Me 1,715 na Ke 394) walipatiwa huduma mbalimbali ikiwemo marekebisho ya tabia, unasihi, chakula, malazi, mavazi, huduma za matibabu, msaada wa kisaikolojia na wa kisheria na wengine kuwekwa chini ya uangalizi wa Maafisa Ustawi wa Jamii. Hadi kufikia mwezi Aprili 2022, jumla ya watoto 127 (Me 115 na Ke
12) walifuzu programu za marekebisho ya tabia ikilinganishwa na watoto 82 (Me 77 na Ke 5) kwa mwaka 2020/21. Aidha, Wizara imetoa huduma kwa watoto 257 (Me 232 na Ke 25) katika Mahabusu za Watoto tano (5) za Mbeya, Kilimanjaro, Tanga, Arusha na Dar es Salaam ikilinganishwa na watoto 413 (Me 380 na Ke 33) mwaka 2020/21 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 2**.

**Jedwali Na. 2:** Mwenendo wa Watoto walio katika Mahabusu za Watoto.

| MWAKA | WASICHANA | WAVULANA | JUMLA |
|---|---|---|---|
| 2015/16 | 37 | 349 | **386** |
| 2016/17 | 18 | 237 | **255** |
| 2017/18 | 13 | 278 | **291** |
| 2018/19 | 34 | 320 | **354** |
| 2019/20 | 18 | 120 | **138** |
| 2020/21 | 33 | 380 | **413** |
| Aprili, 2022 | 25 | 232 | **257** |

**Chanzo:** *WMJJWM*

Kupungua kwa idadi ya watoto katika Mahabusu za Watoto kunatokana na kuanzishwa kwa Programu za Kijamii za marekebisho ya tabia kwa watoto wanaokinzana na sheria ambayo inawachepusha watoto waliofanya makosa ya jinai kwa kutowashtaki Mahakamani na kuwaunganisha na huduma ya marekebisho ya tabia.

54. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia imeendelea kusimamia huduma ya marekebisho ya tabia kwa watoto waliobainika kufanya makosa ya jinai kupitia Shule ya Maadilisho Irambo Mbeya. Hadi kufikia mwezi Aprili 2022, watoto tisa (9) kutoka Shule hiyo wameunganishwa na familia zao katika Mikoa ya Njombe, Shinyanga, Iringa na Arusha baada ya kukamilisha hukumu za marekebisho ya tabia. Watoto hao ni miongoni mwa watoto 296 (Me 280 na Ke 16) waliopewa hukumu ya marekebisho ya tabia kupitia Mahakama mbalimbali za Watoto nchini baada ya kupatikana na hatia kwa makosa ya jinai ikilinganishwa na watoto 219 (Me 210 na Ke 9) waliopatiwa huduma hiyo mwaka 2020/21. Shule hii inatoa marekebisho ya tabia kwa watoto na kuwapatia ujuzi ili wanapokamilisha hukumu zao waweze kujitegemea na kuwa raia wema. Ninapenda kuwapongeza watumishi kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kuhakikisha kwamba watoto waliokinzana na sheria wanarejea kuwa na maadili mema na kuwa raia wema.

55. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha upatikanaji wa haki kwa watoto wanaokinzana na sheria, Wizara imefanya ufuatiliaji katika Magereza yaliyopo Mikoa ya Rukwa, Katavi, Dar es Salaam, Morogoro na Dodoma. Ufuatiliaji huu umewezesha watoto 16 kuachiwa huru kutoka Gereza Kuu la Segerea na kuwekwa chini ya uangalizi wa Maafisa Ustawi wa Jamii, Jijini Dar es Salaam. Watoto hao kesi zao zimekamilika ambapo baadhi yao wamepewa adhabu kulingana na kesi zao na kutozwa faini na wengine walipewa adhabu ya huduma kwa jamii. Mtoto mmoja (1) kati yao amepata ufadhili kutoka Kanisa la *Assemblies of God* Dar es Salaam kwa ajili ya kusoma masomo ya uchungaji ambapo ameshajiunga Chuo cha Uchungaji Mtama - Lindi.

56. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu imeendelea kuratibu huduma kwa Watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi hapa nchini ambapo jumla ya watoto 218,369 (Me 85,699 na Ke 132,670) walitambuliwa na kupewa huduma mbalimbali zikiwemo msaada wa Bima za Afya, Ada, Lishe, vifaa vya shule, kuunganishwa na familia pamoja na msaada wa kisaikolojia na matibabu. Huduma hizo zimetolewa kwa kushirikiana na Halmashauri na wadau mbalimbali. Hata hivyo, bado nchi yetu inakabiliwa na uwepo wa watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani.

57. ***Mheshimiwa Spika,*** utafiti uliofanyika mwezi Julai 2021 katika mikoa sita (6) ya Dodoma, Mwanza, Dar es Salaam, Mbeya, Arusha na Iringa ulibaini uwepo wa watoto 5,732 (Me 4,583 na Ke 1,149) wanaoishi na kufanya kazi mitaani. Sababu kuu za uwepo wa watoto hao ni pamoja na kuvunjika kwa ndoa, malezi hafifu kwa familia, msongo rika kati ya watoto wenyewe na umaskini wa kaya. Wengi wa watoto hao hukimbilia maeneo ya mijini na kufanya kazi mbalimbali zikiwemo kuosha magari, kuombaomba, kuuza bidhaa ndogondogo na wengine kuajiriwa katika kazi hatarishi ambazo zinadumaza maendeleo yao na kuwakosesha haki za msingi ikiwemo shule, malezi na afya bora.

58. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na wadau mbalimbali iliandaa hafla ya kihistoria ya chakula cha hisani kwa ajili ya kula pamoja na watoto waishio na kufanya kazi mtaani katika Jiji la Dar es Salaam. Lengo la hafla hiyo iliyofanyika mwezi Machi 2022 lilikuwa ni kuwaonesha watoto hao kuwa Serikali ipo pamoja nao licha ya changamoto wanazokumbana nazo. Pia, hafla hiyo ililenga kuwasilikiza na kupokea maoni na mapendekezo yao kupitia umoja wao pamoja na kutambua vipawa na vipaji vyao kupitia burudani, michezo na nyimbo mbalimbali zenye ujumbe mahsusi walizoimba wakati wa hafla na mwisho kupata mapendekezo ya pamoja ya namna bora ya kumaliza tatizo hilo.

Kupitia hafla hiyo, Wizara iliunda kikosi kazi chenye wajumbe kutoka Serikalini na Asasi za Kiraia kwa lengo la kutoa ushauri wa kitalaam wa namna ya kutatua tatizo la watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani. Kikosi kazi hicho kimeanza kazi na Wizara imekipatia Hadidu za Rejea ili kuja na ushauri wa namna bora zaidi ya kutokomeza tatizo la watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani hapa nchini. Kikosi kazi hicho kipo chini ya Mwenyekiti **Bw. David Mulongo**, Mkurugenzi wa Shirika la SOS Tanzania. Vilevile, namshukuru sana **Mhe. Amos Makalla**, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam ambapo Mkoa huo utakuwa wa mfano katika kukabiliana na changamoto ya watoto wanaoishi na kufanya kazi mtaani.

59. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 kama ilivyofanyiwa urekebu mwaka 2019, Kifungu cha 9 (3) kimetoa wajibu kwa mzazi na mlezi kumlinda na kumtunza mtoto katika maisha yake ya kila siku. Aidha, Kifungu cha 14 cha Sheria hiyo kimetoa adhabu kwa mtu yoyote atakayekiuka au kuvunja Sheria. Wizara imejipanga kuongeza kasi ya kuwafikia wazazi ambao hawakuwajibika ili hatua za kisheria zichukuliwe kwa wengi zaidi hivyo, natoa wito kwa kila mzazi kuhakikisha anatekeleza wajibu wake au kwa namna yoyote ile anahakikisha havunji sheria ya mtoto kwa kuweka mazingira mazuri ya mtoto husika. Aidha, natoa wito kwa Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto zilizopo ngazi zote kutekeleza majukumu yao kikamilifu na kuhakikisha wananchi wanazijua na kuzitumia. Lengo ni kila mtoto aishi maisha ya stahiki yake.

60. ***Mheshimiwa Spika,*** huduma za malezi ya kambo na kuasili zimeendelea kutolewa kwa watoto wasio na wazazi, walezi au ndugu. Huduma hii inalenga kuhakikisha kuwa watoto wanalelewa katika mazingira endelevu ya familia. Katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya watoto 46 (wavulana 27 na wasichana 19) walipata huduma ya malezi ya kambo na watoto 45 (wavulana 28 na wasichana 17) waliasiliwa. ***Natoa rai kwa wananchi wenye mapenzi mema kuwasilisha maombi ya kulea watoto wenye uhitaji wa malezi ya familia***.

61. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu huduma ya uendeshaji wa makao ya watoto hapa nchini. Katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya Makao 118 yamesajiliwa yakiwa na jumla ya watoto 1,524 (Me 668 na Ke 856). Idadi hii imewezesha kuwa na jumla ya Makao ya Watoto 301 yaliyosajiliwa nchini yakihudumia jumla ya watoto 11,341 (Me 5,713 na Ke 5,628). Aidha, Wizara imeendelea kusimamia Makao ya Watoto yanayomilikiwa na Serikali ambayo ni Makao ya Taifa ya Watoto Kikombo (Dodoma) yenye uwezo wa kuwahudumia watoto 250 na Kurasini Dar es Salaam yenye uwezo wa kuhudumia watoto 100 walio katika mazingira hatarishi. Makao ya Taifa Kikombo ni ya mfano kwa ukanda wa Afrika Mashariki. Ndani ya makao hayo kuna kituo cha kulelea watoto wadogo mchana ambacho kinahudumia watoto wanaozunguka eneo la makao. Pia makao yana maktaba, ukumbi wa mikutano, viwanja vya michezo mbalimbali, karakana, eneo la shamba lenye ukubwa wa hekari 15 na zahanati inayohudumia watoto na wananchi. ***Ninachukua fursa hii kuwapongeza Taasisi ya Abbott Fund Tanzania kwa msaada wao mkubwa wa kifedha katika kujenga makao haya ya Kikombo na ununuzi wa vifaa.***

62. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia huduma za malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana (Day Care Centers). Katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi Aprili 2022, Wizara imetoa leseni za uendeshaji kwa vituo 362 vikiwa na jumla ya watoto 9,638 (Wavulana 4,083 na Wasichana 5,555) wanaopata huduma ya malezi. Idadi hiyo imewezesha kuwa na jumla ya vituo 2,512 vilivyosajiliwa nchini ambavyo vinahudumia jumla ya watoto 173,032 (Wavulana 82,302 na Wasichana 90,730) kama inavyoonesha katika **Jedwali Na. 3**.

**Jedwali Na. 3**: Mwenendo wa Uandikishaji Watoto kwenye Vituo vya Kulelea Watoto Wadogo Mchana

| MWAKA | WASICHANA | WAVULANA | JUMLA |
|---|---|---|---|
| 2015/16 | 34,981 | 33,016 | **67,997** |
| 2016/17 | 39,790 | 33,791 | **73,581** |
| 2017/18 | 51,711 | 49,312 | **101,023** |
| 2018/19 | 76,094 | 72,999 | **149,093** |
| 2019/20 | 82,539 | 76,940 | **159,479** |
| 2020/21 | 85,175 | 78,219 | **163,394** |
| Aprili, 2022 | 90,730 | 82,302 | **173,032** |

**Chanzo:** *WMJJWM*

Aidha, Wizara imeendelea kuboresha utoaji wa huduma katika vituo vya kulelea watoto wadogo mchana kwa kutoa mafunzo kazini kwa Wamiliki wa Vituo na Walezi wa Watoto 1,566 (Me 431 na Ke 1,135) katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mbeya, Tabora, Shinyanga, Pwani, Shinyanga na Iringa ili kuimarisha stadi za uchangamshi wa awali na makuzi ya watoto wadogo pamoja na kutoa ulinzi wa uhakika kwa watoto wakiwa vituoni.

63. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia vyuo 33 vinavyotoa Mafunzo ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto vilivyotambuliwa na kupewa vibali vya kuendesha mafunzo hayo. Kati ya vyuo hivyo, chuo kimoja ni cha Serikali kilichopo Kisangara mkoani Kilimanjaro kinachotoa taaluma ya malezi na makuzi ya awali ya mtoto katika ngazi ya stashahada na vyuo 32 ni vya Watu Binafsi.

64. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kusimamia huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa na matunzo kwa watoto walio kwenye ndoa zenye migogoro na waliozaliwa nje ya ndoa kupitia Mabaraza ya Usuluhishi wa Ndoa nchini. Kwa kutambua hili, Serikali imeendelea kufanyia kazi mashauri ya migogoro ya ndoa kupitia Mabaraza ya Usuluhishi ambapo kwa kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya mashauri ya migogoro ya ndoa 39,571 yalipokelewa. Kati ya mashauri hayo, mashauri ya migogoro 4,576 yalifikishwa mahakamani, mashauri ya migogoro 19,262 yalisuluhishwa na kuwawezesha wanandoa kupata haki zao na mashauri 15,718 yanaendelea. ***Natoa wito kwa wanandoa kuzingatia kujifunza maadili ya ndoa kabla ya kupanga harusi kwani itaepusha migongano na migogoro ambayo mwisho wake inaumiza watoto wasio na hatia.***

65. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais – TAMISEMI imeendelea kuratibu uimarishaji wa utoaji wa Huduma za Ushauri na Msaada wa Kisaikolojia kwa familia na jamii. Huduma hii hutolewa kwa watu wenye misongo ya mawazo, manusura wa vitendo vya ukatili pamoja na migogoro ya ndoa na familia. Kwa kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya wahudumiwa 545,501 katika Makazi ya Wazee, Nyumba Salama, Mahabusu za Watoto, Makao ya Watoto, Vituo vya Mkono kwa Mkono, waathirika wa majanga mbalimbali ikiwa ni pamoja na UVIKO- 19, Janga la moto katika Soko la Karume, manusura wa vita vya Ukraine waliorejea nchini na wazazi wao, wanandoa na wanajamii mmoja mmoja aliyehitaji huduma hii. Aidha, Taasisi ya Ustawi wa Jamii - Dar es Salaam imeanzisha Kituo cha Msaada wa Kisaikolojia na Kijamii kwa lengo la kutoa huduma kwa wanafunzi, wafanyakazi na jamii kwa ujumla. Huduma hizi za Msaada wa Kisaikolojia zinatolewa na Maafisa Ustawi wa Jamii katika Halmashauri na vituo vya kutolea huduma za afya nchini. Wizara imeweka wazi simu za wataalam wake ngazi zote kuanzia Wizarani, Mikoani hadi Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya kusogeza wataalam hao karibu na jamii kwa njia ya teknolojia ya mawasiliano ya simu. Wananchi wengi wameendelea kuwasiliana na wataalam hawa na kupata msaada wa huduma za unasihi hata wakiwa mbali. Hii ni sambamba na **Simu Namba 116** bila malipo ambapo mamilioni ya wananchi wanaoona au kuhisi mazingira ya ukatili hutoa taarifa na kupata msaada na huduma ya unasihi.

66. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu imeendelea kuratibu uendeshaji wa Makazi ya Wazee hapa nchini. Kupitia huduma hii Wizara inaratibu makazi 14 yanayoendeshwa na Serikali ambapo hadi kufikia mwezi Aprili 2022, wazee wasiojiweza 271 (Me 160 na Ke 111) wamehudumiwa katika makazi hayo kama inavyoonesha katika **Kiambatisho Na. 2**. Aidha, Wizara imeendelea kuratibu Makazi ya Wazee yanayoendeshwa na watu binafsi na wakala wa hiari 20 yanayohudumia wazee wasiojiweza 451 (Me 216 na Ke 235). Wazee wasiojiweza wamekuwa wakiongezeka na kupungua kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na baadhi ya wazee kuunganishwa na familia zao pamoja na vifo. Hata hivyo, pamoja na huduma zinazotolewa, baadhi ya Makazi ya Wazee ya Serikali yanakabiliwa na uchakavu wa majengo na miundombinu. Wizara inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuendelea kuboresha majengo na miundombinu kwenye Makazi ya Wazee Misufini yaliyopo Wilaya ya Muheza mkoani Tanga. Makazi haya yakijengwa na kukarabatiwa yatakuwa ya mfano hapa nchini.

67. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kuboresha huduma kwa wazee, Serikali ina mpango wa kuanzisha Makazi ya Wazee Kikanda. Lengo ni kuhakikisha tunaboresha zaidi huduma kwa Wazee na kuwezesha kuwa na Makazi ya Wazee kwa uwiano wa kikanda. Awali huduma zilikuwa zinatolewa kwenye Makazi ya Wazee yaliyopo katika Mikoa mbalimbali bila kuzingatia uwiano wa Kikanda. Aidha, baadhi ya Mikoa ina Makazi zaidi ya moja, uwepo wa Wazee wachache kwenye Makazi na kukosekana wahudumu wa kutosha. Wizara inaendelea kutoa elimu kwa jamii ili familia ziweze kuwalea wazee wao na wale wachache watakaokosa huduma katika familia kupata matunzo katika makazi hayo. Vilevile, Serikali ipo katika mchakato wa kuanzisha miradi katika Makazi ya Wazee ili yaweze kupunguza utegemezi kwa Serikali.

68. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaratibu uanzishaji na uendeshaji wa Mabaraza ya Wazee nchini. Kwa kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi mwezi Aprili 2022, Wizara imeratibu uundwaji wa Baraza la Taifa la Ushauri la Wazee lenye wajumbe 31 ambapo watano (5) ni viongozi wa kitaifa na 26 ni wajumbe/wawakilishi kutoka kila Mkoa. Uzinduzi wa Baraza hilo ulifanyika rasmi tarehe 11 Machi, 2022 Jijini Dodoma. Vilevile, Wizara imekamilisha uundwaji wa Mabaraza ya Wazee katika mikoa ya Geita, Pwani, Rukwa na Njombe na hivyo kufikia lengo la kuwa na jumla ya Mabaraza 20,749 katika Mikoa 26 ya Tanzania Bara. Mabaraza hayo hutumika kama majukwaa ya wazee kwa ajili ya kujadili masuala yanayohusu haki zao pamoja na ushirikishwaji katika masuala yanayohusu maendeleo. Tarehe 17 – 19 Mei 2022, Wizara yangu kwa kushirikiana na Shirika la HelpAge International tuliwezesha Baraza la Wazee la Taifa kufanya kikao jijini Dodoma kwa lengo la kukusanya maoni ya mapitio ya Rasimu ya Sera ya Wazee pamoja na rasimu ya Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Mabaraza ya Wazee nchini. Aidha, jumla ya Wazee 1,547,038 wametambuliwa katika Mikoa 26 na kati yao wazee 937,266 wamepatiwa vitambulisho/ Bima ya Afya kwa ajili ya matibabu. Sambamba na hilo jumla ya madirisha 2,335 ya kutolea huduma kwa wazee yametengwa katika hospitali na vituo vya umma vya kutolea huduma za afya kote nchini.

Pia, Wizara imeendelea kuratibu maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wazee Duniani yanayofanyika tarehe 1 Oktoba kila mwaka ambapo kwa mwaka 2021 maadhimisho hayo Kitaifa yalifanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa Mkoa wa Dodoma. Jumla ya Wazee 291 kutoka katika Halmashauri nane (8) za Mkoa wa Dodoma walishiriki maadhimisho hayo ambapo Wazee 135 walipatiwa huduma za afya. Natoa shukrani za pekee kwa wadau wa masuala ya wazee wakiwemo HelpAge International na REDESO kwa ushiriki wao mkubwa katika kuwezesha shughuli mbalimbali za wazee. Aidha, naishukuru Wizara ya Afya kuendelea kusimamia upatikanaji wa huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini.

69. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na juhudi zote za utoaji wa huduma za ustawi jamii zinazofanywa na Maafisa Ustawi wa Jamii nchini, bado tunakabiliana na changamoto ya upungufu wa Maafisa 22,395 ambayo ni sawa na asilimia 97% ya Maafisa wanaotakiwa kama inavyoonesha katika **Jedwali Na. 4**.

**Jedwali Na. 4:** Idadi ya Maafisa Ustawi wa Jamii katika Ngazi Mbalimbali

| NA. | NGAZI | MAAFISA WANAOHITAJIKA | MAAFISA WALIOPO | | UPUNGUFU | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | IDADI | % | IDADI | % |
| 1. | Mkoa | 26 | 26 | 100 | 0 | - |
| 2. | Hospitali za Rufaa za Mikoa | 168 | 35 | 20.8 | -133 | - 79 |
| 3. | Halmashauri | 1,472 | 490 | 33.3 | -982 | - 67 |
| 4. | Hospitali za Wilaya | 549 | 65 | 11.8 | -484 | - 88 |
| 5. | Kata/Vituo vya Afya | 4,494 | 115 | 2.56 | -4,379 | - 97 |
| 6. | Kijiji/Mtaa / Zahanati | 16,426 | 9 | 0.05 | -16,417 | - 100 |
| **JUMLA** | | **23,135** | **740** | **3.2** | **-22,395** | - 97 |

**Chanzo:** *OR-TAMISEMI*

70. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kukabiliana na changamoto ya upungufu wa Maafisa Ustawi wa Jamii, Wizara itaendelea kuwasiliana na OR-TAMISEMI pamoja na OR-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kutatua changamoto ya upungufu wa Maafisa hao hususan katika ngazi ya Kata kwa kuwaajiri kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa kwa kadiri bajeti ya Serikali itakavyoruhusu kila mwaka.

***Nitoe rai tena kwa Wadau wa Maendeleo yakiwemo Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutoa ajira za muda kwa Maafisa Ustawi wa Jamii hususan katika ngazi ya Halmashauri, Kata na Kijiji/Mtaa ambapo kuna upungufu mkubwa ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa afua za kutatua changamoto za ustawi wa jamii nchini.***

**ENEO LA 4. MAENDELEO YA JINSIA NA UWEZESHAJI WANAWAKE**

71. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza ajenda ya usawa wa kijinsia, Wizara ilifanya uzinduzi wa Kamati ya Ushauri ya Kitaifa ya Utekelezaji wa Ahadi za Nchi kuhusu Kizazi Chenye Usawa (*Generation Equality Forum - GEF*) tarehe 16 Desemba, 2021 Jijini Dodoma ambapo Mgeni Rasmi alikuwa **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kamati hiyo ina wajumbe 25 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar. Pia, Sekretarieti ya GEF imeanzishwa kwa ajili ya kuratibu shughuli za kila siku za Jukwaa hilo. Katika kutekeleza malengo ya Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa, Tanzania imechagua kuwa kinara wa utekelezaji wa eneo la Haki na Usawa wa Kiuchumi. Aidha, Wizara inaendelea kuratibu ukamilishaji wa Andiko la Programu ya Utekelezaji wa Ahadi za Nchi kuhusu Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa ili iweze kuzinduliwa mwishoni mwa mwezi Juni, 2022. Sambamba na hilo, Wizara inaratibu maandalizi ya Mwongozo wa Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi utakaowezesha uundaji na uhuishaji wa Majukwaa hayo kuanzia ngazi ya Kijiji/Mtaa hadi Taifa ambao unatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 30 Juni, 2022. Mwongozo huo utakapokamilika na kuanza kutumika utachochea ufanisi wa utendaji kazi wa Majukwaa hayo na hivyo kuongeza kasi ya jitihada za Serikali katika kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi na kiuongozi. Vilevile, Jukwaa la Kitaifa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi linatarajiwa kuundwa na kuzinduliwa ifikapo tarehe 30 Juni, 2022 baada ya kukamilika kwa zoezi la kuhuisha majukwaa katika ngazi za mikoa.

72. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekamilisha Kanzidata inayolenga kuwezesha ukusanyaji na utunzaji wa taarifa zinazohusu wasifu, ujuzi na utaalam wa Wanawake katika nyanja mbalimbali hapa nchini ambapo uzinduzi wake ulifanyika tarehe 8 Machi, 2022 katika kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani. Kanzidata hii itawezesha utambuzi wa wanawake wenye sifa za kushika nafasi za uongozi na maamuzi ndani na nje ya nchi. Hadi kufikia mwezi Aprili 2022, jumla ya wanawake 978 walikuwa wamejisajili kwenye kanzidata hiyo kupitia ***https://twl.jamii.go.tz.*** Kanzidata hii inahusisha utunzaji wa taarifa za wanawake wenye wasifu mbalimbali kutoka Sekta ya Umma na Sekta Binafsi.

73. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara yangu inalo jukumu la kuratibu



maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani ambayo hufanyika kila mwaka ifikapo tarehe 8 Machi. Kwa mwaka 2022, Tanzania iliadhimisha Siku hii ambapo maadhimisho ya kimkoa yalifanyika katika Mikoa yote 26 Tanzania Bara. Wizara ilishiriki maadhimisho hayo katika mikoa ya Dodoma, Shinyanga na Arusha. Kaulimbiu ya maadhimisho kwa mwaka 2022 ilikuwa **"Kizazi cha Haki na Usawa kwa Maendeleo Endelevu: Tujitokeze Kuhesabiwa"**. Kaulimbiu hii ililenga kuhamasisha uwajibikaji kwa wote katika kuleta usawa wa kijinsia pamoja na kukumbushana umuhimu wa usawa wa kijinsia katika kuchochea ukuaji wa uchumi na maendeleo jumuishi. Kaulimbiu ilitoa fursa ya kutathmini utekelezaji wa Maazimio na Mikataba ya Kimataifa, Kikanda na Kitaifa yenye lengo la kuimarisha jitihada za kuleta amani, usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi. Vilevile, kaulimbiu ililenga kutoa wito kwa wananchi kuona umuhimu wa kujitokeza kuhesabiwa katika zoezi la Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika mwezi Agosti, 2022. Halikadhalika maadhimisho yalilenga kutathmini mafanikio na changamoto katika utekelezaji wa Maazimio ya Ulingo wa Beijing; Malengo ya Maendeleo Endelevu (2030) hususan Lengo Namba 5 linalohusu Usawa wa Jinsia; na Ajenda ya Afrika Tuitakayo (2063) pamoja na kujenga hamasa na ushiriki wa wananchi katika kuchangia na kuleta usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake. Aidha, maadhimisho haya hutoa fursa ya masoko kwa wanawake wajasiriamali ambapo katika wiki ya kuelekea kilele cha maadhimisho kuanzia tarehe 1 hadi 7 huwa ni wiki ya maonesho ya bidhaa zinazozalishwa na wanawake wajasiriamali.

74. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilishiriki kwenye Mkutano wa Sita (6) wa Kamati Maalum ya Mawaziri wa Umoja wa Afrika wanaoshughulikia masuala ya Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji Wanawake uliofanyika Addis Ababa, Ethiopia tarehe 1 Machi 2022. Lengo kuu la mkutano huo lilikuwa ni kuweka mashauriano ya nchi za Afrika kuhusu Mkutano wa 66 wa Kamisheni ya Wanawake Duniani (*Africa-Wide Consultation for the 66th Session of the Commission on the Status for Women - CSW66*). Mkutano huo ulikuwa ni sehemu ya maandalizi ya nchi za Afrika kushiriki Mkutano wa 66 wa Kamisheni ya Wanawake Duniani uliofanyika New York, Marekani kuanzia tarehe 14-25 Machi 2022. Kaulimbiu ya mkutano wa 66 wa Kamisheni ya Wanawake Duniani ni **Kufanikisha Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji Wanawake na Wasichana kwenye Sera na Programu za Kukabiliana na Maafa Yanayosababishwa na Mabadiliko ya Tabianchi na Mazingira**. Katika mkutano huo, ilikubaliwa kuwa nchi za Afrika ziweke mipango ya kitaifa ambayo inashirikisha kikamilifu wanawake kwenye juhudi za kukabiliana na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi na mazingira, kuwezesha ushiriki wa Wanawake na Wasichana kwenye nafasi za uongozi, kutokomeza ukatili wa kijinsia kwa wanawake na wasichana, kuongeza ufadhili na uwekezaji kwenye miradi ambayo inazingatia usawa wa kijinsia. Pia, nchi za Afrika zimekubaliana kuimarisha uwezo wa Taasisi za Takwimu za Kitaifa katika kukusanya takwimu na kuzitumia kutambua changamoto na fursa za wanawake na wasichana kushiriki katika kazi za uzalishaji kwenye sekta za kilimo na uchumi wa bluu. Sambamba na mkutano huo, Wizara kwa kushirikiana na Asasi za Kiraia za LANDESA na OXFAM zilifanya Mkutano wa Pembeni (*Side Event*) unaohusu *Promoting Women's Participation and Decision Making in Addressing Climate Change: Tanzania's Village Land Use Planning Framework* ambao ulifanyika tarehe 16 - 17 Machi, 2022 katika ukumbi wa Morena, Jijini Dodoma kwa njia ya mtandao ambapo jumla ya wadau 150 walishiriki mkutano huo.

75. ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania kupitia Wizara ninayoiongoza ilipokea mwaliko kutoka Ubalozi wa Ujerumani kushiriki Mkutano wa G7 uliofanyika Berlin, Ujerumani kuanzia tarehe 6 - 8 Aprili, 2022. Mkutano huo ulilenga kujadili masuala mbalimbali kuhusu ***Uzingatiaji wa Usawa wa Kijinsia na Uthaminishaji Mchango wa Wanawake Wanaofanya Kazi Zisizo na Ujira katika Uchumi wa Familia na Taifa***. Mkutano huo uliratibiwa na Shirika la UN Women kwa kushirikiana na Shirika la Kazi Duniani (ILO). Aidha, katika mkutano huo Tanzania ilipongezwa kwa juhudi kubwa inayoifanya katika utekelezaji wa lengo namba 5 la Malengo ya Maendeleo Endelevu linalohimiza kukuza ushiriki wa wanawake katika uongozi na nafasi za maamuzi na uwezeshaji wanawake kiuchumi na kuweza kuliweka suala la kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi kuwa moja ya vipaumbele vya Taifa.

76. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza majukumu yake ya uwezeshaji wanawake kiuchumi, Wizara imeendelea kuwajengea uwezo wanawake wajasiriamali ili kuwa na stadi za kufanya biashara. Katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya wanawake wajasiriamali 1,167 wamejengewa uwezo kupitia mafunzo yaliyotolewa katika Mikoa ya Shinyanga, Geita, Katavi na Tanga. Katika mafunzo hayo, wanawake walijengewa uwezo kwa kupatiwa elimu kwenye baadhi ya maeneo kama vile kodi, urasimishaji wa biashara, elimu ya hifadhi ya jamii na elimu ya viwango na ubora wa bidhaa. Pia, mbinu mbalimbali za kukuza mitaji pamoja na kupata masoko ya uhakika ya bidhaa zao zilitolewa kupitia Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo (SIDO), Taasisi za Fedha na Wakala wa Usajili wa Leseni na Biashara (BRELA). Mafunzo hayo yataendelea kutolewa kwa wanawake katika mikoa yote Tanzania Bara. Aidha, katika kuwezesha wanawake wajasiriamali kupata mitaji ya biashara, Dirisha la Wanawake katika Benki ya Biashara Tanzania (Tanzania Commercial Bank) limewezesha mikopo yenye thamani ya Shilingi 16,138,750,000 kwa wanawake 3,421 wa Tanzania Bara hadi kufikia mwezi Aprili, 2022.

77. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na vitendo vya unyanyasaji na ukatili wa kijinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati, Wizara imewezesha kuandaliwa na kuzinduliwa kwa Mwongozo wa Uanzishaji, Uendeshaji na Ufuatiliaji wa Dawati la Jinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati. Mwongozo huo ulizinduliwa na **Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb),** Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 25 Novemba 2021 ikiwa ni jitihada za Serikali za kuweka mfumo wa kushughulikia matukio ya unyanyasaji wa kingono na vitendo vya ukatili katika maeneo ya Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati. Hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya Madawati 13 yameanzishwa katika Vyuo 13 kati ya Vyuo 50 vilivyokusudiwa kufikiwa ifikapo Juni 2022. Vyuo hivyo ni; Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu cha Mzumbe, Chuo Kikuu cha Iringa, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST), Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ruaha, Chuo cha Maendeleo ya Jamii Buhare, Chuo Kikuu cha St. Augustine (SAUT) Mwanza, Chuo cha Mipango (IRDP) Dodoma na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi.

78. ***Mheshimiwa Spika,*** miongoni mwa jitihada zinazofanywa na Wizara katika kuhakikisha Madawati yanaanzishwa kwenye Taasisi za Elimu ya Juu na Elimu ya Kati ni pamoja na: -
   i. Kuvielekeza Vyuo kuhakikisha kuwa vinateua waratibu, wajumbe na kutenga sehemu maalum kwa ajili ya kutekeleza shughuli za Dawati;
   ii. Kuwajengea uwezo menejimenti za Vyuo na Waratibu wa Madawati ya Jinsia kuhusu namna bora ya uanzishwaji wa madawati hayo; na
   iii. Kufuatilia uanzishaji wa Madawati ya Jinsia katika Vyuo vya Elimu ya Juu na Elimu ya Kati ili kufikia lengo tarajiwa.

Aidha, Wizara imeweka mkakati wa kuhakikisha kuwa ifikapo Juni 2022, Vyuo 50 viwe vimeanzisha Madawati ya Jinsia na kuhakikisha yanafanya kazi. Katika kuwezesha hilo, Wizara inaratibu na kufuatilia matumizi ya Daftari lililoandaliwa mahsusi kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za taarifa za vitendo vya ukatili katika Taasisi za Elimu ya Juu na Kati. Vilevile, Wizara imeandaa Kitini cha Mafunzo kwa ajili ya kuwafundisha Waratibu na Wajumbe juu ya namna ya kuendesha Dawati hili.

**ENEO LA 5: URATIBU WA MASHIRIKA YASIYO YA KISERIKALI**

79. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia usajili, uratibu na ufuatiliaji wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ili yachangie katika kuleta maendeleo ya Taifa. Katika kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi Aprili 2022, Wizara imesajili jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,217 kati ya Mashirika 500 yaliyopangwa kusajiliwa kwa mwaka 2021/22. Ongezeko la idadi ya Mashirika yaliyosajiliwa linatokana na uboreshaji wa mfumo wa usajili unaowezesha wadau kufanya usajili wa Mashirika kwa njia ya kielektroniki. Aidha, elimu inayoendelea kutolewa kwa jamii kuhusu umuhimu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na mchango wake katika maendeleo ya nchi imechangia kuongezeka kwa usajili.

80. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilifanya zoezi la uhakiki wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa lengo la kupata idadi sahihi ya Mashirika yaliyo hai na yanayotekeleza shughuli zao kwa kuzingatia Sheria Na. 24/2002 ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kuhuisha kanzidata ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Jumla ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 2,479 yalihakikiwa na kutangazwa kwenye tovuti ya Wizara. Aidha, kutokana na Mashirika kuwa mengi na kusambaa nchi nzima, Wizara iliongeza muda wa uhakiki hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2022. Katika kipindi hicho cha nyongeza, jumla ya Mashirika 2,385 yalijitokeza kuhakiki na kufikia jumla ya Mashirika 4,864 yaliyohakiki. Hii imewezesha kanzidata ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuwa na Mashirika 7,533 yaliyo hai kati ya Mashirika 12,442 yaliyopo kwenye kanzidata ya Mashirika.

81. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali yanaratibiwa vizuri nchini, Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali imeanzisha Baraza la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ikiwa ni moja ya chombo cha uratibu wa Mashirika hayo. Chombo hiki ni asasi mwamvuli wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Uanzishwaji wa Baraza hilo umerahisisha uratibu wa Mashirika katika ngazi za Mikoa na Halmashauri kwa kuanzisha mitandao katika ngazi hizo, kuwepo kwa Kanuni za Maadili za Mashirika Yasiyo ya Kiserikali zenye kuimarisha uwazi na uwajibikaji na kuwezesha uwepo wa uwakilishi wa Sekta ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika Bodi ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Aidha, Baraza kwa kushirikiana na Serikali limewezesha kufanyika kwa Mkutano wa kwanza wa mwaka wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini mwaka 2021. Lengo la Mkutano huo ni kuimarisha ushirikiano baina ya Serikali na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali na kutambua mchango wa mashirika katika maendeleo ya nchi ikiwa ni utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali (2001) na Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2020 Ibara ya 127 (a) na (d). Mkutano huo ulizinduliwa rasmi na **Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan**, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 30 Septemba, 2021 Jijini Dodoma ambapo jumla ya Mashirika na Wadau 1,448 walishiriki.

82. ***Mheshimiwa Spika,*** wakati wa uzinduzi huo, Mheshimiwa Rais aliielekeza Wizara yangu kushirikiana na wadau wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kama hatua ya kupunguza utegemezi na kuyawezesha kuwa himilivu. Katika kutekeleza agizo hilo, Kamati ya kitaalam inayohusisha wajumbe 20 kutoka Serikalini na kwenye Mashirika hayo iliundwa mwezi Novemba 2021 ambapo mpaka sasa Kamati hiyo imefanikiwa kuandaa andiko la majadiliano na ushirikishaji wa wadau wa Sekta mbalimbali zikiwemo sekta binafsi na wadau wa maendeleo. Kupitia andiko hilo, nyenzo za kukusanyia taarifa zimeandaliwa na zimeanza kutumika kupokea maoni ya wadau nchi nzima katika Kanda tano (5) ambazo ni; Kanda ya Mashariki, Kanda ya Ziwa, Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini na Kanda ya Kati. Pia, Kamati imefanikiwa kuajiri Mtaalam Mwelekezi ili kukusanya na kuchakata taarifa na takwimu kisayansi ambapo jumla ya wadau 1,089 wamefikiwa kutoka katika Mashirika Yasiyo ya Kiserikali 1,015 sawa na asilimia 13.7 ya Mashirika 7,533 yaliyo hai. Hata hivyo, zoezi la ukusanyaji wa maoni ya wadau linaendelea kwa njia ya dodoso mtandao (*KoboCollect*). Aidha, Kikosi Kazi kinatarajia kuendelea kukusanya maoni ya wadau kutoka Sekta Binafsi pamoja na wadau mbalimbali wa maendeleo (DPGs). Vilevile, mchakato wa uandaaji wa andiko la Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali unatarajiwa kukamilika ifikapo tarehe 30 Julai, 2022.

83. ***Mheshimiwa Spika,*** Sambamba na uzinduzi wa Mkutano huo, Taarifa ya Mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya mwaka 2020 ilizinduliwa ambayo ilibainisha kuwa **Shilingi Trilioni 1.1** zilitumika katika utekelezaji wa miradi ya afya, elimu, hifadhi ya jamii, uwezeshaji kiuchumi, utawala bora, mazingira, maji, jinsia na haki za binadamu ambapo jumla ya wanufaika 49,697,214 walifikiwa pamoja na kutoa ajira kwa

Watanzania 8,918.

84. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha uratibu, usajili na usimamizi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, Wizara imekamilisha ujenzi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa asilimia 100 ambapo umeshaanza kutumika. Aidha, Wizara inaendelea kupitia mfumo huo na kufanya maboresho kwa kila hatua iliyokamilika ili kuwezesha utendaji mzuri wa mfumo huo.

85. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imetoa mafunzo kuhusu Sheria, Kanuni na Miongozo inayosimamia Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kupitia mikutano ya wadau na vyombo vya habari. Jumla ya wadau 970 wamefikiwa kati wadau 1,000 waliyopangwa kufikiwa kwa kipindi cha mwaka 2021/22 katika mikoa ya Arusha (150), Pwani (125), Songwe (50), Mbeya (50), Mtwara (50), Kinondoni (60), Morogoro (25), Geita (52), Shinyanga (70), Tanga (100), Mwanza (123) Tabora (65) na Simiyu (50). Lengo la mafunzo hayo ni kuyawezesha Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo ili kuchangia ipasavyo katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa Taifa.

Aidha, katika kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa Sera ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini, Sheria ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali imeanzisha Bodi ya uratibu wa Mashirika hayo. Kwa mwaka 2021/22, Bodi ya nne (4) imewezesha kufanyika kwa zoezi la uhakiki wa Mashirika Tanzania Bara lililoendeshwa kuanzia mwezi Machi 2021 hadi mwezi Machi 2022 na Mkutano wa mwaka wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali uliofanyika kwa mara ya kwanza Septemba, 2021. Vilevile, Bodi imewezesha na kuboresha mazingira ya uwajibikaji na utendaji kazi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ikiwemo ujenzi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali.

86. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha ushirikiano baina ya Tanzania Bara na Zanzibar juu ya Masuala ya Muungano na Yasiyo ya Muungano, Idara ilishiriki vikao viwili (2) vilivyofanyika tarehe 18 Novemba, 2021 na tarehe 10 Desemba, 2021 ikiwa ni sehemu ya kuimarisha mashirikiano baina ya Ofisi ya Msajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Tanzania Bara na Ofisi ya Mrajis wa Asasi za Kiraia Zanzibar. Kupitia vikao hivyo, uratibu na usimamizi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kwa pande zote mbili (2) za Muungano umeboreshwa hususan katika masuala ya usajili na kuweka utaratibu wa kutoa barua za utambulisho kwa Mashirika yanayotaka kufanya kazi upande wa Tanzania Bara au Zanzibar.

**ENEO LA 6: URATIBU WA UTEKELEZAJI WA MTAKUWWA**

87. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) kupitia maeneo nane (8) ya utekelezaji (*Thematic Areas*). Utekelezaji wa MTAKUWWA ulianza mwezi Julai, 2017 na utafikia ukomo mwezi Juni, 2022 na umekuwa ukitekelezwa kwa ushirikiano wa Wizara za Kisekta na Wadau mbalimbali. Baadhi ya mafanikio ya utekelezaji wa Mpango Kazi huu ni kama ifuatavyo: -

(i) Matukio ya ukatili wa kijinsia yaliyoripotiwa katika Dawati la Jinsia na Watoto la Polisi yamepungua kwa asilimia 31 kutoka matukio 42,414 mwaka 2020 hadi matukio 29,373 mwaka 2021 **(Kielelezo Na. 1)**. Aidha, matukio ya ukatili wa kijinsia kwa watoto yaliyoripotiwa kwenye Dawati hilo yamepungua kwa asilimia 28 kutoka matukio 15,870 mwaka 2020 hadi matukio 11,499 mwaka 2021 kama inavyoonesha katika **Kielelezo Na. 2**;

(ii) Jumla ya Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto **18,186** kati ya 20,750 (sawa na asilimia 88) zimeanzishwa katika ngazi ya Taifa, Mkoa, Halmashauri, Kata na Kijiji/Mtaa mwaka 2021/22 kutoka Kamati 16,343 zilizoanzishwa mwaka 2019/20 sawa na ongezeko la Kamati 1,843. Kamati hizi zinawezesha kubaini na kushughulikia vitendo vya ukatili nchini kuanzia ngazi ya Kijiji/Mtaa hadi Taifa. Serikali inaendelea kufanya ufuatiliaji ili kuziimarisha na kuziwezesha kutekeleza majukumu yao ipasavyo;

(iii) Hadi mwezi Februari 2022, Serikali kupitia OR-TAMISEMI imetoa mikopo yenye thamani ya **Shilingi Bilioni 35.55** kupitia asilimia 10 ya Mapato ya ndani ya Halmashauri. Kati ya fedha hizo, **Shilingi Bilioni 19.36** zimetolewa kwa vikundi vya wanawake wajasiriamali 2,881. Fedha hizo zimeendelea kuwawezesha wanawake kujiimarisha kiuchumi na kuboresha uchumi wa kaya;

(iv) Hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya Vituo 21 vya Mkono kwa Mkono (*One Stop Centers*) vimeanzishwa katika Hospitali mbalimbali za Serikali kwenye Mikoa 12 ikilinganishwa na Vituo 14 vilivyoanzishwa hadi kufikia mwaka 2020/21. Jumla ya manusura wa vitendo vya ukatili 1,857 walipatiwa huduma jumuishi ikiwemo huduma za kitabibu, polisi, msaada wa kisheria, ustawi wa jamii kupitia Vituo hivyo. Lengo ni kuwezesha utoaji wa huduma hizo katika eneo moja ili kuepusha usumbufu, ucheleweshaji wa huduma, kuharibu au kupoteza ushahidi. Serikali kwa kushirikiana na Wadau itaendelea kuratibu uanzishwaji wa Vituo vya Mkono kwa Mkono katika Mikoa ambayo haijaanzisha Vituo hivyo ikiwemo Mikoa ya Dodoma, Singida, Tanga, Geita, Katavi, Rukwa, Mtwara, Lindi, Ruvuma, Mara, Kagera, Njombe, Songwe na Manyara. Vituo hivi vinarahisisha huduma kwa kumpa fursa manusura kufika katika kituo na kupata huduma za unasihi, utoaji taarifa kwa Afisa wa Polisi na kupata matibabu. Aidha, vinarahisisha upatikanaji wa haraka wa ushahidi unaotokana na vipimo vya kitabibu unaowasilishwa katika Mahakama;

(v) Kuanzishwa kwa Nyumba Salama 10 katika mikoa ya Arusha (3), Iringa (1), Kigoma (1), Mara (2), Manyara (1), Morogoro (1) na Mwanza (1). Nyumba hizi zinatumika kutoa huduma za msingi na hifadhi ya dharura kwa manusura wa ukatili nchini. Kwa kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi mwezi Aprili 2022, jumla ya manusura 493 walihudumiwa kupitia Nyumba hizo. Serikali kwa kushirikiana na Wadau itaendelea kuratibu uanzishwaji wa Nyumba Salama katika maeneo mbalimbali kulingana na uhitaji wake. **Napenda kuishukuru Serikali ya Uingereza kupitia Taasisi ya *British Council* kwa kutupatia msaada wa majengo kwa ajili ya kuanzisha kitengo cha kupambana na usafirishaji haramu wa binadamu huduma ambayo uratibu wake utashirikisha sekta mbalimbali**;

(vi) Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma iliratibu kikao kilichowakutanisha wajumbe wa Kamati ya Ulinzi wa Wanawake na Watoto ngazi ya Mkoa ili kujadili utekelezaji wa MTAKUWWA, kukumbushana majukumu ya Kamati ngazi ya Mkoa na kuweka mikakati ya kutokomeza ukatili. Kikao hicho kilifanyika tarehe 15 Februari, 2022 ambapo kilihudhuriwa na washiriki 67. Aidha, Wizara iliratibu kikao cha Wadau wanaotekeleza afua mbalimbali za kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto kilichofanyika tarehe 26 Februari, 2022 Jijini Dodoma kwa lengo la kuweka Mkakati wa pamoja wa kukabiliana na vitendo vya ukatili katika jamii ambapo Wadau zaidi ya 200 waliweza kushiriki. Maazimio ya kikao hicho yalikuwa ni pamoja na: Kuimarisha Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto ngazi zote ili zitekeleze majukumu yao ipasavyo katika kutokomeza vitendo vya ukatili na kuwezesha upatikanaji wa taarifa na takwimu za matukio ya ukatili dhidi ya wanawake na watoto; Kuelimisha jamii kupitia majukwaa mbalimbali ikiwemo redio za kijamii, sanaa, vyombo vya habari na wadau ili kuijengea jamii uelewa wa masuala ya Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto; na kuwe na mabalozi wa MTAKUWWA; na (vii) Wizara iliwezesha kuzinduliwa kwa Kampeni ya "**Twende Pamoja, Ukatili Tanzania Sasa Basi**" katika Mkoa wa Mwanza lengo lilikuwa ni kuimarisha utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) ambapo hadi kufikia mwezi Aprili 2022, Kampeni hii ilitekelezwa katika mikoa mitano (5) ya Dar es Salaam, Mara, Mwanza, Katavi na Kigoma. Mikoa hii imefanikiwa kuzindua mpango wa Kampeni hii kati ya mikoa 12 iliyopangwa kufikia 2021. Kutofikiwa kwa idadi hii kulitokana na athari za UVIKO-19.

88. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na Takwimu za Jeshi la Polisi kuhusu Hali ya Uhalifu na Matukio ya Usalama Barabarani kuonesha kupungua kwa matukio ya ukatili yaliyoripotiwa mwaka 2021 ikilinganishwa na miaka iliyopita, bado tumeendelea kushuhudia matukio ya vitendo vya ukatili mara kwa mara kwenye vyombo vya habari hususan kupitia mitandao ya kijamii. Pamoja na hatua za kila siku za Serikali na wadau mbalimbali kupambana na ukatili kupitia MTAKUWWA, Wizara inaratibu utekelezaji wa kampeni kubwa ya kupambana na ukatili sambamba na kuimarisha mifumo ya kubaini viashiria vya ukatili na kuchukua hatua za kuzuia.

89. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuwa utekelezaji wa MTAKUWWA unafikia ukomo mwezi Juni 2022, Wizara imeanza mchakato wa kufanya tathmini ya Mpango huo kwa lengo la kubaini mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji kwa kipindi cha miaka mitano, changamoto na upungufu wa kimuundo na kiutendaji ulioathiri kufikiwa kwa malengo ya Mpango. Aidha, tathmini inatarajiwa kubainisha masuala ya kuigwa (*best practices*) na kutoa mapendekezo ya namna bora zaidi ya kukabiliana na changamoto na upungufu uliobainika. Matokeo au mapendekezo yatakayobainishwa katika taarifa ya Tathmini ya Mpango yatawezesha kuanza kwa maandalizi ya MTAKUWWA awamu ya pili itakayotoa mikakati mahsusi ya kutokomeza aina zote za ukatili dhidi ya wanawake na watoto kwa miaka mitano ijayo.

Katika hatua ya sasa, Wizara imesaini Mkataba na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) kutoa huduma ya Ushauri Elekezi katika zoezi la Tathmini ya MTAKUWWA sambamba na kuandaa MTAKUWWA II. Hatua za awali ikiwemo kukamilika kwa wasilisho la kwanza yaani "Inception Report" zimekwishafanyika na hivyo maandalizi kwa ajili ya zoezi la kukusanya na kuchakata taarifa kutoka kwa Wadau mbalimbali linaendelea. Tathmini na Maandalizi ya MTAKUWWA II yanatarajiwa kukamilika ifikapo mwezi Septemba, 2022.

**D. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA TAASISI ZILIZO CHINI YA WIZARA**

90. ***Mheshimiwa Spika,*** kama nilivyoeleza awali, Wizara imekuwa ikisimamia utekelezaji wa majukumu yake kupitia Taasisi zilizo chini yake ambazo ni Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Taasisi ya Ustawi wa Jamii.

91. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru imeendelea kutoa mafunzo ya taaluma ya maendeleo ya jamii katika ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada na Stashahada ya Uzamili. Pia, Taasisi imeendelea kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ili kuboresha shughuli za utoaji mafunzo. Katika mwaka 2021/22, Taasisi ilipanga kukusanya kiasi cha **Shilingi 3,560,574,000** kutoka vyanzo mbalimbali. Hadi mwezi Aprili 2022, Taasisi imefanikiwa kukusanya jumla ya Shilingi **2,669,377,825** sawa na asilimia **75** ya makadirio.

92. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha mwaka wa masomo 2021/22, Taasisi ilidahili wanafunzi 2,800 katika ngazi zote (Ke 1,857 na Me 943) ikilinganisha na wanafunzi 2,492 waliodahiliwa mwaka 2020/21. Aidha, kwa mwaka 2021/22, jumla ya wanafunzi 1,464 (Ke 1,006 na Me 458) walihitimu katika fani na ngazi mbalimbali ikilinganishwa na wanafunzi 1,003 (Me 262 na Ke 741) waliohitimu mwaka 2020/21.

93. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi iliandaa Kongamano kubwa la wanawake tarehe 7 Machi 2022 kuelekea kilele cha Siku ya Wanawake Duniani. Jumla ya washiriki 306 walihudhuria wakiwemo Mabalozi, Mashirika ya Kimataifa, Taasisi za Serikali, Maafisa kutoka Wizara mbalimbali, Wakurugenzi na Maafisa kutoka WMJJWM, Maafisa kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki na wawakilishi wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Aidha, Taasisi ilifanikiwa kuandika maandiko na kupata ufadhili wa kiasi cha **Shilingi Milioni 70** kutoka kwa wadau.

94. ***Mheshimiwa Spika***, Taasisi imeandaa programu sita mpya za kitaaluma ambapo programu moja ya kitaaluma ilibadilishana na Taasisi ya Mafunzo ya Serikali za Mitaa (LGTI) – Hombolo. Ushirikiano huu umeongeza idadi ya watumishi wa kitaaluma na wasaidizi wanaofadhiliwa na Taasisi kwa kozi ndefu na fupi. Hadi kufikia mwezi Desemba 2021, wafanyakazi 20 wameanza programu za PhD katika Vyuo Vikuu mbalimbali. Vilevile, wafanyakazi 11 wanaendelea na masomo ya shahada ya uzamili. Pia, watumishi watatu (3) wanahudhuria kozi ya Mhasibu wa Umma Aliyeidhinishwa (CPA) na





mmoja anahudhuria kozi ya taaluma ya ununuzi na ugavi. Ili kuongeza umahiri na maarifa ya wafanyakazi kitaaluma, mafunzo ya ndani kuhusu mbinu za utoaji na tafsiri ya mtaala yalifanyika kwa wiki moja Desemba 2021. Aidha, mafunzo kuhusu udhibiti wa msongo wa mawazo yalifanyika kwa wafanyakazi wote ili kuwa na wafanyakazi wenye afya bora wanaofanya kazi. chini ya udhibiti na udumishaji wa utamaduni thabiti, wenye afya mahali pa kazi ambao unafaa kwa ubunifu na tija.

95. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imeendelea kutekeleza programu ya kuchochea na kuendeleza ubunifu (*innovation*) miongoni mwa wanafunzi kupitia Kituo cha Huduma Tandaa na Ubunifu wa Kidijitali (*Jamii Outreach Digital Innovation Center – JODIC*). Kituo hiki kinatumika kuratibu utekelezaji wa programu za ubunifu wa kidijitali, ushirikishaji jamii na uanagenzi katika kazi pana za Taasisi. Kupitia kituo hicho, Taasisi imetekeleza kazi zifuatazo: -

(i) Taasisi iliandaa Wiki ya Maendeleo ya Jamii kuanzia tarehe 6-11 Desemba 2021. Katika maadhimisho hayo, maonesho yaliandaliwa katika viwanja vya TICD ambapo wadau wakuu walishiriki na kuonesha bidhaa na huduma zao. Pia, vikundi mbalimbali vya wanafunzi wa Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru walionesha bidhaa zao. Maonesho hayo yaliongeza mwonekano wa bidhaa zao, pia kujenga mitandao/muunganisho na kuboresha ujuzi wa masoko, uuzaji na uwekaji chapa kwa wanafunzi;

(ii) Kuhamasisha na kutoa mafunzo kwa vikundi 17 vya wanawake, vijana na walemavu kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Arusha kuhusu stadi za ujasiriamali;

(iii) Kuanzisha ushirikiano na Kampuni ya Gongali *Model* ambapo Kituo kiliwasilisha andiko la kufadhili shughuli za Kituo (JODIC);

(iv) Kuendesha mafunzo kuhusu uundaji wa vikundi, taratibu za usajili, fursa za mikopo, uuzaji wa kidijitali, unyanyasaji wa kijinsia na ulinzi wa haki za binadamu kwa wanafunzi 49 na viongozi wa vikundi vya kijamii;

(v) Kuadhimisha siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia ambapo shughuli mbalimbali zilifanyika ikiwemo mijadala kuhusu migogoro ya kifamilia inavyochangia unyanyasaji wa kijinsia miongoni mwa wanandoa. Mojawapo ya mambo muhimu yaliyochukuliwa kutoka kwenye mazungumzo hayo ni kutambua kuwa wanaume pia ni waathiriwa wa unyanyasaji wa kijinsia. Aidha, mafunzo kuhusu unyanyasaji wa kijinsia yaliendeshwa kwa wanawake 500 kutoka Kata za Akheri, Kikwe na Kiutu Wilayani Arumeru. Pia, ilifanyika kampeni ya uhamasishaji juu ya mambo yanayoendeleza unyanyasaji wa kijinsia na hatua za kukabiliana nayo kwa wanafunzi 200 na 300 wa shule za msingi na sekondari mtawalia; na

(vi) Kutoa mafunzo kwa wanafunzi 289 na wafanyakazi wa taaluma 53 kuhusu uanagenzi na stadi za kuajiriwa kwa ajili ya utekelezaji bora wa programu ya uanagenzi. Aidha, Kituo (JODIC) kilifanya uchanganuzi wa upungufu wa ujuzi kwa wanafunzi 289 ili kubaini maeneo yanayofaa kwa programu ya uanagenzi. Vilevile, Kituo kiliendesha zoezi la ufuatiliaji na tathmini kwa wanagenzi 274 waliokuwa waandaaji katika mashirika mbalimbali nchini Tanzania.

96. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii ambayo nayo ipo chini ya Wizara ninayoiongoza ni kwamba Taasisi hii imeendelea kutoa mafunzo katika ngazi ya Astashahada, Stashahada, Shahada, Stashahada ya Uzamili na Shahada ya Uzamili katika fani ya Ustawi wa Jamii na fani nyinginezo zinazoshabihiana nayo. Aidha, Taasisi imeendelea kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato kutoka kwenye vyanzo vikubwa vya mapato ambavyo ni; ada za wanafunzi, tafiti, ushauri elekezi na vyanzo vingine. Katika mwaka 2021/22, Taasisi ilipanga kukusanya kiasi cha **Shilingi 6,356,968,500.** Hadi kufikia mwezi Aprili 2022, Taasisi imekusanya **Shilingi 4,877,734,052** sawa na asilimia 77 ya makadirio.

97. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa masomo 2021/22, Taasisi imedahili wanafunzi 3,234 (Ke 2,104 na Me 1,130) ikilinganishwa na wanafunzi 2,542 (Ke 1,680 na Me 862) waliodahiliwa mwaka 2020/21 sawa na ongezeko la asilimia 27. Kati ya wanafunzi waliodahiliwa mwaka 2021/22, wanafunzi 879 walidahiliwa katika ngazi za Astashahada, wanafunzi 674 ngazi ya Stashahada, wanafunzi 1,586 ngazi ya Shahada na wanafunzi 95 ngazi ya Shahada ya Uzamili. Aidha, katika mwaka 2020/21, Taasisi iliwezesha wanafunzi 2,493 (Ke 1,645 na Me 848) kuhitimu katika fani na ngazi mbalimbali ikilinganishwa na wanafunzi 1,246 (Ke 928 na Me 318) waliohitimu mwaka 2019/20. Kati yao, wanafunzi 938 walihitimu katika ngazi ya Astashahada, wanafunzi 687 ngazi ya Stashahada, wanafunzi 692 ngazi ya Shahada na wanafunzi 176 walihitimu katika ngazi ya Shahada ya Uzamili.

98. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Ustawi wa Jamii imeendelea kutoa huduma ya msaada wa kisaikolojia kwa wanafunzi na jamii kupitia Kituo chake cha Elimu, Ushauri na Msaada wa Kisaikolojia kilichokarabatiwa kwa ufadhili wa Shirika la *Korea International Cooperation Agency* (KOICA). Taasisi ilitoa huduma za kisaikolojia na ushauri kwa manusura 345 wa janga la moto katika Soko la Karume ikiwemo watu wenye mahitaji maalum 150. Kupitia Kituo hiki Taasisi pia imeweza kutembelea shule nne (4) za Wilaya ya Kinondoni na shule moja (1) katika Wilaya ya Mwanga ili kuelimisha wanafunzi kuhusiana na nidhamu, ufaulu na mahusiano. Vilevile, elimu ilitolewa juu ya viashiria vya ukatili wa kijinsia, stadi za kuepukana na makundi mabaya na matumizi ya dawa za kulevya. Kupitia afua hizo, Taasisi iliweza kuwafikia jumla ya wanafunzi 853 na kutoa huduma za ushauri, unasihi na kisaikolojia kwa wanajamii 1,034 wanaoizunguka Taasisi. Yote haya yamelenga katika kuhakikisha malezi na makuzi yanaimarishwa ili kukuza ustawi wa mtu mmoja mmoja, familia na Taifa kwa ujumla.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Ustawi wa Jamii pia imekuwa ikiendesha programu za kushirikisha jamii (*community engagement*), uanagenzi (*apprenticeship*) na ubunifu (*innovation*). Kupitia kituo chake cha ubunifu, Taasisi imeweza kuwajengea ujuzi na uwezo wanafunzi 180 katika muda wa wiki nane (8) ili waweze kutumia teknolojia ya kidijitali kama nyenzo ya kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Kupitia programu yake ya uanagenzi, Taasisi imeweza kuwaunganisha wanafunzi 11 kupata ajira na kuwezesha wanafunzi wengine 56 kupata nafasi mbalimbali za kujifunza stadi za kazi katika mashirika mbalimbali kwa kipindi cha mwaka 2021/22. Pia, Taasisi kupitia porgramu yake ya kushirikisha jamii imewapatia vijana 428 wa Manispaa ya Kinondoni elimu na ushauri juu ya namna ya kukabiliana na changamoto za maisha, afya, mahusiano na namna ya kujikwamua na umaskini.

100. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi ya Ustawi wa Jamii iliadhimisha Siku ya Kimataifa ya Ustawi wa Jamii duniani tarehe 15/3/2022 kwa kutoa huduma za ustawi wa jamii bure kwa wananchi. Huduma zilizotolewa ni pamoja na; ushauri wa masuala ya ndoa na mahusiano, masuala ya watoto waliotelekezwa na ushauri wa kisaikolojia. Vilevile, Taasisi iliadhimisha siku hiyo kwa kufanya vipindi vya luninga kuelimisha jamii juu ya Ustawi wa Jamii na wataalam wa ustawi wa jamii wanavyoweza kusaidia kupunguza changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika jamii.

101. ***Mheshimiwa Spika,*** Taasisi imeendelea kufanya tafiti zinazohusu changamoto mbalimbali za kijamii ikiwemo utafiti kuhusu utumiaji wa taasisi za kimila na kijamii kukabiliana na ukatili wa kijinsia na jinsi ya kuondoa unyanyasaji wa kijinsia katika Taasisi za Elimu ya Juu. Aidha, Taasisi imejielekeza katika kuimarisha elimu ya malezi na makuzi ya watoto kwa kutoa kozi za awali za makuzi kwa walezi wanaolea watoto katika vituo vya SOS vya Arusha, Dar es Salaam na Mwanza. Katika kutambua umuhimu wa elimu ya awali ya malezi na makuzi, Taasisi imeanza maandalizi wa Mtaala wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Watoto (*Early Childhood Care and Development*) ambao utatumika kuwajengea uwezo na uelewa walezi hususan walio katika vituo vya kulelea watoto.

102. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 Ibara ya 80, Taasisi imefanya maboresho mbalimbali katika miundombinu yake ya kujifunzia na kufundishia kama ifuatavyo: -

(i) Taasisi imeendelea kutekeleza mradi wa kujenga maktaba ya kisasa hatua ya nane (phase VIII) na ya mwisho ambapo kazi zilizofanyika ni pamoja na kufunga mfumo wa mawasiliano ya TEHAMA, mfumo wa umeme, kuweka mfumo wa mabomba ya maji, kufunga kiinua (*lift*), ujenzi wa kuta za ndani na kupaka rangi;

(ii) Katika kuimarisha matumizi ya TEHAMA, Taasisi imenunua vifaa mbalimbali pamoja na kujiunga na mtandao wa Serikali (Government Network). Pia, Taasisi imefunga seva ya kompyuta yenye uwezo wa kuruhusu hadi wanafunzi 10,000 kutumia mifumo ya TEHAMA iliyopo kwa wakati mmoja na kuongeza wigo wa upatikanaji wa mtandao (*Internet Band- Width*) kutoka 12MbPs hadi kufikia 22MbPs; na

(iii) Taasisi imekamilisha ujenzi wa madarasa mawili (2) pamoja na ofisi mbili za wafanyakazi katika Kampasi yake ya Kisangara iliyopo Mwanga Kilimanjaro. Madarasa hayo yana uwezo wa kuhudumia wanafunzi 500 kwa wakati mmoja na Ofisi hizo zina uwezo wa kuhudumia watumishi sita (6).

103. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha utendaji kazi na kutoa elimu yenye tija itakayoweza kukuza Ustawi wa Jamii nchini, Taasisi imewafadhili watumishi 32 wanaoendelea na masomo yao katika Shahada ya Uzamivu (PhD), Watumishi sita (6) katika Shahada ya Uzamili (*Master's*) na watumishi 48 katika mafunzo ya muda mfupi (*Short Courses*).

**F. UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO**

104. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi, Wizara imeendelea kutekeleza afua mbalimbali za miradi ya maendeleo ikiwemo ujenzi na ukarabati wa majengo na miundombinu katika Taasisi na Vyuo vilivyo chini yake. Kwa kipindi cha mwezi Julai 2021 hadi mwezi Aprili 2022, Wizara iliweza kupokea kiasi chote cha fedha za ndani za maendeleo kiasi cha **Shilingi Bilioni 4.9** kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii na Mradi wa Huduma za Ustawi wa Jamii. Kati ya fedha za ndani zilizopokelewa, **Shilingi Bilioni 3.6** ni kwa ajili ya Mradi wa Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii ambapo fedha hizo zimeanza kutumika kwa ajili ya kujenga mabweni mawili, maktaba na ukumbi wa mihadhara katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Ruaha, kujenga bweni lenye ghorofa mbili katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Rungemba na kujenga bweni lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 600 katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Uyole. Aidha, fedha hizo zimeanza kutumika kwa ajili ya ujenzi wa jengo la utawala na darasa moja katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Mlale, kukarabati kumbi mbili za mihadhara (zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500 kila ukumbi kwa wakati mmoja) pamoja na kujenga ukumbi wa mihadhara (wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 450 kwa wakati mmoja) katika Chuo cha Maendeleo ya Jamii Monduli. Ujenzi wa miradi hiyo umeanza na upo katika hatua za awali za utekelezaji.

Aidha, kiasi cha **Shilingi Bilioni 1.3** kimeelekezwa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo na miundombinu katika Taasisi na Vituo vya Ustawi wa Jamii ikiwemo: ujenzi na ukarabati wa majengo na miundombinu katika Shule ya Maadilisho Irambo, Mahabusu za Watoto za Mbeya, Tanga na Arusha; na ujenzi wa hosteli ya wanafunzi katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii (Kampasi ya Kisangara) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 400 kwa wakati mmoja. Ujenzi na ukarabati katika Taasisi na Vituo hivyo unaendelea.

105. ***Mheshimiwa Spika,*** hata hivyo, katika kuunga mkono juhudi za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Wizara kupitia Vyuo vya Maendeleo ya Jamii inaandaa miradi ya maendeleo ambapo kupitia miradi hiyo ifikapo mwaka 2024/25 inatarajia kukusanya kiasi cha **Shilingi Bilioni 2.1**. Aidha, kiasi hicho cha fedha kitaweza kupunguza kwa kiasi kikubwa utegemezi wa Vyuo hivyo kwa Serikali katika uendeshaji wake. Mchanganuo wa miradi hiyo na makadirio ya makusanyo umeoneshwa katika **Kiambatisho Na. 3.**

**G. VIPAUMBELE VYA WIZARA NA BAJETI YA MAPATO, MATUMIZI YA KAWAIDA NA MIRADI YA 2022/23 MAENDELEO KWA MWAKA**

106. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Wizara kupitia Idara na Taasisi zilizo chini yake itatekeleza vipaumbele nane (8) ili kuboresha utoaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii: -

(i) Kuratibu afua za kukuza usawa wa kijinsia, uwezeshaji wanawake kiuchumi na kiuongozi na kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake, watoto na wazee;

(ii) Kukuza ari ya jamii kushiriki katika kupanga na kutekeleza miradi ya maendeleo iliyoibuliwa ngazi ya jamii;

(iii) Kutambua na kuratibu makundi maalum wakiwemo wafanyabiashara ndogondogo (Machinga) ili kuboresha mazingira ya biashara zao;

(iv) Kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru na Vyuo vya Maendeleo ya Jamii; (v) Kuratibu utoaji wa huduma za msingi kwa watu wenye mahitaji maalum, huduma za usuluhishi wa migogoro ya ndoa na familia na huduma ya msaada wa kisaikolojia kwa manusura wa majanga mbalimbali na makundi mengine yenye uhitaji katika jamii;

(vi) Kuratibu na kuwezesha upatikanaji wa huduma za ustawi wa jamii kwa wazee;

(vii) Kuratibu na kusimamia afua za upatikanaji wa haki za mtoto, ulinzi na malezi chanya ya watoto; na

(viii) Kuimarisha ushiriki na mchango wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali katika maendeleo ya Taifa.

107. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kutekeleza vipaumbele vilivyoainishwa hapo juu, Wizara kwa mwaka 2022/23 imekadiria kutumia kiasi cha **Shilingi Bilioni 43.4** zitakazotumika kutekeleza majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na kuwezesha uendeshaji wa ofisi na utekelezaji wa miradi wa maendeleo. Baadhi ya maeneo yaliyotengewa fedha kwa mwaka 2022/23 ni pamoja na: -

(i) Katika eneo la ukatili na masuala ya usawa wa kijinsia, kiasi cha **Shilingi Bilioni 2.65** kimetengwa kwa ajili ya kuratibu utekelezaji wa afua za kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto ikiwemo Kampeni ya "**Twende Pamoja, Ukatili Tanzania Sasa Basi**". Pia, fedha hizo zitatumika kwa ajili ya kusambaza Mwongozo wa Majukwaa ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi, kuwezesha utekelezaji wa Ahadi za Nchi kuhusu Jukwaa la Kizazi Chenye Usawa na kuwezesha ushiriki wa wanawake katika Maonesho ya Kitaifa na Kimataifa;

(ii) Kwenye eneo la watoto, kiasi cha **Shilingi Bilioni 2.36** kimetengwa kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa huduma kwa watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi na marekebisho ya tabia kwa watoto waliokinzana na sheria, kukarabati Mahabusu za Watoto katika Mikoa ya Mbeya na Arusha, kujenga Mahabusu ya Watoto mpya katika Mkoa wa Mwanza, kuratibu utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Mtoto (2021/22 – 2025/26) na kuanzisha vituo vya kijamii vya malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto;

(iii) Katika eneo la wazee, **Shilingi Bilioni 1.45** zimetengwa kwa ajili ya kuwezesha utoaji wa huduma za ustawi kwa wazee wasiojiweza katika Makazi ya Wazee 14 na ukarabati wa majengo na miundombinu katika Makazi ya Wazee ya Ipuli na Njoro;

(iv) Kwenye eneo la Taasisi na Vyuo, kiasi cha **Shilingi Bilioni 5.6** kimetengwa. Fedha hizo ni kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo na miundombinu katika Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, Taasisi ya Ustawi wa Jamii (Kampasi ya Kisangara) na Vyuo nane (8) vya Maendeleo ya Jamii;

(v) Eneo la uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali limetengewa kiasi cha **Shilingi Milioni 642.3** kwa ajili ya ufuatiliaji wa Mashirika 1,000 katika Kanda tano (5), kuendesha Mfumo wa Kielekroniki wa Usajili wa Mashirika, kuwezesha vikao vya Bodi ya Uratibu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, kusajili Mashirika na kuratibu Jukwaa la Mashirika Yasiyo ya Kiserikali;

(vi) Eneo la maendeleo ya jamii limetengewa kiasi cha **Shilingi Milioni 160.2** kwa ajili ya kutekeleza Kampeni ya Kitaifa ya Kuamsha Ari ya Jamii kuhusu ujenzi wa nyumba bora za gharama nafuu kwa kutumia teknolojia rahisi katika mikoa 26 ya Tanzania Bara; na

(vii) Katika eneo la ufuatiliaji na tathmini, kiasi cha **Shilingi Milioni 200** kimetengwa. Fedha hizo ni kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa mipango, programu na miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika Taasisi, Vyuo na Vituo vya Ustawi vilivyo chini ya Wizara.

**H. SHUKRANI**

108. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imekuwa ikipata ushirikiano mkubwa kutoka nchi rafiki, Mashirika ya Kimataifa na Sekta mbalimbali zinazosaidia na kuchangia katika huduma za maendeleo na ustawi wa jamii.

109. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kuchukua nafasi hii ya kipekee kuzishukuru Serikali za nchi za Marekani, Ujerumani, Ubelgiji, Ufaransa na nchi nyingine ambazo zimeendelea kuisaidia Wizara kwa njia mbalimbali. Aidha, naishukuru Serikali ya Uingereza kupitia Shirika la Misaada la FCDO ambalo limefadhili kazi ya kupokea maoni ya wadau katika maandalizi ya Mkakati wa Kitaifa wa Uendelevu wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali nchini. 110. ***Mheshimiwa Spika,*** nayashukuru pia Mashirika ya Kimataifa kwa ushirikiano wao waliotoa kwa Wizara. Mashirika hayo ni pamoja na: Mashirika yaliyo chini ya Umoja wa Mataifa (UNICEF, UN-Women, UNFPA, WHO, IOM na UNESCO); Umoja wa Nchi za Ulaya (EU); Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB); USAID; Abbott Fund; na Global Fund (for HIV, TB na Malaria). Aidha, nazishukuru Taasisi za Kifedha zinazoshirikiana na Wizara ambazo ni pamoja na NMB, CRDB, Stanbic Bank na Benki ya Biashara Tanzania (TCB).

111. ***Mheshimiwa Spika,*** nayashukuru Mashirika Yasiyo ya Kiserikali ya ndani ya nchi na Mashirika ya Dini kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Mashirika hayo ni pamoja na; WiLDAF, TCRF, TAMWA, TAWLA, TGNP, TAYOA, LSF, Plan International - Tanzania, Kivulini, FSDT, The Aga Khan Foundation, CBM International, Segal Foundation, HelpAge International, Save the Children, World Vision, PACT Tanzania, TradeMark East Africa (TMEA), Equality for Growth (EfG), Landesa, TAWIA, CAMFED, SOS Children's Village Tanzania, C- SEMA; Railway Children Africa, REPPSI, Amani Girls Home, Pelum Tanzania, LHRC, ECPAT, INTERPOL, Haki Elimu, SOS Children Tanzania, TWCC, Compassion International, Care International Tanzania, TECDEN, Pact Tanzania, BAKWATA na CCT.

112. ***Mheshimiwa Spika,*** nazishukuru Taasisi mbalimbali za Serikali zikiwemo SIDO, BRELA, NIMR, TBS, Shirika la Posta Tanzania, NSSF, TFS, TASAC, TPA, NHIF, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF), TASAF, Jeshi la Polisi Tanzania, Jeshi la Magereza Tanzania Bara na TAKUKURU kwa kuendelea kushirikiana na Wizara yangu. Pia, navishukuru Vyuo vilivyo chini ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kuwa mstari wa mbele katika kuchangia uimarishaji wa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii. Aidha, nawashukuru wadau wengine waliotoa huduma ya elimu kwa njia za redio, luninga, magazeti na mitandao ya kijamii kuhusu masuala ya maendeleo na ustawi wa jamii. Wadau hao ni pamoja na; Joyce Kiria (kupitia kipindi cha Wanawake *Live*), Mhe. Vicky Kamata (kupitia kipindi cha Wanawake na Maendeleo) na wadau wengine. Vilevile, navishukuru Vyama mbalimbali vya kitaaluma ikiwemo; CODEPATA, TASWO na Tanzania Bankers Association. 113. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha utekelezaji wa majukumu yangu nikiwa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, nimepata ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi na wafanyakazi wa Wizara. Napenda kumshukuru **Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis (Mb)**, Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa ushirikiano anaonipa katika kutekeleza majukumu yangu. Pia, naomba kuwashukuru **Dkt. Zainab Abdi Seraphin Chaula,** Katibu Mkuu na **Bw. Amon Anastaz Mpanju**, Naibu Katibu kwa mchango na ushirikiano wao katika kuwezesha utekelezaji wa majukumu yangu. Aidha, nawashukuru Makamishna, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Wataalam wote wa Wizara kwa utendaji wao mzuri uliowezesha kukamilisha maandalizi ya Hotuba yangu kwa wakati muafaka. Vilevile, kupitia OR-TAMISEMI nawashukuru sana Wakuu wa Mikoa yote, Makatibu Tawala, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri zote na wataalam wote chini ya ofisi zao na pia wadau wote wa sekta mbalimbali wanaohudumia katika maeneo yao.

114. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee naomba kuwashukuru Wakuu wa Taasisi ya Ustawi wa Jamii na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru. Pia, nawashukuru Wakuu wa Vyuo nane (8) vya Maendeleo ya Jamii kwa ushirikiano wao mzuri unaonirahisishia utekelezaji wa majukumu yangu. Natoa shukrani kwa sekta zote ambazo tunashirikiana nazo katika kutoa huduma za maendeleo na ustawi wa jamii pamoja na wananchi wote kwa ushirikiano wao. Nawaasa waendelee kuzingatia misingi ya huduma bora na kufanya kazi kwa bidii kwa manufaa ya Taifa letu. Aidha, naishukuru Kamati ya Ushauri ya Kitaifa ya Utekelezaji wa Ahadi za Nchi kuhusu Kizazi Chenye Usawa (*Generation Equality Forum - GEF*) chini ya uongozi mahiri wa **Mheshimiwa Anjellah Kairuki** ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo.

115. ***Mheshimiwa Spika,*** nichukue fursa hii pia kuishukuru familia yangu, hususan mume wangu **Advocate Metusela Gwajima** na watoto wetu pamoja na wote ambao wamekuwa sehemu ya familia yetu kwa uvumilivu wao na kipekee kwa kunitia moyo katika kutekeleza majukumu yangu ya Kitaifa. Aidha, nawashukuru wananchi wote wa Tanzania kwa kuipatia ushirikiano Wizara ninayoisimamia wakati wote wa kutekeleza majukumu yangu na pia kwa wao binafsi kuendelea kupambana kuhakikisha maendeleo na ustawi wa jamii kwa usawa wa jinsia huku wakitumia **Simu Namba 116** bila malipo kwa ajili ya kuripoti matukio au viashiria vya ukatili saa 24 kila siku. Aidha, nawahimiza kuendelea kutumia simu zote za wataalam waliopo Wizarani na katika Mikoa na Halmashauri nchi nzima pamoja na namba yangu **0734124191** kwa ajili ya kutoa taarifa za viashiria vya ukatili kama tulivyotangaza kwenye vyombo vya habari na kuziweka kwenye tovuti yetu ya Wizara ambayo ni ***www.jamii.go.tz***.

**I. MAOMBI YA FEDHA KWA KAZI ZILIZOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA 2022/23**

**Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli kwa Mwaka 2022/23**

116. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Wizara imekadiria kukusanya **Shilingi 8,500,000,000** kutokana na ada na tozo mbalimbali za usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali, mapato ya ada za mitihani na uuzaji wa mitaala ya Mafunzo ya Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii na mapato mengine.

**Matumizi ya Kawaida**

117. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2022/23, Wizara inakadiria kutumia kiasi cha **Shilingi 32,310,981,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 18,169,057,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 14,141,924,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi.

**Miradi ya Maendeleo**

118. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa upande wa shughuli za maendeleo, Wizara inakadiria kutumia **Shilingi 11,092,080,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 6,900,000,000** ni Fedha za Ndani na **Shilingi 4,192,080,000** ni Fedha za Nje.

119. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa mwaka 2022/23, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (Fungu 53) inaomba jumla ya **Shilingi 43,403,061,000** ili kutekeleza majukumu yake kwa maendeleo na ustawi wa jamii.

120. ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii inapatikana pia katika tovuti ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum *www.jamii.go.tz.*

121. ***Mheshimiwa Spika,*** naomba kutoa hoja





# Waziri ataja madhara lishe duni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Kilimo, Umwagiliaji Maji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shaame Khamis, amesema miongoni mwa maradhi yanayotokana na lishe duni ni udumavu wa watoto, uzito pungufu na upungufu wa damu kwa wajawazito na wanaonyonyesha.

Aliyasema hayo katika uzinduzi wa kampeni ya kitaifa ya lishe bora ni mtaji uliofanyika katika viwanja vya bustani ya Forodhani Mjini Unguja ambao umeandaliwa na Umoja wa Ulaya pamoja na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) ili kupambana na utapiamlo.

Alisema kumekuwa na ongezeko kubwa la uzito wa kupindukia kwa wananchi na kusababisha kuongezeka kwa maradhi yasioambukiza ikiwamo shinikizo la damu na kisukari.

Alisema ripoti ya utafiti ya afya ya uzazi na mtoto ya (DHS) mwaka 2015/2016 na ya utafiti wa lishe nchini (NNS) ya mwaka 2018 inaonyesha kuwa udumavu umepungua kidogo kutoka asilimia 23 mwaka 2015 hadi asilimia 21.5 mwaka 2018.

"Hali ya uzito kupungua imeongezeka kutoka asilimia 13.8 hadi asilimia 14 mwaka 2018," alisema waziri huyo.

Alisema hali hiyo imetokana na kubadilika kwa tabia za ulaji kwa kula mlo usio kamili na vyakula visivyo na siha na kuwa juhudi kubwa zinahitajika kupunguza kwa kasi hali hiyo na lishe ni suala la kushirikiana kwa pamoja ili kupunguza matatizo hayo. Alieleza kuwa njia moja kubwa ni kuboresha ulaji na kufanya mazoezi ili kuepukana na maradhi yasiyoambukiza.

Naye Mkuu wa Umoja wa Ulaya, Cedric Merel, alisema kilimo sio fursa za kiuchumi pekee bali pia huboresha afya za watu na mpango huo uliozunduliwa unalenga kufanya mfumo wa chakula Tanzania kustahimili changamoto na kuongeza uelewa wa watu kuhusu wa karibu kati ya kinacholimwa, na kinacholiwa.

Alisema kampeni hiyo itajumuisha shughuli mbalimbali ikiwamo programu za mapishi, ziara za elimu ya lishe katika dadala, mafunzo kwa vijana wa kike na kuanzishwa kwa maeneo ya msosi asilia, kampeni hiyo inatarajiwa kuwafikia wananchi milioni 32 kwa muda wa kipindi cha miaka miwili.

Mwakilishi wa FAO Tanzania, Dk. Nyabenyi Tipo, alisema wakati janga la dunia likiendelea kuna haja ya kuwa na umuhimu wa mlo bora katika kukabili madhara.

"Mabadiliko katika tabia za jamii kuhusiana na uzalishaji wa chakula, ulaji na ufikiwaji wa masoko utaongeza upatikanaji wa chakula, kuimarisha kinga ya mwili na kuwapa wakulima wadogo kipato," alisema.

Alisema kampeni hiyo ya lishe bora ni mtaji italeta manufaa ya kiafya, kijamii na kiuchumi katika kukabiliana na utapiamlo kuanzia mtoto akiwa tumboni hasa katika siku 100 za kwanza.

Kwa upande wake Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Hamza Hassan Juma, akimwakilisha Waziri wa Afya Zanzibar, alisema wananchi wa vijijini ndiyo wanaongoza kwa tatizo la utapiamlo licha ya chakula kingi kinalimwa vijijini.

## Serikali kuwapatia wavuvi boti kwa mkopo nafuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Masoud Suleiman, amesema serikali ina mpango wa kuwapatia wavuvi boti za uvuvi kwa ajili ya mkopo wa masharti nafuu kupitia fedha za ahuweni za UVIKO-19.

Aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la mwakilishi wa Jimbo la Pandani, Prof. Omar Fakihi.

Alisema taratibu za ununuzi zimeshakamilishwa na boti hizo tayari zinatengenezwa na zitakabidhiwa wizarani kwake.

Alisema baadaye boti hizo watapatiwa wananchi kupitia utaratibu uliowekwa na serikali na kuwawezesha wajasiriamali katika vikundi vyao vilivyosajiliwa na kutambulika kukidhi masharti ya mkopo huo nafuu.

Alisema utaratibu unaotakiwa kufuatwa na wavuvi kupata boti ni wavuvi kujikusanya katika vikundi rasmi, kupata usajili na kuhakikiwa.

Alisema mkopo utaidhinishwa taratibu zote za uhakika wa vikundi hivyo kwa mujibu wa hatua za kibenki zitakapokamilika na kutolewa kwa vikundi vitakavyokidhi masharti nafuu.

Alisema boti zitakazotolewa ni 500 kwa wakulima wa mwani na 577 kwa wavuvi wadogo.



Washiriki wa mkutano mtandao wa Mpango Jumuishi wa Maendeleo katika Jamii (CBID) uliofanyika ukumbi wa Makonyo Wawi Chakechake wakiwa katika mkutano huo, ambao umeandaliwa na MECP-Z kwa ufadhili wa Shirika la Watu Wenye Ulemavu la Norway (NAD). **PICHA: MWANDISHI WETU**

## Wizara Afya yakabiliwa uhaba wafanyakazi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar, imesema inakabiliwa na changamoto ya uhaba wa wafanyakazi katika ngazi zote.

Hayo yalisemwa na Naibu Waziri wa wizara hiyo, Hassan Khamis Hafidh, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Tumbe, Said Saleh, aliyetaka kujua wizara itafungua kituo cha afya lini jimboni kwake Tumbe ili kuwapunguzia wananchi usumbufu.

Alisema, kutokana na uhaba huo wa wafanyakazi hasa wa kada ya wauguzi, wizara kwa sasa imeshindwa kukifungua kituo hicho cha afya Tumbe.

Alisema wizara yake imeshawasilisha mahitaji yake ya wafanyakazi wa kada za afya ikiwamo wauguzi na maofisa tabibu na kwa sasa wanasubiri kibali kutoka utumishi wa umma.

"Kituo cha afya Tumbe kitafunguliwa pindi watakapopatikana wafanyakazi," alisema.

Alikiri kuwa vituo vingi vya afya vinakabiliwa na ukosefu wa dawa ikiwamo kituo cha afya Tumbe, hali hiyo ilichangiwa na ukosefu wa fedha kwa ajili ya kununua dawa muhimu kwa ajili ya vituo vya afya Unguja na Pemba.

"Nawaomba wananchi kuwa wastahimilivu karibu wizara itasambaza dawa zote muhimu katika vituo vya afya," alisema.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## AMEPOTEA



Ndugu **MIKAELY JEMSY TWEVE** kabila la **MKINGA dini MKRISTO** mwenye umri wa miaka 21, aliekuwa akiishi **KIMARA (STOP OVER)** ametoweka pasipo kujulikana tarehe **22/05/2022** siku ya **JUMAPILI mida ya ALASIRI saa tisa(9)** mchana,muonekano ni mweusi, mrefu kiasi,maeneo anayopenda kutembelea ni mbezi mwisho ya kimara,yeyote atakayemuona atoe taarifa kituo chochote cha polisi AU piga simu namba **0713 421 144-SILVESTER MGONJA**-baba mlezi

**Polisi taarifa KIM/RB/2175/2022**

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**ESTER JOSEPH MWAKYOMA** anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **TAE 180965** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe **02/9/2019.** Muda wake wa kuisha matumizi ni tarehe **01/9/2029.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu naye. **Taarifa ya Polisi: DSM/PHQ/RB/212480/2022.**

**TEGEMEZA FINANCE COMPANY & COURT BROKER**

## MNADA, MNADA, MNADA

Kwa mamlaka tuliyopewa na mahakama kuu kitengo cha kazi tunawajulisha tutakuwa na mnada.

**AINA YA MALI TAREHE MAHALI**
Gari T568 DLV TOYOTA IST 1/6/2022 Mbezi Beach Tangi Bovu D.S.M , saa 4:00 asubuhi T625 DQK TOYOTA IST 1/7/2022 mbezi beach Tangi bovu, DSM , saa 4:00 asubuhi

Mali itakayouzwa
Kesi namba 614/2020
Mdai:........................ Zuhura Idriss
Dhidi ya
Wadaiwa :........................ Azure Oneh Limited
Rehema Fedrick Fussy

| AINA YA MALI | TAREHE | MAHALI |
|---|---|---|
| Gari T568 DLV TOYOTA IST | | Mbezi Beach Tangi Bovu D.S.M , saa 4:00 asubuhi |
| T625 DQK TOYOTA IST | 1/7/2022 | mbezi beach Tangi bovu, DSM , saa 4:00 asubuhi |

**MASHARTI YA MNADA**

Mali iliyouzwa italipiwa 25% baada siku 14 atamalizia 75% asipomalizia haitarudishwa pesa aliyolipa awali.
Mali inauzwa kama ilivyo, kwa mawasiliano tel:**0719-187677**

KIBAIGWA AUCTION MART & CO. LTD
COURT BROKER

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

TUTAFANYA MNADA TAREHE 16/06/2022 SAA NNE ASUBUHI WA KUUZA ENEO LA KIWANJA LILILOPO MBWANGA MALI YA KEVIN ERICK BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO ALIYOKOPA UHUMA FINANCIAL SERVICES P.BOX 1111058 - DODOMA. MNADA UTAFANYIKA MAHALI KIWANJA KILIPO, HIVYO TUNAPENDA KUWATANGAZIA WAHITAJI WOTE.

**KWA MAWASILIANAO PIGA NO. 0688729841 au 0657222838**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**GODFREY EMANUEL MALLYA** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA GARI AINA YA NOAH YENYE NAMBA ZA USAJILI **T330 DDP**. KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA POLISI.

**POLISI TAARIFA: ARU/ARU/RB/210698/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA, KAGERA LILILOPO BUKOBA**

**MAOMBI NA. 14/2022**

**LENA JOEL RWEHABURA ........................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**NMB PLC NA WENZAKE..................WAJIBU MAOMBI**

**KWA: JUSTUS NDIBALEMA**

**ELICK GWAJE (POPOTE MLIPO)**

Mnaarifiwa kuwa Maombi Na. 14/2022 yamepangwa kutajwa tarehe 02/06/2022 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, R. Mtei saa 2:00 asubuhi.
Hivyo, mnaamuriwa kuhudhuria kuhudhuria nyinyi wenyewe/ mwakilishi wenu mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Msipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.
AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 12/05/2022.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
BUKOBA

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie: 0782253676*

**KWA HABARI MOTOMOTO USIKOSE GAZETI LAKO LA NIPASHE KILA SIKU**

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI MICHEZO

# DTB FC 'YABATIZWA', SASA KUITWA SINGIDA BIG STAR

Na Saada Akida

BAADA ya kupanda daraja sasa ikijiandaa kushiriki Ligi Kuu Bara msimu ujao, DTB FC imebadilishwa jina ambapo sasa itaitwa Singida Big Star huku ikitumia Uwanja wa Liti (zamani Namfua) uliopo mkoani Singida, imeelezwa.

**Singida Big Star (DTB FC) na Ihefu FC ya Mbarali, Mbeya, zimepanda moja kwa moja Ligi Kuu zikitokea Ligi ya Championship msimu huu.**

Mtendaji Mkuu wa timu ya Singida Big Star, Muhibu Kanu ndiye aliyetangaza 'ubatizo' huo wa jina jana huku pia akimtangaza Hussein Massanza kuwa msemaji wa klabu hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kanu alisema awali timu hiyo ilikuwa inatumia jina la DTB FC na lakini sasa imebadilishwa jina na itakuwa ikijulikana kama Singida Big Star huku ikitumia Uwanja wa Liti.

Alisema hatua hiyo ya kubadilisha jina kutoka DTB FC hadi Singida Big Star ni kwa sababu awali ilikuwa chini ya Benki ya DTB, lakini sasa ipo chini ya kampuni nyingine.

"Kwa sasa DTB FC itajulikana kwa jina Singida Big Star na kutumia Uwanja wa Liti uliopo Namfua, Singida pia leo tumemtambulisha rasmi ofisa habari wetu, Hussein Massanza," alisema Kanu.

Alisema kuhusu usajili wako katika mchakato wa kupitia ripoti ya benchi la ufundi kwa kufanya usajili mkubwa katika timu yao ya msimu ujao wa Ligi Kuu.

"Mikakati iko vizuri, tutafanya usajili mzuri na kuwa tishio kwa msimu ujao, Singida hii ya sasa si ile ambayo ilishuka misimu miwili iliyopita," alisema Kanu.

Alisema timu hiyo itakuwa ya kila mtu, na kwamba haijawekeza kwa upande mmoja licha ya maamuzi kutolewa katika bodi ya kuhakikisha timu hiyo inafanya vizuri.

MAANDALIZI...



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Wanawake ya Tanzania Bara, Twiga Stars, wakiwa mazoezini katika Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba, Kagera jana, kujiandaa na mashindano ya CECAFA Chalenji Wanawake yanayotarajiwa kuanza kesho nchini Uganda. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Tembo Warriors kuelekea Poland wiki ijayo

Na Saada Akida

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Hassan Abbas, amesema mchakato wa safari ya timu ya Taifa ya Watu wenye Ulemavu, Tembo Warriors, kwenda nchini Poland, tayari umekamilika na kikosi hicho kitaondoka wiki ijayo.

Tembo Warriors inatarajia kuondoka Jumatano ijayo kuelekea Poland kushiriki mashindano ya Ulaya 'Amp-Futbal Europe 2022', ambayo yanatarajiwa kufanyika kuanzia Juni 10-13, mwaka huu katika mji wa Warsaw nchini humo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Dk. Abbas, alisema serikali iko imara zaidi katika kuhakikisha timu za taifa za michezo yote zinapata mahitaji yote na kwamba itahakikisha Tembo Warriors inakwenda kushiriki mashindano hayo.

Alisema safari ya Tembo Warriors mambo yanaenda vizuri na tayari mchakato umekamilika kwa asilimia kubwa, hivyo itakapofika tarehe husika iliyopangwa itaondoka nchini kwenda kucheza michuano hiyo ya kujiandaa na mashindano ya Kombe la Dunia, Oktoba mwaka huu.

"Nikiwa miongoni mwa viongozi wa Kamati ya Mashindano kwa timu za Taifa, tunaendelea vizuri na timu zote zinapata mahitaji yote ikiwamo kuziwezesha kufanikiwa malengo yao. Kwa Tembo Warriors kwenda Poland, ngumi na riadha kwenda kushiriki mashindano ya Jumuiya ya Madola," alisema Dk. Abbas.

Alisema licha ya timu hizo, lakini pia wako katika kampeni ya timu ya Taifa ya Wasichana chini ya umri wa miaka 17, Serengeti Girls kufuzu kucheza Kombe la Dunia.

Kikosi cha Serengeti Girls kiliibuka na ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya wenyeji wao, Cameroon katika mchezo wa kwanza uliopigwa katika Uwanja wa Ahmadou Ahidjo jijini Yaounde.

Serengeti Girls itakuwa mwenyeji wa mechi ya marudiano itakayopigwa Uwanja wa Amaan visiwani Zanzibar na timu itakayopata matokeo ya jumla itafuzu moja kwa moja kushiriki Fainali za Kombe la Dunia kwa Wasichana chini ya umri wa miaka 17, mwaka huu nchini India.

# Coastal chereko tupu, Azam vilio

Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo

KOCHA Mkuu wa Coastal Union, Juma Mgunda, ameeleza furaha yake kwa kutinga hatua ya fainali ya Kombe la FA baada ya kuitupa nje Azam FC kwa mikwaju ya penalti 6-5, kwenye mechi ya nusu fainali iliyopigwa juzi katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Wakati Mgunda akitamba, Kocha Mkuu wa Azam Abdihamid Moallin, na msemaji wao, Thabit Zacharia 'Zaka Zakazi', wamesema haikuwa bahati yao, kwani walipata nafasi nyingi kipindi cha kwanza, lakini walishindwa kuzitumia.

"Mechi ilikuwa nzuri sana na ngumu, ilikuwa na ufundi mwingi, tulikuwa tunacheza na wachezaji wazuri na wazoefu, ndiyo maana hata kwenda dakika 120 sikushangaa, yote kwa yote vijana wamefanya kazi kubwa na tumepata matokeo mazuri na tumekwenda fainali," alisema Mgunda.

Baada ya ushindi huo amesema anakwenda kufayanyia kazi mapungufu yote yaliyoonekana kabla ya kucheza fainali dhidi ya Yanga, Julai 2, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha.

"Tunakwenda kucheza na timu nzuri na yenye wachezaji bora, na wazoefu, Yanga, tunakwenda kujipanga na tutapambana nao," alisema kocha huyo.

Naye kocha wa Azam aliipongeza Azam FC, lakini akidai wachezaji wake walipoteza nafasi kadhaa kipindi cha kwanza, wakawa chini kipindi cha pili na nyongeza, lakini kuhusu penalti alidai huwa ni nusu kwa nusu na ni bahati pia.

Maneno kama hayo yalisema pia na msemaji wa timu hiyo, Zaka Zakazi.

"Tuwapongeze kwanza Coastal, kila timu iliihitaji nafasi hiyo, lakini wameipata wao, dakika 30 za kwanza tungeweza kuua mechi, dakika ya pili Lusajo Mwakenda alikosa bao, Mudathir Yahaya na Kenneth Muguna nao walikosa, hata Rodgers Kola, tungeweza kuwa mbele kwa mabao 4-0 hadi mapumziko, haikuwa siku yetu. Lengo lilikuwa ni kuchukua taji lolote msimu huu, lakini hatukufanya hivyo, sasa tunarudi kwenye ligi kufanye vema kwa ajili ya kuisaka nafasi ya tatu," alisema Zakazi.

## ZISIKUPITE

### MANE KUONDOKA LIVER

MSHAMBULIAJI wa kimataifa wa Senegal anayekipiga Liverpool, Sadio Mane mwenye umri wa miaka 30, ataiarifu klabu yake hiyo, matamanio yake ya kuondoka msimu huu wa majira ya joto. ***(Fabrizio Romano)***

### TORRES HUYO UNITED

BEKI wa Villarreal na Hispania, Pau Torres mwenye umri wa miaka 25, anakaribia kuhamia Manchester United baada ya wakala wake kusafiri kwenda England kuendelea na mazungumzo ya uhamisho huo. ***(Cadena Ser, kupitia Mirror)***

### ADAMU ATAKIWA WEST HAM

WEST Ham na Southampton wanafuatilia maendeleo ya mshambuliaji wa Red Bull Salzburg na Austria, Junior Adamu mwenye umri wa miaka 20. ***(Mail)***

### MANE ANUKIA BAYERN

KLABU ya Bayern Munich inakaribia kufikia makubaliano ya pauni milioni 34 kwa ajili ya kumsajili Sadio Mane. ***(Matteo Moretto)***

### LEICESTER KWA GARNER

KLABU ya Leicester City ina nia ya kumsajili kiungo wa kati wa Manchester United, James Garner baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, kuonyesha kiwango kizuri alipokuwa kwa mkopo Nottingham Forest. ***(Mirror)***

### ARSENAL KUMUUZA LENO

ARSENAL wameiambia Benfica mlinda mlango wa Ujerumani, Bernd Leno mwenye umri wa miaka 30, anauzwa kwa pauni milioni 8.5. ***(Sun)***

### RAPHINHA KWENDA UNITED

MSHAMBULIAJI wa Leeds United raia wa Brazil, Raphinha mwenye umri wa miaka 25, huenda akapendelea kuhamia Manchester United badala ya Barcelona. ***(Express)***

### BUTLAND AIVUTIA RANGERS

KLABU za Bournemouth na Rangers zinavutiwa na kipa wa Crystal Palace na timu ya Taifa ya England, Jack Butland mwenye umri wa miaka 29. ***(Sun)***

### DEMBELE NA LIVERPOOL

KLABU ya Liverpool imewasiliana na wawakilishi wa winga wa Barcelona, Mfaransa Ousmane Dembele mwenye umri wa miaka 25. ***(Sport)***

### EDWARDS AGOMBEWA EPL

ASTON Villa na Southampton ni miongoni mwa klabu kadhaa zinazomwania beki wa Peterborough, Ronnie Edwards mwenye umri wa miaka 19. ***(Sun)***

### CELSO AWEKWA SOKONI

KLABU ya Tottenham Hotspur imewaambia Villarreal kuwa wanataka pauni milioni 17 ili kumuuza kiungo wa kati wa Argentina, Giovani Lo Celso mwenye umri wa miaka 26. ***(Sun).***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI ULAYA




# BENZEMA ANASTAHILI BALLON D'OR - HENRY

**●●● Nilitaka tu kusema kitu kwa France Football au yeyote anayepiga kura, funga kura, ameshinda...**

**PARIS,** Ufaransa

THIERRY Henry amesema mbio za kuwania Ballon d'Or zimemalizika baada ya Karim Benzema kunyanyua taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Real Madrid.

**Benzema amekuwa nahodha wa pili wa Ufaransa kubeba taji hilo, baada ya Didier Deschamps akiwa na Marseille mwaka 1993, kutokana na ushindi wa bao 1- 0 dhidi ya Liverpool kwenye Uwanja wa Stade de France.**

Vijana wa Carlo Ancelotti walikuwa na deni kubwa kwa ushujaa wa Thibaut Courtois baada ya kipa huyo kuokoa hatari tisa. Vinicius Junior alifunga bao la ushindi mjini Paris na kuipa Madrid Kombe la 14 la Ulaya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, alifunga hat-trick dhidi ya Paris Saint-Germain, mabao manne dhidi ya Chelsea na matatu kwenye sare na Manchester City, ikiwa ni pamoja na penalti ya muda wa ziada na kushinda nusu fainali.

Benzema amehusika katika mabao 59 msimu huu (mabao 45, asisti 15) katika michuano yote, huku mchezaji mwenzake wa Ufaransa, Kylian Mbappe (60) pekee akifunga jumla ya mabao hayo katika ligi tano bora za Ulaya.

Lakini nguli wa Arsenal, Henry anaamini kuwa Benzema alimaliza mjadala wa nani ashinde Ballon d'Or mwaka huu kwa mafanikio yake kule Paris.

"Nilitaka tu kusema kitu kwa France Football au yeyote anayepiga kura. Funga kura, Benzema ameshinda. Kwa heri," alisema Henry akiiambia CBS Sports baada ya fainali.

Kocha wa Ufaransa, Didier Deschamps atatumaini Benzema anaweza kuiongoza 'Les Bleus' kutwaa ubingwa wa Kombe la Dunia Novemba mwaka huu, na aliunga mkono maoni ya Henry kwa kupendekeza kwamba nyota huyo wa Madrid ashinde tuzo hiyo.

"Jibu ni rahisi: Ndio. Taji hili jipya na msimu wa michezo uliopatikana akiwa na timu yake, na kile alichoweza kufanya, alikuwa na maamuzi," alisema Deschamps akiiambia Telefoot.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 233,

MECHI KALI
THAILAND
VERSUS
BAHRAIN
1 | 2.14
X | 3.48
2 | 3.71

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# WAKALA WA KOULIBALY AIKATAA BARCELONA



**NAPLES,** Italia

WAKALA wa Kalidou Koulibaly, amesema beki huyo wa Napoli hayuko kwenye mazungumzo na klabu nyingine yoyote huku kukiwa na uvumi kuhusu uhamisho wa kwenda Barcelona.

Mkataba wa Koulibaly na kikosi hicho cha Luciano Spalletti unatarajiwa kumalizika Juni 2023, na kumeibuka uvumi kwamba, 'Blaugrana' wanaweza kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30.

Rais wa Napoli, Aurelio De Laurentiis, alikubali mapema mwezi huu kwamba mchezaji huyo wa kimataifa wa Senegal hangeweza kulazimishwa kubaki, baada ya beki huyo wa kati kusema "tutaona kitakachotokea mwishoni mwa msimu".

Spalletti atakuwa na hamu ya kumbakisha Koulibaly, baada ya Napoli kuruhusu mabao machache zaidi kwenye Serie A (31).

Fali Ramadani, wakala wa Koulibaly, amesema mazungumzo ya mteja wake kuhama ni mapema.

"Kuna uvumi mwingi, na ninataka kufafanua kwamba hatuko kwenye mazungumzo na klabu yoyote kwa ajili ya Koulibaly," alisema Ramadani akiliambia gazeti la Italia Corriere dello Sport.

"Tunasubiri kukutana na Napoli ili kuamua suluhu bora kwa pande zote mbili."



# Lewandowski usiondoke Bayern - Rummenigge

**MUNICH,** Ujerumani

ROBERT Lewandowski hawezi kuwa na matumaini ya kushinda mataji zaidi akiwa Barcelona na hivyo basi anapaswa kubakia Bayern Munich, huku hali ya sintofahamu kuhusu mustakabali wake ikiendelea.

Huo ni ujumbe kutoka kwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa zamani wa Bayern, Karl-Heinz Rummenigge, ambaye amewasihi wababe hao wa Bundesliga kumbakisha Lewandowski katika klabu hiyo.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Poland amefurahia msimu mwingine mzuri, akifunga mabao 35 katika mechi 34 za Ligi Kuu - hakuna mchezaji aliyefunga zaidi katika ligi tano bora za Ulaya zaidi yake.

Lakini Lewandowski, ambaye mkataba wake unaisha Juni 2023, amekuwa akihusishwa na Barca baada ya kufurahia msimu mwingine mzuri na kuisaidia Bayern kutwaa taji la ligi kwa mara 10 mfululizo.

Maswali yamebaki kuhusu mustakabali wake baada ya Lewandowski na wakala wake kusema kuwa hawakupokea ofa ya mkataba mpya, huku Bayern, kwa upande mwingine, wakisisitiza "ofa halisi" ilikuwa mezani.

Na Rummenigge anaar
kuwa timu yake ya zamani
ima ifanye kila liwezalo k
bakisha mchezaji huyo m
nye umri wa miaka 33.

"Naona mambo yak
yamelegea zaidi. Kuna jar
moja muhimu: Robert Lew
dowski ana mkataba am
hautaisha mwaka huu, la
mwaka ujao," alisema akii
bia BILD.

"Hiyo ina maana klabu
aweza kuamua nini cha ku
ya, iwe inamuuza au la. N
hani (Mkurugenzi Mtendaj
Bayern), Oliver Kahn alitu
maneno 'Lewandowski al
kuonyesha mlango umefu
wa, hatumuuzi!

## HABARI MICHEZO

.880,320

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 01/06/22 | 21:45 | Scotland vs Ukraine | 2.27 | 3.13 | 3.33 |
| 02. 01/06/22 | 21:45 | Italy vs Argentina | 2.82 | 3.02 | 2.41 |
| 03. 03.06.22 | 00:00 | Real Cartagena vs Leones FC | 2.68 | 3.02 | 2.53 |
| 04. 02.06.22 | 02:30 | Fortaleza CE vs Ceara CE | 2.24 | 3.16 | 2.97 |
| 05. 02.06.22 | 02:30 | USA vs Morocco | 2.24 | 3.18 | 3.33 |
| 06. 02.06.22 | 03:30 | CRB AL vs CSA AL | 2.39 | 2.91 | 2.96 |
| 07. 02.06.22 | 19:00 | Bulgaria vs North Macedonia | 2.54 | 2.98 | 2.93 |
| 08. 02.06.22 | 19:00 | Cyprus vs Kosovo | 3.25 | 3.15 | 2.25 |
| 09. 02.06.22 | 21:45 | Czech Republic vs Switzerland | 2.90 | 3.25 | 2.39 |
| 10. 02.06.22 | 21:45 | Spain vs Portugal | 2.24 | 3.25 | 3.15 |
| 11. 02.06.22 | 21:45 | Serbia vs Norway | 2.27 | 3.10 | 3.25 |
| 12. 02.06.22 | 21:45 | Slovenia vs Sweden | 3.21 | 3.11 | 2.29 |
| 13. 02.06.22 | 21:45 | Northern Ireland vs Greece | 2.85 | 3.00 | 2.60 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### JUMANNE - 31/05/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:45 | 4895 | Albirex Niigata (SIN) vs Young Lions | 1.21 | 6.61 | 8.36 |
| 15:00 | 3120 | Thailand vs Bahrain | 2.14 | 3.48 | 3.28 |
| 15:00 | 5433 | Perth SC vs Armadale SC | 1.49 | 4.48 | 4.87 |
| 17:00 | 3920 | Nassaji Mazandaran vs Teraktor Sazi | 2.90 | 2.38 | 3.30 |
| 18:30 | 4105 | Honka W vs Aaland Utd W | 5.07 | 4.29 | 1.49 |
| 18:45 | 4865 | CR Belouizdad vs US Biskra | 1.16 | 5.83 | 15.56 |
| 19:45 | 3057 | Vastra Frolunda IF vs BK Astrio | 2.32 | 4.08 | 2.36 |
| 20:00 | 1239 | Gyori Eto W vs Ferencvarosi TC W | 5.05 | 4.66 | 1.46 |
| 20:00 | 1426 | Excursionistas W vs Deportivo Espanol | 1.82 | 3.70 | 3.56 |
| 20:00 | 1540 | Grorud IL 2 vs Ready | 2.24 | 3.99 | 2.48 |
| 20:00 | 1902 | Vllaznia vs Laci | 2.82 | 2.87 | 2.53 |
| 20:00 | 2053 | Tegs SK vs Umeaa FC | 7.81 | 5.27 | 1.28 |
| 20:00 | 3788 | Kjelsaas 2 vs Skeid Fotball 2 | 4.85 | 4.85 | 1.45 |
| 20:30 | 1626 | IF Algarna vs IFK Ostersund | 3.84 | 3.84 | 1.73 |
| 21:30 | 3713 | Roma Youth vs Inter Youth | 2.07 | 3.65 | 2.92 |
| 23:00 | 2025 | Deportes Quindio vs Tigres FC (COL) | 1.55 | 3.41 | 6.23 |
| 23:00 | 2071 | UTC Cajamarca vs Escuela Municipal Deportivo Binacional | 2.11 | 3.40 | 3.01 |
| 23:00 | 4953 | Black Rock FC vs Western Mass Pioneers | 4.37 | 4.18 | 1.58 |

### JUMATANO - 01/06/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01:00 | 1979 | Arturo Fernandez Vial vs Union San Felipe | 2.49 | 2.89 | 2.84 |
| 01:00 | 4716 | Sport Recife vs Ponte Preta | 1.88 | 3.11 | 4.08 |
| 02:00 | 5456 | Atletico Bucaramanga vs Junior Barranquilla | 3.21 | 3.06 | 2.17 |
| 02:15 | 5809 | Ypiranga AP vs Independente EC AP | 2.90 | 3.75 | 2.18 |
| 03:00 | 1916 | CD Alianza Cotopaxi vs Imbabura Sporting Club | 2.20 | 2.88 | 3.37 |
| 03:30 | 4604 | San Luis Quillota vs Univ de Concepcion | 2.37 | 2.97 | 2.93 |
| 03:30 | 5671 | Bragantino SP vs Goias | 1.61 | 3.56 | 5.07 |
| 04:00 | 2790 | FC Edmonton vs Forge FC | 2.72 | 3.35 | 2.31 |
| 04:05 | 2107 | Atletico Nacional vs Millonarios FC | 2.30 | 3.06 | 2.96 |
| 12:00 | 1903 | Adamstown Rosebud FC vs Lambton Jaffas | 9.40 | 6.40 | 1.24 |
| 12:00 | 4482 | Valentine FC vs Hamilton Olympic | 4.17 | 4.17 | 1.61 |
| 16:00 | 1198 | Australia U23 vs Kuwait U23 | 1.28 | 4.87 | 8.97 |
| 16:00 | 5395 | Belarus U21 vs Cyprus U21 | 2.22 | 3.26 | 2.92 |
| 16:00 | 5916 | Iran U23 vs Qatar U23 | 2.14 | 2.96 | 3.39 |
| 18:30 | 3973 | France U18 vs Saudi Arabia Youth | 1.27 | 5.60 | 9.40 |
| 18:30 | 4734 | Uzbekistan U23 vs Turkmenistan U23 | 1.16 | 6.02 | 14.57 |
| 19:00 | 5244 | Poland vs Wales | 1.80 | 3.46 | 4.41 |
| 20:00 | 2626 | Jordan U23 vs Iraq U23 | 2.84 | 2.89 | 2.49 |
| 20:00 | 3369 | Australia vs Jordan | 1.93 | 3.33 | 4.14 |
| 20:00 | 5133 | Faroe Islands U21 vs Ukraine U21 | 6.22 | 4.18 | 1.43 |
| 21:45 | 1649 | Scotland vs Ukraine | 2.31 | 3.14 | 3.24 |
| 21:45 | 4468 | Italy vs Argentina | 2.77 | 2.97 | 2.48 |
| 22:00 | 2568 | Tenerife vs Las Palmas UD | 2.45 | 3.03 | 2.93 |

### ALHAMISI - 02/06/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 02:00 | 5096 | La Equidad vs Envigado FC | 1.80 | 3.12 | 4.49 |
| 02:30 | 1190 | Fortaleza CE vs Ceara CE | 2.23 | 3.07 | 3.07 |
| 02:30 | 2072 | USA vs Morocco | 2.28 | 3.22 | 3.22 |
| 03:30 | 4877 | CRB AL vs CSA AL | 2.39 | 2.91 | 2.96 |
| 13:00 | 2663 | Japan vs Paraguay | 1.82 | 3.49 | 4.45 |
| 14:00 | 2867 | South Korea vs Brazil | 7.10 | 4.46 | 1.44 |
| 16:00 | 2808 | South Korea U23 vs Malaysia U23 | 1.10 | 6.83 | 21.47 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# MWAMNYETO: YANGA WOTE TUNA KIU KALI YA MAKOMBE

**Na Adam Fungamwango**

NAHODHA wa Yanga, Bakari Mwamnyeto, amesema kujituma kwa wachezaji pamoja na sapoti wanaoipata kutoka kwa mashabiki ni kwa sababu wote wana kiu ya kutwaa makombe baada ya muda mrefu kupita.

**Mwamnyeto amesema kwa sasa hisia za wachezaji wa Yanga na mashabiki zinafanana, na kila upande una kiu ya makombe, ndiyo maana mashabiki wamekuwa na hamasa kubwa, wakijazana na kuwapa sapoti kila wanapopita na kwenda kucheza, na hiyo ipo hata kwa wachezaji.**

"Watu wanavyotushangilia tunahisi tuna deni kubwa, kwa sababu wachezaji wengi tuliokuja Yanga tuna kiu ya kuchukua makombe, na mashabiki wana kiu, sasa hisia zetu zinaonekana kwenda sawa, wao wana kiu na sisi pia, nina imani mwaka huu tukichukua makombe yote, mashabiki watafurahi kama sisi tutakavyofurahi," alisema Mwamnyeto.

Alisema misimu yote minne ambayo walikuwa wakitoka kapa, ilikuwa inawaumiza, lakini wana uhakika msimu huu wa kutwaa taji moja au mawili, huku yeye akiwa ndiye nahodha atakayepokea makombe hayo.

Alisema kabla ya mechi dhidi ya Simba alikaa na wachezaji wenzake akiwa kama nadhodha na kumwambia Fiston Mayele kuwa atakabwa sana kama ilivyo kawaida, lakini wakamwandaa Feisal Salum kwa ajili ya kupiga mashuti ya mbali kutokana na kipaji alichojaaliwa.

"Tukamwambia wewe ndiye utakuwa msaada mkubwa kwa sababu jamaa nyuma watakuwa wanamkaba sana Mayele, ukipata nafasi piga, na kweli akapata mbili, moja ikatoka nje, moja ikatinga kambani," alisema.

Mwamnyeto alisema awali walikuwa wakishutumiwa kuwa wanakata pumzi kupindi cha pili, lakini kwa sasa timu wanazocheza nazo ndizo zinakata pumzi.

"Kwa sasa hatukati pumzi, timu tunazocheza nazo ndizo zinachoka, sisi mwanzo mwisho, na kilichotusaidia msimu huu hatudharau timu, yoyote anayekuja sisi mchakamchaka ule ule," alisema Mwamnyeto aliyesajiliwa misimu miwili iliyopita kutoka Coastal Union, timu ambayo timu yake ya sasa inatakiwa kucheza nayo fainali ya Kombe la FA Julai 2, mwaka huu katika Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

Wakati Yanga ikiichapa Simba bao 1-0 kwenye mechi ya nusu fainali iliyochezwa Uwanja wa CCM Kirumba Mwanza Jumamosi iliyopita, Coastal Union iliiondosha Azam FC kwa mikwaju ya penalti 6-5 kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha baada ya dakika 120 za suluhu.



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Tanzania, 'Taifa Stars' wakiwa mazoezi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi, kujiandaa na michezo ya kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2023 dhidi ya Niger na Algeria itakayochezwa Juni 4 ugenini na Juni 8 nyumbani kwa Mkapa. **PICHA: TFF**

# *Taifa Stars kuifuata Niger Alhamisi*

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha Timu ya Taifa, Taifa Stars kinatarajia kukwea pipa keshokutwa, Alhamisi kuifuata Niger tayari kwa mechi itakayopigwa nchini Benin Jumamosi wiki hii, kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON) 2023 zitakazofanyika nchini Ivory Coast.

Baada ya mechi hiyo, Stars itarejea nyumbani, tayari kuikaribisha Algeria katika mechi itakayopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Juni 8, mwaka huu.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Shirikisho la Soka nchini (TFF), Taifa Stars ambayo ilianza mazoezi mwishoni mwa wiki, itaendelea kujifua katika Uwanja wa Benjamin Mkapa hadi kesho kabla ya Alhamisi kukwea pipa kuelekea Benin tayari kwa mechi hiyo.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Clifford Ndimbo, jana aliliambia gazeti hili kuwa wachezaji wote walioitwa na Kocha Mkuu, Kim Poulsen kwa ajili ya michuano hiyo, tayari wameingia kambini na kuanza mazoezi.

"Wachezaji wote wameingia kambini ikiwamo wanaocheza soka la kulipwa nje ya nchi, na wameanza mazoezi kwa ajili ya mechi hizo," alisema.

Kuhusu mlinda mlango namba moja wa Stars, Kipa wa Simba, Aishi Manula, ambaye aliumia kidole na kushindwa kuitumikia klabu yake katika mechi mbili zilizopita dhidi ya Geita Gold FC kwenye Ligi Kuu Bara na dhidi ya Yanga katika mchezo wa nusu fainali ya Kombe la FA, Ndimbo alisema naye amejiunga na wenzake kambini na anaendelea na mazoezi.

"Aishi Manula yupo kambini na anaendelea na mazoezi na wenzake, kama kutakuwa na taarifa tofauti daktari wa timu akitoa tutawaeleza," alisema.

Michezo
Jumanne Mei 31, 2022
Nipashe



'Benzema anastahili Ballon d'Or'
UKURASA 21



Rais wa Heshima na Mwekezaji wa Klabu ya Simba, Dk. Mohamed "Mo" Dewji. **PICHA: MAKTABA**

# Yanga na hesabu kali kwa Coastal

**Na Shufaa Lyimo**

MKURUGENZI wa Mashindano wa Klabu ya Yanga, Thabit Kandoro, amesema baada ya kuitoa timu ya Simba kwenye michuano ya Kombe la FA, kwa sasa wanaelekeza nguvu na akili katika mchezo ujao wa Ligi Kuu ya NBC dhidi ya Coastal Union kabla ya kukutana nao katika mchezo wa fainali ya kombe hilo la Shirikisho la Soka nchini.

Coastal Union juzi iliitupa nje Azam FC kwa mikwaju ya penalti 6-5 baada ya dakika 120 kumalizika kwa suluhu kwenye mechi ya nusu fainali ya pili iliyopigwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, hivyo sasa itavaana na Yanga Julai 2, mwaka huu katika fainali itakayochezwa uwanjani hapo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Kandoro alisema mikakati yao ni kuhakikisha timu yao inafanya vizuri katika michezo yote ya Ligi Kuu ya NBC iliyobakia, ambapo baada ya mapumziko ya Kalenda ya Fifa, Juni 15, mwaka huu Yanga itaikaribisha Coastal Union katika Uwanja wa Benjamin Mkapa kwenye mechi ya Ligi Kuu.

"Mikakati tuliyojiwekea ni kuhakikisha tunashinda ule mchezo wetu wa Ligi Kuu ya NBC tutakapokutana nao kabla ya kukutana nao tena katika mchezo wa fainali," alisema Kandoro ambaye kikosi chao kiliitoa Simba katika mechi ya nusu fainali kwa kuichapa bao 1-0 kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza Jumamosi iliyopita.

Alisema mchezo huo ambao watacheza na timu ya Coastal utakuwa mgumu na wa ushindani hivyo inapaswa wapambane.

Yanga kwa sasa ipo kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo, ikiwa na pointi 64, 13 zaidi mbele ya Simba iliyopo nafasi ya pili, hivyo vinara hao wanahitaji alama tatu tu katika mechi nne walizobakiza msimu huu ili kutawazwa mabingwa.

# Mo anguruma tena Simba

## Amwaga mikakati mipya, mashabiki wamfuata kocha Mtunisia wa viungo, Adel Zrane, asema...

**Na Saada Akida**

RAIS wa Heshima na Mwekezaji wa Klabu ya Simba, Dk. Mohamed "Mo" Dewji, amenguruma na kutoa yake ya moyoni baada ya miamba hiyo kutokuwa na msimu mzuri, huku akieleza hawapaswi kurudi nyuma na badala yake kuboresha pale kwenye mapungufu.

**Simba msimu huu haukuwa mzuri kwao baada ya kupoteza mataji yote mawili ikiwamo Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC) maarufu FA Cup na Ligi Kuu Tanzania Bara, ambalo licha ya msimu kutomalizika, lakini kuna zaidi ya asilimia 95 ya kulipoteza kutokana na watani wao wa jadi, Yanga kuhitaji pointi tatu tu katika michezo minne iliyobaki ili kutwaa taji hilo.**

Simba ambayo taji pekee ililotwaa msimu huu ni Kombe la Mapinduzi Januari mwaka huu visiwani Zanzibar, baada ya kutolewa Ligi ya Mabingwa iliangukia Kombe la Shirikisho Afrika ambako nako ilitolewa hatua ya robo fainali na Orlando Pirates ya Afrika Kusini.

Lakini pia, ilifungua msimu huu vibaya baada ya kuukaribisha kwa kuanza kupoteza Ngao ya Jamii, dhidi ya watani wao, Yanga.

Taarifa kutoka Idara ya Habari na Mawasiliano ya Klabu Simba, Mo Dewji amesema miaka mitano iliyopita walikuwa na mafanikio makubwa na bajeti iliongezeka mara tano na kusababisha kushinda mataji ya ndani na kuacha alama kimataifa kwa kufika robo fainali tatu za michuano ya Afrika.

Alisema baada ya mafanikio hayo, lazima kikosi kifanyiwe marekebisho kadhaa kutokana na wachezaji kutumia muda mrefu ili kurudi katika mstari wa kuendelea kupambania mataji kwa msimu ujao wa ligi na kufanya vizuri michuano ya kimataifa.

"Hakuna kurudi nyuma, tunatakiwa kufanya mabadiliko katika maeneo ambayo kuna upungufu na kwenda mbele, mapambano yanaendelea wala hakuna kukata tamaa.

"Najivunia kusema tupo katika orodha ya klabu bora 12 barani Afrika, hii imekuwa mara ya kwanza Simba kuwa na mwendelezo mzuri katika miaka 86 ya historia yetu, hatupaswi kubweteka badala yake kupambana kufikia malengo tuliyojiwekea," alisema Mo Dewji.

Alisema huu umekuwa msimu ambao ni mbaya zaidi kwa Simba katika kipindi cha miaka mitano iliyopita na kwamba wachezaji walikosa ari, shauku na njaa ya kushinda makombe msimu huu.

"Bodi inahitaji kufanya maamuzi magumu msimu huu na kutafuta njia ya kusonga mbele, tunahitaji kurekebisha timu na mkakati wa usajili msimu ujao katika kutwaa makombe yaliyopo mbele yetu," alisema Mo Dewji.

Wakati huo huo mashabiki wa Simba wamemfuata aliyekuwa kocha wa viungo wa timu hiyo, Adel Zrane na kutaka kurejea kuinoa timu hiyo

Akizungumza na gazeti hili kwa njia ya simu Zrane, alisema amepokea ujumbe kutoka kwa mashabiki na ana imani iko siku atarejea kufanya kazi ndani ya klabu hiyo.

"Naipenda Simba na msimu ujao ninaimani nitarejea ndani ya klabu hiyo, tuko pamoja," alisema Zrane, ambaye ni raia wa Tunisia.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >